# KITABU CHA MISINGI YA BIBLIA

Carelinks, PO Box 152, Menai NSW 2234 AUSTRALIA www.carelinks.net email: info@carelinks.net

# YALIYOMO

1) Biblia
2) Mungu
3) Mpango na nia ya Mungu
4) Mauti
5) Ahadi za Mungu
6) Bwana Yesu Kristo
7) Ahadi ya Mungu kwa Daudi
8) Ufufuo wa Yesu
9) Kurudi kwake Yesu Kristo
10) Injili
11) Ubatizo
12) Ufalme wa Mungu

# MBINU YA KUJIFUNZA

Mfululizo huu wa masomo 12 umekusudiwa kukusaidida upate msingi wa ufahamu wa mafunzo ya Biblia na jinsi unavyoweza kuwafaa wengine kwa Ukristo wako. Utafikia upeo wa faida ya masomo haya kwa kuyapitia mara kadha na kwa kutafuta vifungu vilivyopendekezwa kutoka katika Biblia. Kisha ujibu maswali yanayohitaji uchaguzi mwishoni mwa kila somo , huku ukirejelea uliyoyasoma ukiwa na shaka na majibu yako. Hapana haja ya kupurukusha masomo na kukisia majibu ; maelezo yaliyotolewa ni yanakifu kukuwezesha kujibu maswali yote kwa usahihi , na yawe msingi wa kwa masomo ya juu zaidi yatakayokufuatia.

Ukisha kamilisha maswali yote ya masomo 12, hamisha majibu yako kwa shiti ya muhtasari wa majibu iliyo katikati ya kijitabu hiki. Masomo yakishakamilika tuma shiti ya muhtasri kwa anwani iliyoonyeshwa . Tukipata majibu yako utapata mwalimu wako atakayesahihisha na kukurejeshea, huku akitoa maelezo ya ziada yanayofaa pamoja na kitabu cha Misingi ya Biblia ambacho kina masomo 11 katika kurasa 408 ili kukufunulia mafunzo zaidi ya Biblia.

Ukiwa na maswali yoyote juu ya mambo yanayohusu Biblia, tutafurahia kukusaidia kuyapata majibu kutoka katika Biblia

........................

# Mafunzo ya mwanzo / utangulizi

Nia ya kitabu hiki cha Misingi ya Biblia ni kukuwezesha uwe na masomo ya mfululizo ya Biblia kibinafsi. Mwisho wa masomo, utaweza kupambanua kwa uwazi injili ya kimsingi aliyofunza Yesu. Aliamuru wanafunzi wake waihubiri Injili ulimwenguni mwote, na kuwabatiza waumini kwa kuwachovya majini- kwa mfano mauti na ufufuo wake.Tuna matumaini kuwa kufikia mwisho wa masomo haya na yale yaliyo katika kozi ndefu, utakuwa umefikia kiwango cha kufanya uamuzi wa kuamini injili ili ubatizwe. Hapa ulipo ni mwanzo tu, kwa hakika safari imeanza. Omba dua kama uwezavyo Mungu aweze kukufunulia ufahamu wa neno lake. Mwambie juu ya masuala yanayojitokeza katika maisha yako na ujaribu kuangalia anavyokuongoza kupitia kwa neno lake huku akikuleta karibu naye.

Mwisho wa kila somo kuna maswali. Waweza kutoa rai yako au uulize swali kuhusu jambo lolote la kibiblia . Ni furaha yetu kuwasiliana nawe juu ya mambo haya. Anwani imetolewa katika kijitabu hiki.

Kuna Masomo 12 katika mafunzo haya ya utangulizi/mwanzo . Baada ya haya kuna masomo 11 zaidi yaliyo na maelezo marefu katika kitabu cha kurasa 408 kiitwacho "Misingi ya Biblia."
Tutakutumia kitabu hicho pindi ukamilishapo masomo haya 12. . Haya yote yatolewa pasi na kuyagharamia. Hutozwi hela zozote , twakuhakikishia kama ungependa kukutana na mmoja wetu kwa minajili ya majadiliano, twambie kwani kuna uwezekano wa mmoja wetu kuwa maeneo yako.

Tunakujali vilivyo na twataka kukusaidia ili upate nafasi katika Ufalme wa milele wa Mungu hapa duniani,Yesu arudipo. Kwa hivyo twakuombea dua njema, na twatarajia kupokea majibu. kutokana na mafunzo haya na pia rai au maoni yako kuyahusu.

# Biblia

Biblia ina madai mengi. Yaeleza bayana kuwa mwandishi ni Mungu- Muumba ulimwengu. Inadai kutufunulia Mungu ni nani na nia yake ni ipi kwa kupaza sauti. Kama madai haya hayawezi kukubalika basi Biblia itakuwa imechezea wanadamu shere kwa ulaghai uliokiuka mipaka.Ikiwa madai ya Biblia yataungwa mkono, basi tutakuwa tumepata tunu ya ajabu ulimwenguni.

Biblia, kama Neno la kweli la Mungu, ina ufunguo wa amani na furaha. Inatoa majibu kwa masuala yanayowasumbua wanadamu sana kuhusu maana na sababu ya kuwepo kwetu na hatima ya ushindani kati ya wema na maovu.

## HEBU TUANGALIE KWA MAKINI MADAI YAKE

Paul alipokuwa akiandika kuhusu Agano la Kale anasema," Kila andiko,lenye pumzi ya Mungu " (2Tim2:16). Kila neno la miswada ya asili iliandikwa kwa uongozi wa Mungu. Mtume Petro alitilia mkazo jambo hilo. "Maana unabii haukuletwa popote kwa mapenzi ya mwanadamu: bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu,wakiongozwa na roho mtakatifu" (2 Petro 1:21)
Mitume hawa wawili wanadai kuwa maandiko ya Agano La Kale ni kazi ya mamlaka ya Mungu.Mamlaka haya ya Mungu ndiyo sababu hasa ya ulinganifu mwafaka wa mafunzo yaliyofunuliwa katika Biblia Ingawa waandishi walitengwa kwa wakati, elimu, kazi, ujuzi na tabaka tofauti maishani; maandishi yao ni kusanyiko la kitabu kimoja hasa.

**KWA NINI BIBLIA ILIANDIKWA**
Biblia inatuambia jinsi jamii ya mwanadamu ilivyoanza na vile mpango wa Mungu wa wokovu ulivyo kuhusu ushindi wa wema juu ya mabaya utakavyoangamiza kabisa dhambi na uovu. Nia muhimu ya Biblia ni kuonyesha kizazi cha mwanadamu kilicholaaniwa kitakavyopata wokovu kupitia kwa Yesu Kristo.
Agano La Kale na Agano Jipya zinaungana na kumwonyesha Yesu kama Mwokozi wa pekee wa wanadamu.

Katika kurasa za Biblia tunapata mafunzo ambayo yanamwelimisha mwanadamu kuhusu ufafanuzi wa Mungu juu ya wema na uovu, na wajibu wa mwanadamu kwa Mungu na kwa mwanadamu mwenziwe (2Timotheo 3:15-17).
Hatimaye tumepewa Biblia itwambie kwa upana mambo ya usoni ili tupate kujitayarisha kwa kuja kwa Kristo (2Petro 1:19)

YALIYOMO BIBLIANI
Biblia ni mkusanyiko wa vitabu vilivyogawanywa katika sehemu mbili kuu. Vitabu vya Agano La Kale viliandikwa kabla ya kuwepo Kristo na vya Agano Jipya baada ya wakati wa

Yesu Kristo.Kuna vitabu 66 kwa ujumla. Utapata orodha ya vitabu hivi mwanzo wa Biblia yako. Viliandikwa na takriban waandishi 40 kwa muda unaozidi miaka 1500. Vitabu hivi viliandikwa katika nchi mbalimbali kama vile Israeli, Misri, Utaliano na Babiloni
Vitabu vyote vinaunganika katika wazo moja - wazo la utendaji kazi wa Mungu na nia yake kwa mwanadamu- tangu hapo, kama ilivyonukuliwa katika kitabu cha Mwanzo hadi "Ufalme wa dunia umekwisha kuwa ufalme wa Bwana wetu na wa Kristo wake ,naye atamiliki hata milele na milele" (Ufunuo 11:15)

AGANO LA KALE

Vitabu vya Agano La Kale viko katika sehemu nne kuu:-

a) VITABU VYA MUSA

Kitabu cha kwanza kinaitwa Mwanzo, ikiwa na maana ya utangulizi.
Inatueleza mahusiano yake Mungu na wanadamu wa kwanza duniani. Halafu vinafuata vitabu kama Kutoka, Mambo ya Walawi, Hesabu na Kumbukumbu la Torati. Vinasema jinsi Mungu alivyomwita Ibrahimu, akafanye agano naye pamoja na uzao wake, ambao aliwatoa Misri na kuwapa nchi inayoitwa Israel hivi leo.

b) VITABU VYA KIHISTORIA

Hivi, kuanzia kitabu cha Yoshua hadi kitabu cha Esta, ni rekodi ya historia ya Waisrael ( au Wayahudi) na mlahiki wa Mungu nao.

c) VITABU VYA KISHAIRI

Vitabu vya Ayubu, Zaburi, Mithali, Mhubiri na Wimbo Ulio Bora viliandikwa katika lugha ya Kiebrania (lugha ya Waisrael) katika mtindo wa kishairi. Vitabu hivi vina mafunzo muhimu kuhusu njia zake Mungu na hisia na wajibu wa mwanadamu.

VITABU VYA MANABII

Maana ya neno nabii ni mtabiri- aliye na utambuzi au maono, si ya matukio ya siku za usoni tu, bali pia matakwa yake Mungu kwa mwanadamu. Vitabu virefu vya unabii vya
Isaya, Yeremiah na Ezekiel vinafuatiwa na vingine vifupi.

AGANO JIPYA

a) REKODI ZA INJILI

Kuna maelezo mbalimbali kuhusu maisha ya Kristo, Kama yalivyoandikwa na Mathayo,Marko,Luka na Yohana; kila mmoja wao anaeleza injili (habari njema) kwa mtindo wake

b) KITABU KIITWACHO "MATENDO YA MITUME"

Kitabu hiki kiliandikwa na Luka na kinatoa maelezo kuhusu hali ilivyokuwa baada ya kufufuka kwake Yesu Kristo kutoka kwa wafu. Tunaambiwa jinsi makanisa ya mwanzo yalivyoanzishwa wakati mitume walipoeneza habari njema katika himaya nzima ya Ufalme wa Roma.

c) NYARAKA

Ziliandikwa na baadhi ya mitume kuwasaidia waumini wa mwanzo waliokuwa katika

makanisa madogo na machanga yaliyokuwa yameenea kote.

d) KITABU CHA UFUNUO

Huu ulikuwa ujumbe wa mwisho wa Yesu , uliotolewa kwa njia ya maono kwa Mtume Yohana.

YESU KRISTO ALIAMINI KILA KITU KATIKA AGANO LA KALE

Yesu Kristo ni mtu wa maana katika mpango wa Biblia, na alipozaliwa, Agano Jipya haikuwepo. Maandiko aliyoyatumia na kudurusu yalikuwa yale ya Agano La Kale. Yesu aliyakubali maandiko haya, alifunza kwa kuyategemea na kuyakubali kama mamlaka yasiyokanika kwani ni ya kuaminika. Angalia vifungu vifuatavyo:

Yohana 5:46-47 ; Luka 24:27 ; Luka 24:44-48 ;
Mathyo 22:29 ; Marko 7:6-13

Yesu anawazungumzia akina Ibrahimu, Isaka,Yakobo,Daudi na Suleiman na kuhusu watu wengine tunaosoma habari zao katika Agano La Kale na kuonyesha alivyotegemea Agano La kale kwa mafundisho yake huku akidhihirisha wazi kuwa aliwatambua waliotajwa kama watu halisi na kuwa Agano La Kale lote ni Neno la Mungu.

BIBLIA HAINA UDANGANYIFU

Ustawi wa dhana ya kisasa na teknolojia imechangia kuthibitisha kuwa yaliyoandikwa katika Biblia ni sahihi. Adui wengi wa Biblia, kukiwepo watu wenye akili zao , wamejaribu sana kuonyesha udhaifu wake, lakini wameshindwa . Kwa kuwa ukweli hauwezi kujipinga/ kuhitilafiana , bila shaka twatarajia Neno la Mungu lichukuane na kanuni za taaluma ya kisayansi.

Ushahidi wa ziada wa mamlaka ya Biblia ni vile ambavyo imeweza kuhifadhiwa kwa karne kadha. Biblia imerejelea ushindi katika jitihada zote za binadamu kujaribu kuiangamiza. Imekandamizwa na watu yakhe kunyimwa matumizi yake ; matokeo mazima yameteketezwa na vitabu vingi vimeandikwa katika juhudi za kutoikubali . Hakuna kitabu kimepitia mchujo wa ukinzani wa mfulilizo hivi: Biblia yabaki imara pasi na kutetereka wala kushindwa.

Kale wa Biblia,uhifadhi wake na jinsi inavyoathiri jamii ya mwanadamu, ni vipengele ambavyo haviwezi kupuuzwa , Ushahidi wa wanaakiolojia wa watu kama Rawlinson,Layard, Smith , Woolley na Kenyon, katika Misri, Ninawi , Ashuri, Babilon, Uri, Siria , Lebanon na Israel ni thibitisho bayana ya ukweli wa historia ya Biblia. Vizibiti katika makavazi ulimwenguni mwote inadhihirisha haya yote : Maneno yaliyoandikwa kwenye minara ya ukumbusho ya mataifa yaliyopigana na Israel yanathibitisha maelezo ya matukio na desturi za kale na desturi za mitaani. .

Akiolojia ya kisasa yazidi kuchangia nyenzo zinazounga mkono sababu zetu za kuamini ukweli wa Biblia nzima. Hata ukosoaji unaotokana na utunzaji wa wanukuzi Wayahudi wa maandishi asilia yanatupiliwa mbali kwa ugunduzi wa miswada ya kale . Ugunduzi usio kifani wa mwaka wa1947 ya Hati za Bahari ya Chumvi imethibitisha zaidi ushuhuda wa thamani wa usahihi wa Biblia . Miswada hii ni baadhi ya ile ya mwanzo iliyopatikana , tangu karne ya pili baada ya kuzaliwa Masihi.

Licha ya umri wake , na mabaliko ya kiasi yanatokea ni yale ya tahajia na hayaathiri

mafundisho , unabii au ukweli wa historia.
Kwa hivyo kazi ya wanaakiolojia inathibitisha pasi na kifani ukweli na utegemezi wa Biblia na kwa hivyo ,kwa njia nyingine , kuonyesha ni mazao ya pumzi ya Mungu.

UNABII UNATHIBITISHA BIBLIA KUWA YA KWELI

Mungu mwenyewe ameteuwa unabii kama njia kuu ya kuthibitisha ukuu wake usio na kikomo kuwapita miungu wengine wote (Isaya 46:9-10; Isaya 42:9)

Biblia yazungumzia mambo ambayo hayana budi kutokea miaka mia kadha baadaye. Katika Mathayo 2 imerekodiwa kuwa Mamajuzi walikuja Yerusalemu na kuuliza , "Yuko wapi yeye aliyezaliwa mfalme wa Wayahudi?" Herodi alipowauliza wakuu wa Makuhani Swali hili , walijibu mara moja, "Katika Bethlehemu ya Uyahudi" kwa sababu miaka mia kadha kabla ya tukio hili ilikuwa imetabiriwa katika mojawapo ya vitabu vya Agano La Kale (Mika 5:2)

Kuongezea kwa unabii kumhusu Yesu Kristo, kuna wa ziada unaohusu mataifa ya kale, na hasa, kuwahusu Wayahudi: Mataifa mengi ya Kale yametoweka kutoka kwaramani au mambo ya ulimwengu , lakini Biblia ilisema Wayahudi wangesalia . Wayahudi wangalipo leo ingawa kumekuwepo na jitihada ya kuwaangamiza (Yeremia 30:10-11) . Kama Biblia ingekuwa kazi ya matokeo ya mwanadamu , jambo hili lingetokea kuwa la udanganyifu wakati wowote katika historia . Wayahudi wangalipo nasi hivi leo wakiwa na taifa lao,Israel, na mji wao mkuu, Yerusalemu, ukiwa chini ya mamlaka yao kabisa.
Biblia inatupa sababu za ukweli wa mambo haya . Hili ni thibitisho mwafaka kuonyesha kuwa Biblia ni kazi ya pumzi ya Mungu na kwa hivyo pasi na dosani /kosa.

MUHTASARI WA BAADHI YA SABABU YA KUFANYA BIBLIA IAMINIKE INA PUMZI YAKE MUNGU

1. Umoja wa ujumbe wake licha ya waandishi wengi walioandika kwa kipindi cha muda mrefu.
2. Uhifadhi wa kimuujiza.
3. Ushahidi wa ugunduzi wa wanaakiolojia.
4. Kutimizwa kwa unabii wa Biblia - (mifano zaidi itatolewa katika masomo yafuatayo)

MASHARTI YA KUKABILIWA

Ikiwa twataka kuilewa Biblia, Yesu alisema itatupasa tuwe wa kufunzika kama watoto wadogo,
Mathayo 11:25 Itatubidi kutaka kujua sisi wenyewe. ukweli na hekima ya neno la Mungu (Mithali 2:3-6). Inatupasa kuamini ya kuwa Mungu atatupa thawabu kwa utafiti wetu (Waebrania 11:6). Tuwe tayari kuyafanya maisha yetu yachukuane na amri zake mwenyezi Mungu.

Yesu alisema, " Mkiyajua hayo, heri ninyi mkiyatenda "( John 13:17) na , " si kila mtu aniambiaye , Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni ; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni "(Mathayo 7:21). Mtume Paulo aliandika , "Utimizeni wokovu wenu wenyewe kwa kuogopa na kutetemeka " ( Wafilipi 2:12).

TUSOMEJE BIBLIA?

Kama ilivyo udurusu wa kozi yoyote ile , usomaji wa kila mara na ulio na mpangilio mahususi ndio unaosaidia . Kwanza, fuata mapendekezo ya kudurusu yaliomo katika somo hili. Biblia yenyewe yajua kutoa tafsiri mwafaka . Kila mara angalia vifungu katika muktadha wake na linganisha Andiko kwa Andiko.

Unapopitia hizi kozi ,utaona ya kuwa kila msingi wa imani unaungwa mkono kwa udhahiri na wazi kabisa na Maandiko. Kwa utaratibu wa msingi huu vifungu vyovyote vinavyoonekana kuwa na "ugumu " au "kutilafiana" vyaweza kupata upatanifu au ulinganifu mwafaka .

Matumizi ya vitabu vilivyo na maneno muhimu ya Biblia yaliyopangwa kialfabeti, maelezo ya pembezoni au sherehe za Biblia zaweza kusaidia kwa kiasi fulani, lakini ikumbukwe ya kuwa watunzi wa kazi hizi hawakuongozwa kwa pumzi ya Mungu . Ikiwa hatima ya maoni yao inakinzana na mafundisho ya maandiko, wamepotoka (Isaya 8:20 )

Nia ya kozi hii ya masomo ni kukusaidia wewe binafsi kuweza kuifahamu Biblia mwenyewe , ili uikubali mwenyewe kama ilivyo, ni neno la Mungu lenye kutoa matumaini kwa wale wote watakaolisikia na kulitii.

VIFUNGU VYA KUSOMA KATIKA BIBLIA
2 TIMOTHEO 3:2 ; 1 PETRO
1 ; LUKA 24 ; ISAYA 8:20 :
LUKA 24 ; ISAYA 8:20 ;
MATENDO 28 :23-31 ; WAEFESO 4 : 21-32

KITIHANI CHA SOMO LA 1

Pigia mstari jibu lililo sahihi kwa kila swali lililoulizwa kisha uhamishe majibu hadi hati ya muhtasari ya majibu iliyo katikati ya kurasa za hizi.

1. Nani ndiye mwandishi wa Biblia ? a.Paulo b.Musa c.Mungu d. Danieli

2. Ni sehemu gani ya Agano la Kale iliyotumiwa na Yesu kuwaelezea wale wanafunzi wawili wakiwa njiani kwenda Emau kumhusu ? a.Maandishi ya manabii b. Maandishi ya Musa c. Zaburi d. Mithali

3. Hati za Bahari ya Chumvi ziligunduliwa lini? a.1749 b.1794 c.1947 d.1914

4. Mika alitabiri kuwa Yesu angezaliwa wapi? a.Yerusalemu b.Bethel c.Bethlehemu d. Babiloni

5. Vitabu vya Biblia viliandikwa katika kipindi kipatacho miaka: a.50 b.15 c.1500 d.150

6. Yesu alisema"mkitenda maneno haya heri ikiwa a.'mtawambia wengine' b.'mkiyatenda' c.'mtayakumbuka' d.'mtakuwa na hakika nayo'

7. Biblia ina vitabu vingapi kwa jumla? a.66 b.27 c.39 d.23

8. Ni neno lipi "imara zaidi" alilorejelea Petro katika waraka wake wa pili? a.tabia njema b.ya uimbaji c.ya unabii d.ya kuzungumza.

9. Paulo alikuwa akiishi mji gani wakati yaliyoandikwa katika Matendo 28:23-31 yaliporekodiwa? a.Urumi b.Yerusalemu c.Efeso d.Aleksandria

10. Twaweza kupata wapi ufahamu kuhusu mpango na nia ya Mungu kuhusu dunia? a.Hati za Bahari ya Chumvi b. Sheria za Kiyahudi c.Maandishi ya wanakiolojia d. Biblia Takatifu.

SOMO LA 2

MUNGU

Kuna ubishi mwingi kuhusiana na uwepo wa Mungu.

HOJA YA SAA

Tungeokota saa nzee, na tuwe hatujawahi kuona saa, labda twaweza kuiokota na kuichunguza ..Twaweza kufungua nyuma na kuangalia mashine yenye muundo tata.. Tungeweza kugundua magurudumu yanayofanya kazi kwa kushabihana zikiwezesha akraba kwenye uso wake kusonga.

Bila shaka tungefikia uamuzi kuwa kidude/mashine tatanishi hivi kiliundwa . Saa hii iliundwa kwa usanifu: lazima ilifanyiwa mpango. Saa haikujiunda . Na vijisehemu vyake vyote havikujikusanya pamoja kiajali . Kuwepo kwa hiyo saa ni ushahidi tosha kuwa kuna yule aliyeiunda - lazima tuna muunda saa.

Ulimwengu una mamilioni ya nyota. Dunia ina mwezi ambao huuzunguka. Jua na sayari ni sehemu ya mfumo tatanishi na wa kuajabia kwa kufuata utaratibu uliopangiwa. Kuna utata mkubwa hapa kuliko ule wa saa. Hii haikutokea kiajali. Pana msanii/mbuni."

USHAHIDI WA BIBLIA

Ubishi mkubwa kuhusu uwepo wa Mungu wapatikana katika Biblia. Biblia ina habari mahsusi kuhusu unabii juu ya kuibuka na kuanguka kwa falme na mataifa; kuhusu watu binafsi na matukio . Aghalabu unabii huu ulirekodiwa miaka kadhaa kimbele. Haya si mambo ambayo mwanadamu angetenda. Ni Mungu pekee, mdhibiti wa vitu vyote ambaye aliwezesha unabii huu kuandikwa. Angalia Isaya 40:9-10    Mambo mengine kuhusu utabiri huu yatajadiliwa katika mafunzo yajayo. Kiini kuhusu jinsi Mungu mwenyewe amejidhihirisha katika Biblia.

TUNACHOAMBIWA NA BIBLIA

Mungu amejidhihirisha kama Muumbaji. "Hapo mwanzo Mungu aliumba mbingu na nchi" (Mwanzo 1:1) "Maana nimeumba dunia, nimemhuluku mwanadamu juu yake;Mimi, naam, mikono yangu mimi, imezitanda mbingu, na jeshi lake lote nimeliamuru" (Isaya45:12).

Mungu amejidhihirisha kama wa kuishi milele. Amekuwepo na ataendelea kuwepo.

"Bali Bwana ndiye Mungu aliye hai, Mfalme wa milele...." (Zaburi 90:2.

"Kiti chako cha enzi kilianzishwa mapema zaidi ya wakati huo- na wewe milele wewe peke yake!" (Zaburi 93:2).

Kuna Mungu mmoja tu. Waisraeli walikumbushwa kila mara kuwa miungu ya Wamisri haikuwa na nguvu zozote kama ilivyo sanamu zinazoundwa na wanadamu.

“Maana miungu yote ya watu si kitu; lakini BWANA ndiye aliyeziumba mbingu” (1 Nyakati 16:26).

Mungu ni mweza yote .Anajua yote yanayotendeka na yu kila mahali kwa uwezo wa roho Wake.

“Wewe wajua kuketi kwangu na kuondoka kwangu; umelifahamu wazo langu tokea mbali……Umeelewa na njia zangu zote” (Zaburi 139:2-3).

Daudi katika Zaburi hii anaonyesha jinsi ambavyo akili zetu zilivyo finyu kuelewa ukuu wa Mungu (kifungu cha 6). Bali tukifahamu kuwa Mungu anayaona yote na kuyaelewa mambo yote itakuwa jambo la kutufajiri na kutupa nguvu mpya.

“Ningezitwaa mbawa za asubuhi, na kukaa pande za mwisho za bahari; huko nako mkono wako utaniongoza na mkono wako wa kuume utanishika” (Zaburi 139:9-10).

Biblia yatueleza kuwa Sikio la Mungu li tayari kila mara kuisikiliza kilio cha wana Wake na Mungu ametangaza, pia,

“Sitakupungukia kabisa, wala sitakuacha kabisa” (Waebrania 13:5; Yoshua 1:5).

# UMOJA WA MUNGU

Mafunzo ya Biblia kuwa Mungu ni mmoja ni muhimu, hasa kwa sababu kuna wengi wasioamini hili. Ni funzo bayana linalofunzwa katika Agano La Kale na hali kadhalika Agano Jipya. Angalia vifungu hivi- Isaya 45:5 ; 1 Wakorintho 8:6-9; Waefeso 4:6.
Mtume Paul alimwandikia Timotheo. Kwa sababu Mungu ni mmoja na mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu ni mmoja, mwanadamu Kristo Yesu” (1 Tim 2:5).

Yesu mwenyewe alitilia mkazo fundisho hili la Biblia aliposema, “Na uzima wa milele ndio huu, wakujue wewe Mungu wa pekee wa kweli na Yesu Kristo uliyemtuma” (Yohana 17:3).

# FUNZO LA UTATU

Mafundisho machache yanakubalika kwa urahisi na wengi kama vile lile linalohusu Uungu, funzo linalojulikana kama Utatu. Kanisa Katoliki, kanisa la Kiyunani, na takribani madhehebu yote ya Kiprotestanti, labda wasikubaliane katika vipengee fulani, wakubaliane kwa hili, na

hatimaye waamini ya kuwa 'Baba ni Mungu , Mwana ni Mungu, na Roho Takatifu ni Mungu, ingawa si Mungu watatu, ila ni Mungu mmoja.' Pia wanaamini ya kuwa wote watatu ni nguvu sawa na wadumu milele.

Je, hili ni fundisho sahihi? Ikiwa ni hivyo, ingawa hatulifahamu vema, ni lazima tulikubali? Tutajuaje? Bila shaka kwa yale tu ambayo Mungu mwenyewe ameridhia kutufunulia katika neno Lake . Kwa hivyo, tutaelekea Katika Biblia na twatambua mara kuwa hapana thibitisho la kuunga mkono funzo hili, bali lapata upinzani mkubwa. Maandiko yasisitiza umoja wa Mungu na sio utatu. Vifungu vinavyofuatia vyadhihirisha wazi mambo haya:

"Sikiza, Ee Israeli; BWANA, Mungu wetu, BWANA ndiye mmoja" (Kumb 6:4; Marko 12:29).
"Mimi ni BWANA, wala hapana mwingine, zaidi yangu mimi hapana Mungu" (Isaya 45:5).
"Lakini kwetu sisi Mungu ni mmoja tu, aliye Baba, ambaye vitu vyote vimetoka kwake" (1 Kor 8:6).

Hivi si vifungu vya pekee ila ni mfano tu wa vifungu ambavyo ni vingi na vinavyoweza kutolewa, kuonyesha bayana kuwa Mungu ni mmoja na sio watatu . Kifungu cha mwisho kwa hivi vilivyotajwa ni cha muhimu mno.Yesu alikuwa amefufuliwa , akafa, akawa amefufuliwa kutoka kwa wafu na akainuliwa kukaa mkono wa kuume wa Baba na Paulo anashikilia kuwa kuna MUNGU MMOJA TU. Na ni nani huyu? Mungu wa Utatu wa imani inayoshikiliwa na wengi-BAba,Mwana na Roho mtakatifu? La hasha! Ni BABA. Paulo alimwabudu Mungu huyu.

## JE, YESU ALIKUWA MUNGU MWANA?

Tutasemaje kumhusu Yesu Kristo? Kwani hakuwa 'Mungu Mwana'? Jinsi msemo huu unavyotumika aghalabu na wengi siku hizi, ni ajabu kuwa msemo huu haupatikani katika Biblia. Twasoma "mwana wa Mungu" na sio "Mungu Mwana". Jambo la kukubalika hatimaye ni kuwa funzo hili halipati ukubalifu wa maandiko.Imani ya Athanasia yaeleza kuwa Baba na Mwana ni wenye uwezo sawa na ni wa kudumu milele. Kuendeleza dhana hii ya Baba na Mwana kuwa ni wa kudumu milele, Biblia yasema nini kuhusu nguvu sawa? Yaeleza waziwazi juu ya jambo hili. Je, Kristo alikuwa na uwezo sawa na Baba alipokuwa hapa na miaka 1900 iliyopita? Wacha mwenyewe ajibu swali hili:-
"Mimi siwezi kufanya neno mwenyewe" (Yohana 5:30).
"Mafunzo yangu si yangu mimi, ila yake yeye aliyenipeleka" (Yohana 7:16).
"Kwa maana Baba ni mkuu kuliko mimi" (Yohana 14:28).

Ukweli kuwa alitumwa na baba (Yohana 5:24,37) inakanusha nadharia ya kuwa nguvu sawa, na upungufu wake wa kujua wakati wa kurejelea kwake mara ya pili ikiwa ni ushuhuda wa ziada kupinga imani pendwa, kwani ni vigumu kufikiria Mtu wa Pili wa Utatu kushindwa kujua chochote. Hapakuwepo uwezo sawa kati yao hapo awali, na hata sasa usawa huo haupo! Tafakari maneno ya Paulo anaposema ." Mungu na Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo " (2 Kor.11:31), kama Yesu mwenyewe , baada ya ufufuo wake , "alimlinganisha Baba kama , "Mungu wangu " (Yohana 20:17). Ukweli mwingine ni kuwa "kuna Mungu mmoja na mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu, mwanadamu Kristo Yesu" (1 Tim 2:5), ni thibitisho kutilia nguvu haya.

# NAFASI YA KRISTO SIKU ZA USONI

Ushahidi huu unaweza kuendelezwa zaidi. Twatazamia wakati wa mwisho wa kutawala Kristo duniani kwa miaka elfu moja .Twaona nini?

"Hapo ndipo mwisho, atakapompa Mungu Baba ufalme wake…Maana sharti amiliki yeye, hata awaweke maadui wake wote chini ya miguu yake….Basi vitu vyote vikiisha kutiishwa chini yake, ndipo Mwana mwenyewe naye atatiishwa chini yake yeye aliyevitiisha vitu vyote, ili kwamba Mungu awe yote katika wote" (1 Kor. 15:24-28)

Awali, sasa, na hata siku za usoni , hata kama Yesu Kristo ameteuliwa kupata nafasi ya juu, Baba anasalia kuwa na mamlaka /uwezo mkubwa, na kuwa sawa si jambo hata la kufikiria.

Kwa hivyo Yesu Kristo ni nani? Ni Mwana wa Mungu , aliyezaliwa na mama bikira kama ilivyorekodiwa katika Mathayo na Luka :

"Roho Takatifu atakujilia juu yako, na nguvu zake Aliye juu zitakufunika kama kivuli; kwa sababu hiyo hicho kitakachozaliwa kitaitwa kitakatifu, Mwana wa Mungu"(Luka 1:35).

Yesu aliishi kama Maandiko yanavyoeleza, alijaribiwa aliteswa na akafa lakini alifufuliwa na Baba kutoka kwa wafu na akainuliwa kukaa mkono wa kuume wa baba kama kuhani Mkuu na Mpatanishi. Atabakia hapo hadi atakaporudi kuimarisha Ufalme wa Mungu duniani.

# UPENDO WAKE MUNGU

Kama kuna sifa ya mwenyezi Mungu inayodhihirisha silika ya Mungu ni tofauti na miungu iliyoundwa na binadamu, ni upendo anaoonyesha.

Fikiria juu ya upendo anaoonyesha mzazi kwa watoto wake. Mungu anaonyesha upendo huo kwetu- na zaidi- kwetu sisi.

"**Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda Ulimwengu hata akamtoa Mwanawe pekee ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele**." (Yohana 3:16)

Kazi ya Bwana Yesu Kristo ni funzo lingine tofauti. Mwanadamu anavyohitaji wokovu itashughulikiwa vilivyo baadaye. Kusudi la Mungu kwa dunia na kwa wanadamu ni jambo ambalo halina budi kuelezwa hapa.

Ni funzo dhahiri la Biblia kuwa Mungu anakusudia kuubadilisha ulimwengu siku za usoni, kuondoa maovu ambayo yanaukabili ulimwengu huu.

# MPANGO WA MUNGU KWA NCHI

Historia asilia ya Waisraeli, yanaonyesha Mungu akitangaza, "Hakika yangu, kama niishivyo, tena kama dunia hii nzima itakavyojawa na utukufu wa BWANA"(Hesabu 14:21)

Kusema ukweli dunia haijajawa na utukufu wa Mungu kwa sasa. Lakini itajawa nao. Huu ndio mpango na nia ya Mungu.

Mtume Paulo aliwaambia watu wa Athenia kuwa siku moja ulimwengu utatawaliwa kwa haki na mfalme ambaye ameteuliwa na Mungu na kuwa ametoa thibitisho la jambo hili kwa kumfufua kutoka kwa wafu .

Ni hakika kuwa dunia haitawaliwi kwa haki sasa. Lakini itakuwa hivyo. Wakati huo ukiwadia utaitwa ufalme wa Mungu na Yesu atakuwa ndiye mfalme. Nia ya Mungu kuhusu dunia hii inashughulikiwa kwa ukamilifu katika funzo linalofuatia. Njia moja hakika inayoonyesha upendo

wake Mungu kwa mwanadamu ni kule kuonyesha mpango huu wake katika Biblia . Upendo wake pia umedhihirika pale ambapo amemtoa mwanawe ili awe kiini cha kusudi hili.

## ROHO

Funzo kumhusu Mungu haliwezi kukamilika pasi na kutaja maneno mawili yanayohusishwa na Mwenyezi Mungu na kazi yake. Neno 'roho' hutumika sana katika Biblia kumaanisha nguvu za Mungu, iliopo wakati wote, mahali pote. "Niende wapi nijiepushe na roho yako? (Zaburi 139:7) "Unirudishie furaha ya wokovu wako ; Unitegemeze Kwa roho ya wepesi" (Zaburi 51:12).

## ROHO TAKATIFU

Neno "takatifu" lina maana ya kitu kuwa maalum, kilichotengwa , tukufu,kilichowekwa wakfu. Tunaposoma kuhusu Roho Takatifu , Biblia yazungumzia juu ya nguvu za Mungu zinapotumika kwa shughuli maalum.

Wakati Mariamu, mamaye Yesu, alipoambiwa atachukua mimba na kumzaa mwana atakayeitwa Yesu, aliambiwa ya kuwa Roho Takatifu atamjilia juu yake na Luka anatilia mkazo maana ya msemo huu kwa kukariri "nguvu zake Aliye juu zitakufunika" (Luka 1:35). Angalia mstari huo. Malaika anaeleza kuwa kuzaliwa kwa Yesu kutakuwa ni kimuujiza kwa kupitia kwa nguvu maalum za Mungu kutendeka kwa Mariamu. Kwa sababu hii , Yesu angeitwa Mwana wa Mungu.

## UANDISHI WA BIBLIA

Tumeangalia tayari mstari katika waraka wa pili wa Petro unaosema "Unabii haukuletwa popote kwa mapenzi ya mwanadamu; bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu ,wakiongozwa na Roho Takatifu."   Hii ilikuwa ni nguvu maalum ya Mungu iliyowafanya manabii kunena na kuandika Maandiko na kupatikana kwa Neno la Mungu. Waliongozwa kwa Nguvu za Mungu.

Neno 'roho' huwa ni neno ambalo limetafsiriwa kwa Kiebrania (katika Agano la Kale) au ni neno katika Kiyunani (katika Agano Jipya) ambalo lina maana ya pumzi. Kwa hivyo Roho wa Mungu ilipomwongoza mtu, twaweza pia kusema , "Mungu alimpulizia pumzi yake". Maelezo haya juu ya neno hili yanaleta taswira maridadi tunapopitia vifungu vinavyotaja nguvu hizi za Mungu. Hii pia ndio sababu ,Paulo, anapomwandikia Timotheo, anasema , kila andiko limepuliziwa-"Kila andiko, lenye PUMZI ya Mungu" (2 Tim. 3:16).

Yesu alipokea nguvu za Roho Takatifu kama Agano Jipya inavyoeleza. Mitume pia walipokea nguvu hizi zilizowawezesha kufanyiza miujiza . Kifungu cha mwisho katika Marko 16:20 chatwambia kuwa sababu kuu ilikuwa ni kulithibitisha lile neno kwa ishara zilizofuatana na mitume .

Paulo anazungumzia jinsi vipawa vya Roho Takatifu vilivyotumika katika karne ya kwanza. Matokeo makubwa ya vipawa hivi vyote ni kupalilia sifa ya upendo. (Soma 1 Kor.12:28-31 halafu 1 Kor 13:1-13).

Mungu amedhihirisha upendo wake kwetu sisi kwa njia nyingi. Twaweza kuonyesha upendo

wetu kwake tukijitahidi kuishi maisha ambayo yatampendeza.

# MUHTASARI WA BAADHI YA HOJA MUHIMU

Kuna Mungu mmoja.
Yeye ni muumba.Hapatikani na mauti tangu mwanzo hadi mwisho.
Mungu anaona na kuyajua yote.
Mungu ni mwenye haki.Mungu ni pendo.
Mungu ametufunulia kusudi lake katika Biblia
Nguvu za Mungu zinaelezwa kama Roho Wake.
Maandiko yalisawiriwa kwa nguvu za Roho Takatifu.
Yesu alizaliwa kutokana na kitendo cha Roho Takatifu juu yake Mariamu.
Ni muhimu sana kufahamu hali ya Mungu ikiwa twataka kupata wokovu.

VIFUNGU VYA KUSOMA KATIKA BIBLIA

Mwanzo 1; Isaya 45 ; Matendo 17 (Weka maanani waliyotenda wale Waberoya); Zaburi 139 ; 1 Timotheo 6

KITIHANI CHA SOMO LA 2

Pigia mstari jibu lililo sahihi kwa kila swali lililoulizwa kisha uhamishe majibu hadi hati ya muhtasari ya majibu iliyo katikati ya kurasa za hizi.

1.Ulimwengu uliumbwa vipi?
(a) Kwa bahati tu (b) Kwa nguvu za Mungu
(c) Kwa mageuko sahihi hadi tata

2.Mungu wa kweli ni:
(a) Mungu wa Biblia (b) Mungu wa Kimisri
(c) Hatujui (d) Sanaam ya Baali

3.Ushahidi upi kati ya yafuatayo unaonyesha kuwepo kwa Mungu:
(a) Nyimbo za kitaifa (b) Unabii wa Biblia
(c) Ngano za kimapokeo

4.Katika Zaburi 139:6 mwandishi anasema:
(a) "Maarifa hayo ni ya ajabu yanishinda mimi."
(b) "Mungu anaona na kuyajua yote."
(c) "Mungu ni mweza yote."
(d)"Wewe wajua kukaa kwangu na kuinuka kwangu. "

5.Biblia yafunza kuwa:-
(a)Mungu ni Utatu (b)Mungu ni umoja
(c)Mungu ni miungu wengi katika mmoja

(d)Hakuna Mungu

6.Kwa kumtoa mwanawe (Yohana 3:16) Mungu alionyesha:-

6.(a)Matumaini yake (b) Mapenzi yake (c)Imani yake

(d)Haki Yake

7.Mungu ana kusudi lipi na dunia?

(a)Kuiangamiza (b)Kuiacha ilivyo

(c)Aijaze kwa utukufu wake

8.Roho wa Mungu ni nini?

(a)Nguvu za Mungu (b)Upendo wa Mungu

(c)Hiari ya Mungu (d)Kumtoa mwana wa Mungu

9.Mungu alitumia nini ili Biblia ipate kuandikwa?

(a)Utukufu wake (b)Roho Takatifu (c)Ukweli wake

(d)Rehema na Neema yake

10.Katika matendo 17:11 twasoma kuwa wale waliokuwa Beroya :-

(a)Walimwimbia Mungu nyimbo za sifa

(b)Waliyachunguza maandiko kila siku

(c)Waliwachochea watu

(d)Walifanya ghasia mjini

**SOMO LA TATU**

# MPANGO NA NIA YA MUNGU

Upendo wa Mungu umetiliwa mkazo katika funzo la awali-Upendo wake kwa ulimwengu kwa kumtoa mwanawe pekee. Mungu aliuonyesha upendo huu, ambao sisi pia twahitajika kuuonyesha usichukuliwe kama hisia tu za moyoni au ubozi/uzuzu.

Biblia yatilia mkazo haki ya Mungu na utenda haki wake. Yesu alifufuka kutoka kwa wafu ili Mungu aonyeshe haki yake na upendo wake kwa mwanadamu. Kwa kuwa Yesu hakutenda lolote baya, haikuwa sawa asalie mautini (Matendo2:24). Haingekuwa sawa Yesu kubakia kaburini. Mungu alimfufua kutoka kwa wafu.

Kwa hali hiyo si vema ulimwengu usalie katika hali ya maovu kushamiri na uwe mahali pa mabaya kutendekea. Kitabu cha Mithali chatwambia,"Mizani ya hadaa ni chukizo kwa Bwana"(Mithali 11:1).

**ANGALIA VIFUNGU HIVI:-**

"Mungu aghadhibikaye (waovu) kila siku" (Zaburi7:11).

"...wakati wa kufunuliwa kwake Bwana Yesu kutoka mbinguni pamoja na malaika na uweza wake katika mwali wa moto; Huku akiwalipiza kisasi wao wasiomjua Mungu, na wao wasiotii Injili ya Bwana wetu Yesu " (2 Thess. 1:7-8).

Hii ni sifa bainifu ya Mungu isiyotiliwa maanani. Haki yake Mwenyezi Mungu haitaruhusu uovu kushamiri. Mungu hataruhusu ulimwengu utawaliwe na watu ambao hawawezi kuweka sawa vipeo sanifu.

Ni nia yake Mwenyezi Mungu kuwa siku moja ulimwengu huu utatawaliwa kwa haki na Yesu Kristo (Matendo 17:31). Atakapokuwa Mfalme, matatizo mengi yanayowakumba

wanadamu yatatatuliwa. Wakati huu mzuri unaitwa Ufalme wa Mungu.

Yesu aliwafunza wanafunzi wake kuomba Ufalme uje ili mapenzi yake Mungu yatimizwe hapa duniani kama vile malaika wanavyomtii huko mbinguni(Mathayo 6:10).

# UNABII WA MAMBO YAJAYO

Twapata katika Biblia matumaini yenye hakika yanayoonesha mambo ya usoni; sio mara moja tu, ama kama sehemu chache, ila kwa mafungu mengi ya unabii. Twapata unabii kuwahusu watu binafsi, kuhusu mataifa yenye nguvu, na yale dhaifu, mengine yakiwa hata hayajapata kuwepo. Kuna unabii wa muda mrefu na ule wa muda mfupi, unabii wa mambo yajayo,ambayo yalikuwa hayajadhihirika, matukio ya ajabu ambayo yangefikia mataifa, matukio yasiyokuwa na kifani na yaliyo kinyume na matarajio ya kiasili. Twapata yote haya katika Biblia. Twatambua kuwa pasi na kukosea popote hapana unabii wa uongo.Tutachukuliaje haya? Watu wasiokuwa na msaada wowote wangeyatekeleza haya? Hawangeweza. Hatima ya mambo haya ni kukubali kuwa watu walioandika Biblia walipata mwongozo kutoka juu.

"Maana unabii haukuletwa popote kwa mapenzi ya mwanadamu;bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Takatifu" (2Petro1:21).

Usidharau nguvu za unabii wa Biblia. Petro, katika mlango uliotajwa, anasema ni "neno la unabii lililo imara zaidi " na analinganisha na taa ing'aayo mahali penye giza (k19). Huu ni ulinganifu wa kufaa. Tunapoangalia ulimwengu yaonekana kuwa hauna mwelekeo na hivyo basi kukosa maana au nia ya kufaa. Historia yatokea kuwa shaghalabaghala kwa matokeo yasiyoridhisha, pasipo na kusudu muhimu, isipokuwa labda tamaa ya makuu ya muda mfupi wa watu wanaopitia tu ulimwengu huu. Lakini usomaji mzuri wa Biblia wabadilisha msimamo huu kabisa na kuonyesha pasi na tashwishi yoyote ile kuwa mambo ya mwanadamu yako chini ya mwelekeo fulani na yanaelekezwa kufikia upeo usiotarajiwa-usiotarajiwa kweli, na wote isipokuwa wachache mno.

"Aliye juu ndiye anayemiliki katika ufalme wa wanadamu, naye humpa amtakaye, awaye yote "(Dan 14:32). Maneno haya yalilengwa Nebukadneza, Mfalme wa Babeli .Hakuwa mtu wa kusimuliwa hadithi tu bali alikuwa mtawala mkuu mwenye uwezo katika ulimwengu wa kale. Katika siku za hivi karibuni, mji wake, Babeli, umechimbuliwa na ukathibitishwa kuwa ulikuwa mji mkuu hasa ambao Biblia uliuzungumzia. Mamia ya maelfu ya matofali ambayo yamechimbuliwa ni dhihirisho bayana ya mfalme mkuu mwenye kiburi aliyetawala ulimwengu wakati ule. Nebukadneza anaweza kujidai kuwa mfalme wa kwanza wa ulimwengu. Ni yeye ambaye aliambiwa, "Aliye juu ndiye anayemiliki katika ufalme wa wanadamu ". Na aliambiwa zaidi ya haya tu.

MAONO YA IBRA

Usiku mmoja, Nebukadneza alipokuwa amelalia kochi lake , alitaka sana kujua mambo yatakayokuwa halafu baada ya yeye kufariki na kuacha falme kubwa kama hiyo. "Enzi yangu nitamwachia nani ? "Je, enzi yangu itararuliwa na viongozi wakinzani wenye husuda ?" Kusema kweli, maswali kama haya hupita tu pasi na kupata jibu, kwani hapana awezaye kujua hali ya mtu ya baadaye; lakini Nebukadneza alipewa jibu na Mungu.Twayapata haya katika mlango wa pili wa kitabu cha Danieli.Tafadhali soma mlango huo, ni mojawapo wa

vifungu vya maana sana katika Biblia nzima.

Twaeleza juu ya ndoto iliyomjia na ambayo jibu alilolitaka lilitolewa kwa mfano wa ishara mbalimbali.

Swali laweza kuzuka, kwa nini Mwenyezi Mungu alijitaabisha ili kumfurahisha Mfalme wa kipegani; kwa kuamua kutumia njia ya ndoto, na kwa nini ujumbe ukawa utokee katika ndoto iliyosheheni mifano ambayo mfalme hakuweza kuelewa na hata hakuweza kukumbuka alipoamka .

Uchunguzi ufuatao waweza kutolewa kama jibu na utakuwa kama kielelezo cha unabii kamili na kutimizwa kwake :-

I. Umuhimu wa Nebukadreza katika kusudi la Mungu halikuwa hasa katika kuangalia ukuu wa ufalme wake ila ni katika kuangalia eneo la utawala wake ambao ulishirikisha nchi ya Israel , na watu wa Israel ambao alikuwa amewateka nyara na kuwachukua hadi Babeli walikoishi kwa miaka 70. Nchi ya Mungu - Watu wa Mungu - walikuwa raia chini ya himaya ya Nebukadneza.

II. Njia iliyotumiwa ya kuutoa ujumbe huu ulimtambulisha mtu huyu Danieli, aliyekuwa Myahudi, mtu wa pekee aliyeweza kutoa maelezo ya ndoto hiyo. Hii inatilia mkazo ukweli kuwa "Mungu afunuanaye siri " ni Mungu hasa wa Israeli . Sehemu muhimu ya kusudi la Mungu lajitokeza wazi hapa.

III. Mtindo uliotumika wa mifano iliyotumiwa ni njia mwafaka wa kupitisha ujumbe kwa njia ya kuibana . Mfano mzuri ni katuni zinazoangazia masuala ya siasa katika maisha ya kisasa ni mfano mzuri. Lakini katuni huangazia yaliyopita na yaliyopo. Ndoto ya Nebukadneza iliangazia kwa mapana juu ya siku za usoni.

TAFSIRI YA NDOTO

Katika ndoto yake mfalme sanamu ambayo yeye mwenyewe angeichukulia kama "mungu". Ilikuwa ni sanamu ya mtu aliye na metali kadha. Mchoraji angeonyesha sehemu zifuatazo-kichwa cha dhahabu, kifua chake na mikono yake ni ya fedha, tumbo lake na viuno vyake ni vya shaba, miguu yake ni chuma, na nyayo za miguu yake nusu ya chuma na nusu ya udongo. Sanamu hii ya kimetali ikasimama imara -hadi nguvu isiyojulikana ilipoamuru jiwe kugonga penye nyayo. Sanamu hiyo ikavunjwa vipande vipande na makapi yale yakawa kama viwanda vya kupepetea wakati wa hari, upepo ukavipeperusha hata pasionekane mahali pake ;"na jiwe hilo lililoipiga hiyo sanamu likawa mlima mkubwa, likaijaza dunia yote." (Daniel 12:35).

Haya yote yalimaanisha nini? Maneno ya Danieli aliyoyatamka yanaondolea mbali shaka yoyote iliyopo. Sanamu hiyo ilisimamia falme za wanadamu ambazo zingetokezea katika vizazi ambavyo vingefuatia. Mataifa ya wakati huo yalikuwa chini ya himaya ya mfalme wa Babeli, ambaye aliwakilishwa na kichwa cha dhahabu. "Wewe u kichwa kile cha dhahabu (k 38). Kufuatia kungekuwepo na ufalme wa pili, wa "fedha ," kisha wa tatu na wa nne. Ufalme wa nne ungekuwa na "nguvu mfano wa chuma", na udhaifu ungefuatia hizi nguvu:-

"Na kama vile ulivyoziona hizo nyayo za miguu na vidole vyake, kuwa nusu udongo wa mfinyanzi, na nusu chuma, ufalme ule utakuwa ufalme uliochanganyika. Na kama vidole vya zile nyayo vilikuwa nusu chuma na nusu udongo, kadhalika ufalme ule utakuwa nusu una nguvu na nusu yake umevunjika...hawatashikamana, kama vile chuma kisivyoshikamana na

udongo" (Danieli 2:41-43).

Swali ambalo lazima lijibiwe sasa ni, ukweli wa historia unaambatana vipi na unabii huu?

Ulinganifu ni kamili pasi na kasoro kiasi kwamba watu wengine wanajaribu kusema kuwa mlango wa pili wa Danieli uliandikwa baada ya matukio hayo ambayo yanaelezwa . Hii ni thibitisho tosha la usahihi wa unabii, na ni wazi kuwa haiwezekani, kwani unabii huu unaendelea kutimizwa. Nakala za kitabu cha Danieli zimepatikana katika Hati za Bahari ya Chumvi za karne ya pili kabla ya Masihi.

# HISTORIA YA ULIMWENGU KWA MUHTASARI

Falme nne zilifuatana. Chukua kitabu chochote cha historia uangalie kipindi kinachohusika na utapata maelezo ya jinsi Babeli ilivyoangushwa na Wamedi na Waajemi, falme mbili shirika ambapo kwanza Wamedi kisha Waajemi wakapata umaarufu. Ukuu wao uliangamizwa na Iskaanderia Mkuu mwasisi wa Ufalme wa Wayunani. Nao wakawapisha waliokuwa na nguvu zaidi. Rumi kusema kweli, ukiwa ufalme wa nguvu zaidi na uliodumu muda mrefu kuliko falme hizo nne .

Kwa karne nyingi ufalme wa Rumi umeshamiri Ulimwengu haukuwahi kupata kitu cha kujilinganisha na ufalme wa Warumi uliokuwa na nguvu mfano wa chuma ."Ni taifa gani au watu gani wangeweza kuangamiza ufalme kama huu? Hapangetokea ufalme mwingine zaidi ya hizi nne - Babeli, Wamedi - Waajemi, Wayunani na Warumi.

Ufalme huu wa Warumi kwanza uligawanyika katika sehemu mbili: Rumi ya Mashariki, iliyotawaliwa kutoka Konistantinopo, na Rumi ya Magharibi, iliyotawaliwa kutoka mji wa Rumi wenyewe. (Ita.kumbukwa kuwa ile sanamu ya Nebukadneza iliikuwa na miguu miwili ya chuma)

Baadaye, nusu mbili hizi zilianza kidogo kidogo kuangamizwa na majeshi yenye uhasama kutoka nje na uozo wa ndani kwa ndani enzi, na enzi pana iliyokuwa ikitawaliwa na Rumi ikaanza kuwa na falme huru zilizochipuka, zingine zikiwa na nguvu na zingine zikiwa hafifu . Mambo yamechukua mkondo huu hadi wa leo. HAPANA UFALME MWINGINE WA TANO KUFUATIA MSURURU WA FALME NNE ZILIZOTAJWA AMBAZO ZILITAWALA NCHI YA ISRAELI PIA. Jitihada nyingi zimefanywa lakini zote zimeambulia patupu. Filipo wa II wa Uhuspania, Napolioni I, Kaisari Wilhelm II,Hitler... Leo hii, mataifa ya Uropa yanajaribu kuungana ili yawe taifa moja. Ni kibarua kigumu. (Na hata hivyo, Uropa yenyewe haishirikishi taifa la Israeli.) Maneno ya nabiii yalikuwa hakika: "Lakini hawatashikamana, kama vile chuma kisivyoshikamana na udongo."

Ni nani angeweza kutabiri haya miaka kama elfu mbili unusu iliyopita? Ni nani ambaye angeshikilia kuwepo na falme nne, na sio tatu, tano au sita ? Ni nani ambaye kwa ujasiri na mkupuo wa mara moja angeweza kueleza mambo makuu ya kihistoria kuhusu falme hizi, na mfuatano wa matokeo yake kwa wa ajabu namna hii? Je, kuna yeyote ? Kutokana na yale tunayojua kuhusiana na utabiri wa wanadamu, hatuna budi kujibu, La! Tumeona wazi kuwa Danieli hakujitia kuwa na uwezo huo.

"Mungu aliye mkuu amemjulisha mfalme mambo yatakayokuwa baadaye; na ndoto hii

ni ya hakika, na tafsiri yake ni thabiti" (Danieli 2:45).

Wanaume kwa wanawake ambao wamepitia unabii huu wamepata sababu nzuri ya kuwa na imani kuu kwa Mungu na neno lake. Ni imani ambayo wewe, unayeyasoma mambo haya, kwa hakika yafaa uyashiriki.

## SEHEMU YA UNABII NI YA SIKU ZA USONI

Aidha, utimilifu wa maneno ya Danieli, yanayoonyesha yasiyogeuka kwa uthabiti wake yanatufanya tuwe na mtazamo mpya wenye ari ya kutaka kujua hatima ya unabii huu.

Tutachukuliaje jiwe lile dogo lililoangukia sanamu kwa kishindo pale nyayoni na kuipepetea kama poda na hatimaye kuwa mlima mkubwa ulioujaza ulimwengu wote?

Ikiwa sanamu ile iliwakilisha falme za wanadamu, ni bayana kuwa jiwe nalo lawakilisha nguvu fulani isiyo ya kibinadamu ambayo itajiimarisha kama utawala wa ulimwengu wote baada ya kuondolea mbali tawala za wanadamu. "Utavunja falme hizi zote vipande vipande na kuziharibu." Haya ndiyo maelezo ya Danieli ;

"Na katika siku za Wafalme hao Mungu wa mbinguni atausimamamisha ufalme ambao hautaangamizwa milele, wala watu wengine hawataachiwa enzi yake ... Nao utasimama milele na milele.”

Hii ni mojawapo ya ahadi za Mungu kuwa hajaiacha dunia. Amesawiri mpango - Mpango Mkuu- wa wokovu kwa mwanadamu ; na mpango huo, kitovu chake ni Bwana Yesu Kristo. Wasomaji makini wataweza kutambua "jiwe lililochongwa mlimani bila kazi ya mikono " ni yule Mwokozi wa wanadamu aliyezaliwa, akachongwa tuseme, kutoka kwa mlima wa ubinadamu, pasi na msaada wa mkono wa binadamu, bali kwa nguvu zake Mwenyezi Mungu, katika ule muujiza wa kuzaliwa kwake. Yesu, kwa hakika , amezungumzia huduma yake kama jiwe - "jiwe walilolikataa waashi," na akaendelea kusema, " Naye aangukaye juu ya jiwe hilo atavunjika , naye yeyote ambaye litamwangukia litamsaga tikitiki" (Mathayo 21:42-44).

Ishara zote zaonyesha kuwa jiwe hili litaanguka kwa mshindo mkuu juu ya ulimwengu usiotarajia. Je, utaepuka maangamizi yajayo? Je, utashiriki uzuri wa ufalme wa Mungu, ambao Yesu yuaja kuleta hapa duniani?

Ni Yesu tu awezaye kuokoa. Lakini kabla ya kuachana na unabii wa Danieli, hebu tukumbuke mafunzo ya ndoto ya Nebukadreza yameelezwa zaidi katika maono aliyoyaona Danieli mwenyewe kama ilivyorekodiwa katika mlango wa 7 wa kitabu hicho chenye jina la Danieli. Badala ya metali, alama/ishara ni tofauti na inaendelezwa kwa upana kwa njia ya wanyama wanne wanaowakilisha falme nne kuu kama ilivyo katika ndoto ya Nebukadreza. Maneno malinganifu yanayopatikana katika Danieli 2:44 yanatolewa na maneno ya Danieli 7:27 kama ifuatavyo;

"Na ufalme na mamlaka , na ukuu wa ufalme, chini ya mbingu zote, watapewa watu wa watakatifu wake aliye juu; ufalme wake ni ufalme wa milele na wote wenye mamlaka watamtumikia na kumtii.”

### UFALME WA MUNGU

Lakini msomaji wetu asipotoshwe kwa kufikiria kuwa unabii wa pekee katika Agano la Kale juu ya ufalme wa Mungu unapatikana katika milango hiyo miwili ya kitabu cha Danieli

ambayo tumeipitia. Kutoa maelezo bayana kutilia mkazo dhana hii tutageukia kitabu cha nabii Isaya ambacho kinaeleza kwa lugha sahili, yaani lugha isiyo na mafumbo kwa sababu ya maelezo mengi anayoyatoa Nabii Isaya kuhusiana na Ufalme, ametajwa kama nabii wa Ufalme. Tunampa msomaji wetu kifungu hiki adurusu:

"Na itakuwa katika siku za mwisho, mlima wa nyumba ya Bwana utawekwa imara juu ya vilima; na mataifa yote watauendea makundi makundi. Na mataifa mengi watakwenda na kusema, Njoni twende juu mlimani kwa Bwana, nyumbani kwa Mungu wa Yakobo, naye atatufundisha njia zake, nasi tutakwenda katika mapito yake maana katika Sayuni itatoka sheria na neno la BWANA katika Yerusalemu . Naye atafanya hukumu katika mataifa mengi, atawakemea watu wa kabila nyingi, watatoa panga zao ziwe majembe, na mikuki yao iwe miundu; taifa halitainua upanga juu ya taifa lingine, wala hawatajifuza vita tena kamwe."(Isaya 2:2-4).

"Tazameni; Bwana Mungu atakuja kama shujaa, na mkono wake ndio utakaomtawalia.Tazameni, thawabu yake i pamoja naye, na ijara yake i mbele zake" (Isaya 66:2).

La muhimu pia ni kutaja masharti ya wokovu. Twateua kwa haya yote mojawapo kutoka katika Isaya 66:2 :-

"Mtu huyu ndiye nitakayemwangalia, mtu aliye mnyonge, mwenye roho iliyopendeka, atetemekaye asikiapo neno langu."

## MAELEZO YA DANIELI

Maelezo haya si ubunifu wa wachapishaji wa mfululizo wa mafunzo haya. SOMA Danieli 2. Danieli asema hivi:

"Na kama vile ulivyoona ya kuwa jiwe lilichongwa mlimani bila kazi ya mikono, na ya kuwa lilivunja -vunja kile chuma, na ile shaba na ule udongo, na ile fedha na ile dhahabu, basi Mungu aliye mkuu amemjulisha mfalme mambo yatakayokuwa baadaye; na ndoto hii ni ya hakika, na tafsiri yake ni thabiti"(Danieli2:45).

## UFALME WA MUNGU

Kama jinsi utawala wa Wamedi-Waajemi ulivyofuata wa Babeli; Warumi wakawafuata Wayunani na vile hatujawahi kuwa na ufalme wa ulimwengu wa tano, sehemu ya mwisho ya unabii huu utatimizwa.

"Na katika siku za wafalme hao Mungu wa mbinguni atausimamisha ufalme ambao hautaangamizwa milele...bali utavunja falme hizi zote vipande na kuziharibu, nao utasimama milele na milele."(Daniel 2:44).

Jiwe lile dogo liliangamiza sanamu inayowakilisha utawala wa wanadamu katika karne hizi zote na likawa mlima mkubwa ulioujaza ulimwengu wote. Jiwe ni kiwakilisha cha ufalme wa Mungu .

Daniel alihitimisha unabii wake kwa kusema," na ndoto hii ni ya hakika, na tafsiri yake ni thabiti."

Hii nii mojawapo tu ya unabii unaotuhakikishia kuwa kusudi la Mungu kwa dunia hii halina budi kutimizwa.

## MAFUNZO YA AGANO LA KALE NA AGANO JIPYA

Hebu angalia vifungu hivi vya Biblia ulivyovipitia katika funzo la awali

Hesabu 14:21 na Matendo 17:31.

Wakati Mungu atausimamisha ufalme wake, haki itatendeka katika ufalme huo. Hapatakuwepo na udhalimu wala mateso.

"Hatahukumu kwa kuyafuata ayaonayo kwa macho yake, wala hataonya kwa kuyafuata ayasikiayo kwa masikio yake, bali kwa haki atawahukumu maskini, naye atawaonya wanyenyekevu wa dunia kwa adili" (Isaya 11:3-5).

Hapo ndipo maneno ya Hesabu 14:21 yatakapotimizwa kama jinsi malaika walivyoimba alipozaliwa Yesu . Yesu akiwa mfalme juu ya nchi yote, ndipo ukweli huu utafunuliwa,"Atukuzwe Mungu juu mbinguni, na duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia"(Luke 2:14).

Kitabu cha mwisho cha Biblia kinaeleza hali ya mambo yatakavyokuwa kusudi ya Mungu litakapotimia:

"Nikasikia sauti kubwa katika kile kiti cha enzi ikisema, Tazama, maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu, naye atafanya maskani yake pamoja nao, nao watakuwa watu wake. Naye Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao.

"Naye atafuta kila chozi katika macho yao, wala mauti haitakuwepo tena; wala maombolezo,wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena; kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita" (Ufunuo 21:3-4).

UFALME HASA

Petro alikuwa mnenaji kwa wanafunzi wenziwe alipomwuliza Yesu swali,"Tazama, sisi tumewacha vyote tukakufuata, tutapata nini basi?" (Mathayo19:27).

Jibu la Yesu ni la muhimu . Alitilia mkazo kuwa ufalme aliotangaza ulikuwa ni ufalme hasa ambao hao wanafunzi wataushiriki:

"Amin, nawaambia ya kwamba ninyi mlionifuata mimi, katika ulimwengu mpya, atakapoketi mwana wa Adamu katika kiti cha utukufu wake, ninyi nanyi mtaketi katika viti kumi na viwili, mkiwahukumu kabila kumi na mbili za Israeli. Na kila mtu aliyeacha nyumba, au ndugu wa kiume au kike… na kuurithi ufalme wa milele" (Mathayo 19:28-29).

YESU ATARUDI TENA

Ili apate kuusimamisha ufalme hasa hapa duniani Yesu hana budi kurudi tena. Alipopaa kwenda mbinguni mwisho wa huduma yake, malaika waliwaambia wanafunzi:

"Huyu Yesu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja jinsi iyo hiyo mlivyomwona akienda zake mbinguni."(Matendo 1:11).

Maelezo zaidi kuhusu sehemu ya mwisho ya kutekelezwa kwa kusudi la Mungu na dunia hii wakati wa kurudi kwake Yesu yatatolewa katika mafunzo yanayofuatia. Mafunzo ya Yesu kupitia kwa mifano yake mingi yanaonyesha kuwa wenye haki watalipwa wakati wa kurudi kwake tena . NI muhimu sana kujitayarisha kwa kuja kwake.

MUHTASARI

Biblia inatilia mkazo uadilifu na haki yake Mungu na pia upendo wake.

Si nia yake Mungu kuachilia ulimwengu kuendelea kuwa katika hali iliyomo sasa

Mungu ataingilia kati mambo ya walimwengu na kusimamisha utawala wake kupitia kw a Yesu kama Mfalme .

Muhtasari wa matukio ya ulimwengu kama alivyoyatoa Daniel 2 yatupa thibitisho kuwa hatua ya mwisho ya mpango wa Mungu utatimizwa kwa hakika .

Yesu akirudi kuwa mfalme juu ya Ufalme wa Mungu wafuasi wake watazawadiwa kwa kupewa nafasi katika ufalme wake, lakini yafaa wawe tayari kwa kuja kwake.

| |
|---|
| VIFUNGU VYA KUSOMA BIBLIA<br>Isaya 11 ; Isaya 35 ; Mathayo 19 na 25 Danieli 2 |

KITIHANI CHA SOMO LA 3

Pigia mstari jibu lililo sahihi kwa kila swali lililoulizwa kisha uhamishe majibu hadi hati ya muhtasari ya majibu iliyo katikati ya kurasa za hizi.

1. Mungu aliupenda ulimwengu hata...(a)Akatuma majira (b)Akamtoa mwanawe pekee (c)Akawatoa malaika (d)Akatoa amri
2. Utawala wa pili kama unavyowakilishwa katika ndoto ya Nebukadneza ni (a)Babeli (b) Uyunani (c)Urumi (d)Umedi-Uajemi
3. Nebukadneza aliona nini kikipiga kwa nguvu sanamu katika ndoto yake? (a)Sanamu (b)Jiwe (c)mkono (d)upanga
4. Malaika waliimba nini kuhusu hali itakavyokuwa duniani Yesu akiwa mfalme? ( a)Kila mtu atatenda apendavyo (b)Kila mtu atakuwa mkarimu (c)Hapana atakayefanya kazi (d)Amani itakuwepo duniani
5. Ni nani atakayetawala ulimwengu kwa haki? (a)Mwana wa Mungu (b)Mtume Paulo c)Mtume Petro (d)Nabii Eliya
6. Katika mlango wa pili wa Danieli twasoma, "Na katika siku za wafalme hao Mungu wa mbinguni atausimamisha ufalme ambao ... utasimama (a)Kwa miaka 6,000 (b)Kwa maisha yote (c) milele na milele (d) Kwa miaka 100,000
7. Yesu aliwaahidi wanafunzi wake kuwa (a)na mali na ufanisi (b)watakaa kwenye viti vya enzi wakiwahukumu makabila ya Israeli (c)na mafanikio na furaha
8. Je, Biblia inatwambia kuwa ulimwengu utaendelea kuwa katka hali iliyomo sasa? (a) Ndio (b)La (c) Sijui (d)Biblia haisemi kitu
9. Yesu yuko wapi kwa sasa? (a)Duniani (b)Mbinguni (c)Kaburini (d)Katika nchi ya Israeli
10. Paulo aliwaambia watu wa Athene (Matendo 17) kuwa Mungu amewapa watu wote uthabiti wa mambo haya ya ulimwengu kuhukumiwa kwa haki na mtu yule ambaye Mungu amemchagua. Uthibitisho huo ni upi? (a)Kuzaliwa kwa Yesu (b)Kusulubiwa kwa Yesu (c)Ufufuo wa Yesu

FUNZO LA 4

MAUTI

Maafa bila shaka huwa ndio hugonga vichwa vya vyombo vya habari. Kifo cha ghafla na cha utumiaji wa nguvu huamsha udadisi; lakini mada kuhusu 'mauti' yenyewe si habari na ajabu zaidi ni kuwa hata haishughulikiwi. Hata hivyo, muda uliochukua kusoma sentensi hizo mbili za mwanzo, yakadiriwa kuwa kati ya watu 25-30 wamekufa (yaani, zaidiya watu 6, 250 kwa saa au 150,000 kwa siku). Siku moja utakuwa mmoja wao! Sio lazima upatikane wakati wa tukio la maafa, ambayo hutokea kwa nadra mno, na kusababisha vifo vichache, lakini siku mojawapo ya kawaida tu shughuli za maisha ya kila siku zitakoma na ulimwengu utaendelea mbele pasipo mchango wako. Hii ndio maana funzo juu ya mada ya mauti ni ya muhimu sana.

Wazo la mauti linazua swali, "Mimi ni nani?" Ni nini kinachotokea kwangu ninapokufa?" "Nina nafasi gani katika kusudi la Mungu la uumbaji?"

**Kimsingi, kuna mitazamo mitatu juu ya kifo:-**

1. Ipuuze.
2. Chukulia kuwa sivyo hasa inavyoonekana kuwa.
3. Kabiliana na ukweli unaohusu mauti na utafute njia ya kuhepea.

Hebu tuangalie kwa makini mitazamo hii:

## 1. PUUZA MAUTI

Mtizamo huu unashikiliwa na wengi wanouenzi utamaduni wa Uzunguni. Lengo ni tamaa ya mali na anasa, filosofia inayotawala maisha ya uzunguni ambayo kitovu chake ni elimu ya sayansi. Njia ya kisayansi ya kushughulikia matizo ya maisha ni kuyapima. Kukisia 'Nini hutokea baada ya mauti' si jambo la kupimika kisayansi kwa hivyo hupuuzwa.

Halaiki, wanaostaajabia uvumbuzi wa kisayansi hupuuzilia mbali wazo la kifo kutoka katika akili zao kwa kadri wawezavyo.

### 2. DHANA KUWA MAUTI SI VILE INAVYOCHUKULIWA HASA.

Mtazamo huu ndio unaochukuliwa na wengi wa wafuasi wa madhehebu ya ulimwengu. Mauti yasemekana sio mwisho wa uhai bali ni upenyo wa kuingia katika maisha ya milele. Kitovu cha dhana hii ambayo ina sura kadha ni wazo la mtu kuwa na 'roho isiyopatikana na mauti'; kuwa kuna kitu ndani ya mtu kisichoweza kufa. Kitu hiki humtoka mtu mwilini wakati wa mauti na kuelekea kuishi katika hali nyingine.

Lakini mawazo haya hayawezi kuthibitishwa kwa ujuzi wala kwa vitabu vya ulimwengu wa dini ambayo, mbali na Biblia (2 Timotheo 3:16), ni kukisia tu kwa akili na kupapasa gizani. Ujuzi wa telepathia (uwezo wa kupashana mawazo bila kutumia njia za hisia za kawaida) na hisia ya ziada kuonyesha kuwa kuna mengi ya kujua kumhusu mtu kuliko vile ambavyo sayansi imevumbua, lakini nyezo hizi haziwezi kuthibitisha kuwa kuna 'Kitu' kinachoendelea kuishi baada ya mwili kufa. Mwanadamu anahitaji kuelewa mada hii ya mauti.

Biblia ndicho kitabu cha pekee kinachoelezea hili vema. Inamulazimu kila mtu

3. KUKABILIANA NA UKWELI HALISI WA MAUTI NA KUTAFUTA NAMNA YA KUHEPUKA.

HAKUNA KOKOTE KATIKA BIBLIA DHANA YA KUWA MWANADAMU ANA ROHO ISIYOKUFA NA HUENDELEA KUISHI BAADA YA MAUTI.

Hili ni jambo linaloweza kuwashtua kabisa wale wanaoshikilia imani isiyobadilika ya Wakristo wengi.

> "Walio hai wanajua ya kwamba watakufa; lakini wafu hawajui neno lolote"
> "Hakuna kesi; wala shauri, wala maarifa, wala hekima huko kuzimu uendako wewe" (Mhubiri 9:5,10).

Ukweli huu hautoi starehe ya kutafakari, lakini yaweza kutufanya tunyenyekee na kuamusha hamu ya kutaka kupata namna ya kuhepukia kwa haraka.

## ASILI YA WOKOVU NI UPOLE.

Mungu ametangaza, "Mtu huyu ndiye nitakayemwangalia, mtu aliye mnyonge, mwenye roho iliyopondeka, atetemekaye asikiapo neno langu" (Isaya 66:2)

Maelezo ya 'mnyonge' yana maana ya mwanadamu anayetambua ya kuwa hana chochote cha kujivunia akiwa katika mwili huu wa kufa. Neno 'kupondeka' lina maana ya upole.

Mwanadamu ni kiumbe cha majivuno. Wazo la roho isiyokufa linavutia moyo wake wa kiburi cha asili. Lakini tukitaka ukweli wote, twafanya vema ikiwa tutayatupilia mbali mawazo yaliyomea mizizi, hata kama yana ushawishi kiasi gani ili tutafakari kwa makini yale ambayo Mungu amefunua kuhusu maumbile asili ya mwanadamu.

## MAUMBILE YA MWANADAMU

Biblia yachunguza na kufikia kiini cha suala hili la muhimu. Rekodi inayoelezea juu ya mwanadamu wa kwanza, Adamu na Hawa, si kisasili cha kubuniwa tu. Angalia kwa uketo ukweli unaoelezewa katika mlango wa kwanza wa Biblia.

"Bwana Mungu akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi, akampulizia puani pumzi ya uhai; mtu akawa nafsi hai" (Mwanzo 2:7).

Mwili wa Adamu ulitokana na elementi zote zinazohusisha mata. Elementi hizi zilipewa sura ya kuwa mwili wa ajabu wa mwanadamu kama alivyokusudia Muumba Vyote, vikiwepo vitu vyote vinavyohitaji uangalifu mwingi na ogani zote kama vile mapafu, moyo, na mzizi. Kanuni hii ndiyo inayofuatwa katika ibra ya watoto kukua katika tumbo siku zetu hizi.

Mwili wa mavumbi wa Adamu ulipata uhai kutoka kwa Mungu ambaye "alipulizia katika pua lake pumzi yenye uhai" na kile ambacho kingesalia kama mwili usio na uhai; ukawa "nafsi (mwili) hai".

## ROHO/NAFSI

Maisha ni siri isiyoelezeka lakini inatambulika na kuishia kuhesabika kwa vitu visivyo. Hapana ushahidi popote wa kuonyesha kuwa kuna uwezekano wa uhai kuwepo pasipo na mwili. Biblia yatufunulia haya na ujuzi waonyesha kuwa “mwili” na “uhai” vinategemeana na vikiwa pamoja twapata”nafsi hai” au “kiumbe”.

Neno “nafsi” inatumika sana katika Biblia ikiwa yamhusu mwanadamu au mnyama.Imetafsiriwa kama ‘wazo,’ ‘mnyama,’ ‘mwanadamu,’ ‘kiumbe’ na haina uhusiano wowote na dhana ya kutopatikana na mauti.

## NAFSI HAI

Maelezo yanayopatikana katika Mwanzo 2:7 “Mtu akawa nafsi hai” inamaanisha mtu akawa kiumbe hai kama viumbe vingine ambavyo Mungu alikuwa ameviumba.

Angalia Mhubiri 3:19-20: “Kwa maana linalowatukia wanadamu linawatukia wanyama, jambo moja lawatukia; anavyo kufa huyu ndivyo anavyokufa huyu; naam wote wanayo pumzi moja; wala mwanadamu hana kitu cha kumpita mnyama; kwa maana yote ni ubatili. Wote huendea mahali pamoja, wote hutoka katika mavumbi na hata mavumbini hurudi tena.”

Neno ‘nafsi’ linamaanisha ‘kiumbe’. Nafsi ni mtu. Nafsi haiwezi kuishi kando na mtu au mnyama. Mungu akiondoa pumzi au roho ya uhai kutoka kwa mtu anakuwa kiumbe maiti. Ni muhimu kuelewa hili kwani Wakristo wengi wanaamini visivyo - kuwa mtu ana nafsi/roho isiyoweza kupatikana na mauti na huendelea kuishi baada ya kufa. Hili halifunzwi katika Biblia. Kusema kweli hili ni funzo la yule nyoka mwongo katika Bustani ya Eden. Alimwambia Hawa, “Hakika hamtakufa”- kinyume kabisa na alivyosema Mungu kwa Adamu na Hawa. Mhubiri 12:7 inatuhimiza tumtegemee Mungu ili tuwe hai. “Nayo mavumbi kuyarudia nchi kama yalivyokuwa, Naye roho humrudia Mungu aliyeitoa.” Hiki kifungu hakithibitishi kuwa mtu huenda mbinguni anapokufa. Angalia Yohana 3:13 na uchunguze kwa makini maneno haya: “Wala hakuna mtu aliyepaa mbinguni.”Mtu hufa kwa sababu ya dhambi: “…roho ile itendayo dhambi itakufa.” Na katika Warumi 3:23 twasoma, “Kwa sababu wote wametenda dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu.” Kwa hivyo ni wazi kuwa wote hufa na hukosa fahamu hadi wakati wa ufufuo. 1 Wakorintho 15 inashughulikia matumaini ya ufufuo kwa urefu na mapana.

## MWANADAMU- KIUMBE CHA KUMPA MUNGU RAHA

Shabaha hasa ya kuumbwa mtu, kama ilivyo kwa viumbe wengine wote, ni KUMPA Mungu raha. “Wewe ndiye uliyeviumba vitu vyote, na kwa sababu ya mapenzi yako vilikuwako, navyo vikaumbwa.” (Ufunuo 4:11). Kinyume na wanyama, Mungu alimpa hiari ya moyo kujiamulia kama atatii au ataasi, kwa namna hii aweze kufanya uamuzi wa kibinafsi kuhusu tabia zake. Twaweza kuona jinsi mtu anavyoweza kupendeza Mungu hiari yake mwenyewe; mtu anavyoweza kumpa Mungu raha na sio kujipa raha hiyo yeye tu. Wazazi kwa kiwango cha chini, hupata raha kutoka kwa watoto ambao hujitolea kuwatii na kuwaheshimu.

## KUSHINDWA KWA MWANADAMU

Ili kupima au kutathmini matumizi yake ya uwezo wa hiari ya kujiamulia aliyo nayo mtu, Mungu aliwapa Adamu na Hawa kitihani rahisi. Waliambiwa: “Matunda ya kila mti wa bustani waweza kula, walakini matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile, kwa maana siku utakayokula matunda ya mti huo utakufa hakika” (Mwanzo 2:16-17).

Mtu alishindwa kitihani hiki kwa hivyo akahukumiwa kifo. Adamu na Hawa walishawishiwa na rai ya nyoka kuwa wangekuwa kama Mungu. Wakiyajua mema na maovu, na ule mti waliuona wafaa kwa chakula, wapendeza macho. Kwa njia hii kiburi na tamaa yao iliwalemea. Na hali hii ya mwanadamu imemvaa na kufanyiza sehemu ya hulka yake tangu wakati huo. Yaangalie kwa makini maneno ya nyoka ya kumshawishi Hawa: “Hakika hamtakufa” (Mwanzo 3:4).

Huu ulikuwa uwongo, kulikataa neno la Mungu, na uwongo huu umekuwa sehemu muhimu ya mafundisho ya dini zilizo na msingi wa kibinadamu tangu wakati huo.

## HUKUMU YA MWANADAMU

Adamu na Hawa walihukumiwa kwa haki na Mungu. Maneno yaliyotumiwa kutoa hukumu kwao ni ya muhimu sana kwani yanatupa msingi wa tafsili ya mauti.

“U mavumbi wewe, nawe mavumbini utarudi” (Mwanzo 3:19).

Yaonyesha kuwa mwanadamu anapokufa hukoma kuishi na huishia kuirudia hali ya kuumbwa kwake baada ya kuozeana. “Pumzi yake hutoka, huurudia udongo wake, siku hiyo mawazo yake yapotea” (Zaburi 146:4).

Kifo ni adhabu ya kutotii. Baada ya Mungu kutoa hukumu hii, Akaweka ulinzi kulinda njia ya mti wa uzima, “asije…akaishi milele” (Mwanzo 3:22)

## DHAMBI

Mauti ni adhabu kwa dhambi. “Roho ile itendayo dhambi itakufa” (Ezekiel 18:4).

Pana hoja yenye mantiki mepesi hapa. DHAMBI INASABABISHA KIFO. Kwa hivyo ni jambo la muhimu kufahamu ‘dhambi’ ni nini ikiwa twataka kuepukana na mauti ya milele.

Dhambi ni kutoamini Neno la Mungu na kutotii Mapenzi Yake. Matokeo yake yamewapata wote. “Wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu” (Warumi 3:23). Adamu na Hawa wamewarithisha wana wao hali hii ya kufisha. Udhaifu huu umekuwa sehemu ya maumbile ya binadamu, au kama Biblia inavyoita “Mwili” au ‘mawazo ya mwili’.

Yaweza kuwa katika hali mbalimbali, “Basi matendo ya mwili ni dhahiri, ndiyo haya: uasherati, uchafu, ufisadi, ibada ya sanamu, uchawi, uadui, ugomvi, wivu, hasira, fitina, na mambo yanayofanana na hayo” (Wagalatia 5:19-21).

Haya ndio matokeo ya kimaumbile ya maisha ya Adamu na Hawa kama walivyoanzisha miaka elfu sita iliyopita. Ulimwengu unajikuta katika hali hii ya shida nyingi kwa sababu mwanadamu amekaidi njia za Mungu.

## TUMAINI LA PEKEE

Katika somo la 2 baadhi ya tabia za Mungu zilipitiwa. Tabia ya binadamu imepitiwa sasa kwa sehemu hii. Tofauti ya wazi inayoonekana bayana yajitokeza katika maneno haya:

“Maana mawazo yangu si mawazo yenu, wala njia zenu si njia zangu; asema Bwana. Kwa maana kama vile mbingu zilivyo juu sana kuliko nchi, kadhalika njia zangu zi juu sana kuliko njia zenu, na mawazo yangu kuliko mawazo yenu.” (Isaya 55:8-9).

Ni bayana sasa kufahamu si kwa nini tu mtu hufa bali kwa nini mtu ni lazima afe. Mungu ni mwadilifu na Haki yake haimuruhusu mwenye dhambi kuishi milele. Lakini sifa mbili kati ya nyingi za Mungu ni huruma na msamaha. “Lakini kwako kuna msamaha ili Wewe uogopwe” (Zaburi 130:4).

Kuna sababu nzuri ya kuhitaji msamaha kwa sababu mtu hawezi kuwacha kufanya dhambi. “Tukisema kwamba hatuna dhambi twajidanganya wenyewe, wala kweli haimo mwetu” (1 Yohana 1:8).

Biblia yatoa maelezo kuhusu njia ya Mungu kwa mapana - njia ya pekee ya kumweka mtu huru kutokana na mshiko-sugu wa dhambi na mauti. Njia, msemo huu, ni kupitia kwa imani. Imani ambayo Mungu aitaka ni ustahilifu maalum. Yaelezwa kama; “hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana” (Waebrania 11:1).

Imani si kuamini chochote pasipo na ushuhuda kamili au kuamini upuuzi wowote. Ni kuwa na ithibati wote katika Mungu na imani isiyo na tashwishi kuwa Atatekeleza yale ambayo ameahidi hata kama yaonekana ni magumu na yasiyowezekana. Imani yetu kwa hivyo yafaa kudhihirika katika kutii amri za Mungu. Mlango wa kumi na moja wa kitabu cha Waebrania kimetoa mifano halisi ya imani. Imani muhimu ni ile aliyoonyesha Ibrahimu. “Akamwamini BWANA, naye akamhesabia jambo hili kuwa haki” (Mwanzo 15:16).

Imani yake ilionyeshwa kwa kumtii kwake Mungu. Soma Yakobo 2:17-26. Kwa hivyo imani na utiifu vinaweza, katika huruma yake Mungu, kumpa mtu msamaha wa dhambi na kama matokeo, kifo kitashindwa.

HII NDIYO NJIA YA PEKEE YA MWANADAMU KUFIKIA HALI YA KUISHI MILELE.

Uzima wa milele kusema kweli ni karama. “Karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu.” (Warumi 6:23).

Mambo haya yanawezekana kupitia kwa dhabihu aliyoitoa Yesu Kristo na jambo hili lazungumziwa katika makala yanayofuatia baadaye. Uzima wa milele utapatikana siku za usoni wakati ambapo ufufuo wa wafu utakuwepo. “Tena, wengi wa hao walalao (maana yake waliokufa) katika mavumbi ya nchi wataamka,wengine wapate uzima wa milele, wengine aibu na kudharauliwa milele” (Danieli 12:2).

Na wale wanaostahili karama hii maalum watabadilishwa wawe na miili ya kutokufa. Ufufuo wa wafu waonekana kama kitu kisichoaminika, kisichowezekana lakini ni baadhi ya vitu ambavyo Mungu ataka tuviamini. Twajua kuwa hakuna lisilowezekana kwa Mungu.

Ufufuo utatokea wakati ambapo Yesu Kristo atarejea: “Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni… nao waliokufa, katika Kristo watafufuliwa kwanza” (1Wathesalonika 4:16).

Baadhi ya ishara zinazoonyesha kuwa mambo haya ya muhimu yanakaribia kutokea yameelezwa katika somo la 9. Yafaa tujitayarishe kwa siku hiyo.

## MUHTASARI

1. Mauti ni hatima ya maisha, sio njia ya kuendea uzimani.
2. Wokovu huanza na upole.

3. Mauti husababishwa na dhambi.
4. Dhambi ni kutoamini Neno la Mungu na kutotii mapenzi yake.
5. Binadamu hawezi kuacha kuasi.
6. Mwanadamu aweza kupata msamaha kwa kuliamini Neno la Mungu na kutii mapenzi Yake.
7. Imani ni kuliamini neno la Mungu na inadhihirishwa kwa kutii.
8. Uzima wa milele ni karama ya Mungu, ambao wana wa Mungu walio waaminifu watapokea.
9. Uzima wa milele utapatikana wakati ambapo Yesu Kristo atarudi tena duniani kuwafufua wafu; tumaini la pekee la mwanadamu la kupata maisha ya milele ndilo hili.

**VIFUNGU VYA KUSOMA KATIKA BIBLIA:**

- Mwanzo 2 na 3
- Zaburi 49 na 146
- Mhubiri 9
- Warumi 5 na 6
- 1 Wakorintho 15.

**KITIHANI CHA SOMO LA 4.**

Pigia mstari jibu lililo sahihi kwa kila swali lililoulizwa kisha uhamishe majibu hadi hati ya muhtasari ya majibu iliyo katikati ya kurasa za hizi.

1. **Maelezo yapi ndiyo sahihi?**
   (a) Mauti yanasababishwa na dhambi.
   (b) Watu wote hufanya dhambi.
   (c) Uzima wa milele ni karama ya Mwenyezi Mungu.
   (d) Watu wema hawapatikani na mauti.
2. **Kifungu gani cha Biblia chaonyesha kuwa kifo ni kukosa ufahamu kabisa?**
   (a) Mithali 9:5
   (b) Ezakiel 9:5
   (c) Mhubiri 9:5
   (d) Esta 9:5
3. **Mungu anatafuta sifa zipi za mtu anayetaka wokovu?**
   (a) Kiburi
   (b) Utajiri
   (c) Upole

(d) Furaha

4. **Biblia yafunza kuwa mwanadamu aliumbwa kutokana na?**
   (a) Kiumbe mwingine tofauti.
   (b) Mavumbi ya ardhi
   (c) Maji
   (d) Hakumumba.
5. **Nini maana ya "nafsi hai"?**
   (a) Ni kiumbe mwenye uhai.
   (b) Jicho
   (c) Ni sehemu ya mwili inayoishi milele.
   (d) Kiumbe kisichoweza kupata mauti.
6. **Mwanadamu aliumbwa kwa sababu gani?**
   (a) Ili wachunge wanyama.
   (b) Ili ailime ardhi
   (c) Ampe Mungu raha.
   (d) Ajifurahishe mwenyewe.
7. **Adamu na Hawa walipokea adhabu gani kwa kutotii kwao?**
   (a) Walihukumiwa kifo.
   (b) Walipigwa
   (c) Mungu aliwakatalia mbali kabisa.
   (d) Walipigwa mawe.
8. **Dhambi ni nini?**
   (a) Matendo ya mwili.
   (b) Mauti.
   (c) Kuasi amri ya Mungu.
   (d) Maumbile ya mwanadamu.
9. **Imani ni…..?**
   (a) Kuamini yasiyowezekana.
   (b) Ufahamu wa mpango wa Mungu
   (c) Kuamini yasiyojulikana.
   (d) Kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana.
10. **Biblia hufunza:**
   (a) Hakuna matumaini.
   (b) Ufufuo wa wafu
   (c) Maisha mengine baada ya kufa
   (d) Kutopatikana na mauti mbinguni kwa wenye haki.

SOMO LA 5.

# AHADI ZA MUNGU.

Somo la 4 limeeleza kwa kutumia Biblia, sababu za mtu kufa, hali ya mauti na tumaini la pekee la kumwokoa mtu na adhabu ya milele ya kaburi. Katika somo la 5, tukiangalia baadhi ya ahadi za Mungu tunaweza kupata ufahamu zaidi kuhusu mpango wa Mungu wa wokovu kama unavyodhihirishwa kutoka katika maandiko.

## AHADI YA UKOMBOZI.

Hapo mwanzo, baada ya kutotii kwake Adamu na Hawa na laana kutangazwa kama matokeo ya dhambi ya mtu, kuna ahadi fupi lakini yenye kuleta matumaini iliyotolewa. Inapatikana

katika kifungu ambacho hakieleweki kwa wepesi.

"BWANA Mungu akamwambia nyoka…. Nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke, na kati ya uzao wako na uzao wake; huo utakuponda kichwa, nawe utamponda kisigino" (Mwanzo 3:14-15)

Maelezo kamili kuhusu ahadi hii hayashughulikiwi katika somo hili lakini yaweza kupatikana katika kitabu cha 'Misingi ya Biblia', lakini tunapozidi kupata ufahamu wa mpango wa Mungu wa wokovu, yaonekana bayana kuwa hapa pana ahadi ya mwanzo inayogusia kuwa hatimaye dhambi itashindwa na mmojawapo wa uzao wa Hawa. Dhambi itaangamizwa kabisa lakini uzao wake ambaye atatimiza hili ataumizwa kiasi na kwa kitambo tu (katika lugha ya mafumbo - jeraha kichwani na jeraha kwenye kisigino).

Ni ahadi ya kuja kwake Mwokozi; Biblia haitupi tashwishi kumtambua mwokozi huyu ambaye ni Yesu Kristo na anayeendeleza ahadi zote za Mungu.

## AHADI YA MUNGU KATIKA BUSTANI YA EDEN.

Nyoka amekuwa ndiye kitambulisho cha dhambi kwa kuhusika kwake katika sarakasi ya kumfanya Adamu na Hawa waasi amri ya Mungu. Yesu alitumia msemo huu alipowataja adui zake, Wafarisayo kwa maneno haya, "Enyi nyoka, uzao wa nyoka". Kule kuponda kichwa , pigo la kumfisha nyoka, ni ahadi ya kuangamiza dhambi na mauti kabisa. Yule anayeangamiza ni uzao wa mwanamke, na anapojaribu kutekeleza hili pambano yeye mwenyewe anapondwa kisigino; jeraha ambalo aweza kupona.

Ukisoma kwa makini huu uzao wa mwanamke utaona ya kuwa yazungumzia maisha, kifo na ufufuo wa Bwana Yesu Kristo. Katika pambano hili aliibuka mshindi dhidi ya dhambi na mauti na kuwapenyezea wote wanaomwamini njia ya kuupata uzima wa milele.

Ili kutegua kitendawili cha uzao wa mwanamke yaangalie maneno haya - "Tazama, bikira atachukua mimba, atazaa mtoto mwanamume, naye atamwita jina lake Imanueli"

Ujumbe huu ulinukuliwa wakati ambapo Yusufu aliambiwa na malaika juu ya mkewe aliyekuwa amemposa kuwa " atazaa mwana, nawe utamwita jina lake Yesu, maana yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao. Hayo yote yamekuwa ili litimie neno lililonenwa na Bwana kwa ujumbe wa nabii." Kisha nukuu ya maneno kutoka Isaya 7 yakafuatia, "Hata ulipowadia utimilifu wa wakati, Mungu alimtuma Mwanawe ambaye alizaliwa na mwanamke, amezaliwa chini ya sheria".

Ushindi wa Yesu dhidi ya dhambi na mauti, unaashiria kupondwa kwa nyoka (dhambi) kichwani, yaani kuangamizwa kabisa kwa upande wake Kristo; na kama alivyotabiri nabii Isaya, akawa amepokea mkwaruzo kwenye kisigino kwa kule kufa kwake kwenye mti na kukaa siku chache kaburini. Isaya alikuwa amesema, "Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu."

Hatua ya kwanza ya mpango wake Mungu wa ukombozi ukakamilika. Lakini Kristo ni limbuko tu. Mavuno yenyewe yaja katika awamu mbili na ndipo kuangamizwa kwa dhambi na mauti kutakamilika.

Hatua ya pili itakamilika pale ambapo Kristo atarudi tu kuwazawadi marafiki zake - wale ambao watakuwa wametenda sawasawa na alivyowaamuru. Hawa marafiki zake watafufuliwa kutoka kwa wafu, atawapa uzima wa milele ambao wataufurahia wakiwa papa

hapa duniani huku wakimsaidia yesu kutawala mataifa yote yatakayo nyenyekea na kumkubali atakaporudi tena. Hawamu hii itachukua muda wa miaka elfu moja.

Hatua ya mwisho itafanyika mwisho wa miaka elfu moja, wakati huo kutakuwepo hukumu ya mwisho na ndipo dhambi na mauti vitaangamizwa kabisa. “Maana sharti amiliki yeye (Kristo), hata awaweke maadui wote chini ya miguu yake. Adui wa mwisho atakayebatilishwa ni mauti.” Kama kutoamini kulileta kifo, nayo kuamini Injili na kutii kwa kubatizwa na kisha kuendelea katika kutenda mema kutaweza kuleta uzima wa milele.

## KUFUNULIWA KWA MPANGO WA MUNGU

Biblia inapotufunulia mpango wa Mungu; mada ya wokovu inaendelezwa katika njia nyingi. Jambo linalojitokeza kabisa ni somo tunalojifunza kuhusu tabia za maisha ya watu fulani zilizokuwa ni za mfano mzuri au mbaya wa imani (yaani wale ambao walimwamini na kumtii Mungu au wale ambao waliishi maisha yao kinyume). Kwa wengi waliokuwa waaminifu, Mungu alitoa ahadi za ajabu ambazo tunaziendelezea katika somo hili. Katika somo hili, tutaangalia tabia ya imani, maelezo ya maisha yao yanapatikana katika kitabu cha Mwanzo.

## NUHU

Uzao wa Adamu na Hawa ulipoongezeka, mvuto wa dhambi waliokuwa wamerithi kutoka kwa wazazi wao, ilianza kudhihirika. Katika kitabu cha Mwanzo mlango wa 6 unaeleza: “Bwana akaona ya kuwa maovu ya mwanadamu ni makubwa duniani na kwamba kila kusudi analowaza moyoni mwake ni baya tu siku zote” (Mwanzo 6:5).

Hii ndiyo iliyokuwa hali ya mwanadamu hata “Bwana akaghairi kwa kuwa amemfanya mwanadamu duniani, akahuzunika moyo” (Mwanzo 6:6).

Aliyepata neema mbele za bwana alikuwa Nuhu tu. Angalia Mwanzo 6:8-9). Mungu akaamua kuwa na mwanzo mpya na uumbaji wake na ikawa amemtumia Nuhu katika kutekeleza hili. “ Mungu akamwambia Nuhu, mwisho wa kila mwenye mwili umekuja mbele zangu; kwa sababu wameijaza dunia dhuluma, basi nitawaharibu pamoja na dunia”. (Mwanzo 6:13).

## GHARIKA

Mungu aliamua kugharikisha dunia ili kila kiumbe chenye pumzi ya uhai kiangamie akiwemo mwanadamu ambaye angezama maji. Kisa kilichomo katika kitabu cha Mwanzo kinachochukuliwa na wengi kama kisasili kilichobuniwa tu…Lakini tukikichunguza kisa hiki kwa makini tutapata ukweli wa kisayansi kutilia nguvu uthibiti wa rekodi ya Biblia. Maelezo yanayotolewa na Biblia kuhusu gharika yanasaidia kutoa mafunzo yenye nguvu juu uadilifu. Maisha ya Nuhu ni mfano mzuri sana wa imani kinyume na siku hizi za watu kuishi pasipo na imani.

## AHADI YA MUNGU

Mwenyezi Mungu alitangangaza kuwa hataiharibu nchi kwa gharika tena wakati huu. Mungu anakusudi na dunia na ametoa ahadi ya kuwa majira ya kupanda, na mavuno , wakati wa baridi na wakati wa hari, wakati wa kaskazi na wakati wa kusi mchana na usiku, havitakoma. Angalia Mwanzo 8:21-22.

## WANAOKOLEWA NI WACHACHE

Funzo lingine linalopatikana kutokana na haya ni kuwa Ukweli wa Biblia unayakariri haya, ni wachache ndio huwa tayari kumwamini Mungu na hatimaye ni wachache tu ndio watakaokolewa. Kanuni hii ambayo imejitokeza wazi katika hadithi hii ya Gharika (1 Petro 3:20), mkondo wa wokovu mkuu wa kuepuka kifo cha milele utafuata utaratibu huu.
Yesu Kristo alisema:

"Ingieni kwa kupitia mlango ulio mwembamba, maana mlango ni mpana na njia ni pana iendayo upotevuni, nao ni wengi waingiao kwa mlango huo.Bali mlango ni mwembamba, na njia imesonga iendayo uzimani, nao waionao ni wachache." (Matayo 7:13-14).

Hili na mifano mingine mingi kutoka katika Biblia inatilia shaka dini nyingi za ulimwengu zinatukeuza wingi wa 'waumini' wqao.

Biblia yafunza kuwa kuokolewa kutoka kwa kifo cha milele ni shughuli ya mtu binafsi na ni wachache ambao wamekuwa tayari ama wako tayari kukubali changamoto ya matakwa yake Mungu- kufuata njia iliyosonga na nyembamba ya imani.

## IBRAHIMU

Mfano mzuri wa watu waliokuwa tayari kukubali na kufaulu majaribio magumu ya imani ya neno la Mungu alikuwa Ibrahimu.

## AKIOLOJIA INASAIDIA KATIKA UCHUNGUZI WA BIBLIA.

Ibrahimu aliishi miaka 2,000 hivi kabla ya Masihi katika mji wa Uri uliopatikana kwenye ukingo wa Ghuba la Uajemi. Mahali hasa pa mji wa Uri pamefukuliwa na wanaakiolojia katika siku za karibuni. Ugunduzi wao umeonyesha kuwa mji huo ulikuwa na ustaarabu wa hali ya juu sana, wenye majumba makubwa, makasri na hekalu na huweza kufanyiza kazi bora zaidi za sanaa. Akiolojia inasaidia kazi ya kujifunza Biblia kwa kuchangia picha wazi ya siku za kale. Mambo haya yanachangia kudhamini ukuu wa imani ya Ibrahimu: "Toka wewe katika nchi yako, na jamaa zako, na nyumba ya baba yako uende mpaka nchi nitakayokuonyesha" (Mwanzo 12:1).

Kutokana na uthibitisho wa kiakiolojia, twajua kuwa Mungu alikuwa akimuuliza Ibrahimu aache maisha ya starehe ili ajitokeze katika uwanda mpana ulio na hatari sufufu zisizojulikana na abaki kumtegemea Mungu pekee kama kiongozi wake. Kinyume kabisa na Adamu na Hawa/Eva, Ibrahimu alimwamini na kumtii Mungu. "Kwa imani Ibrahimu alipoitwa aliitika(alitii); akatoka asijue aendako"(Waebrania 11:8).

# AHADI KWA IBRAHIMU

Imani ya Ibrahimu ilijengwa kwa msingi wa ahadi za baraka zilizoambatana na amri yake Mungu. Alitambua kuwa Mwenyezi Mungu, Muumbaji aliye na hekima yote, akitoa ahadi zozote zile, hana budi kuzitimiza. Mungu alimwambia: “Nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa na kukubariki na kulikuza jina lako; nawe uwe baraka, nami nitawabariki wakubarikio, naye akulaaniye nitamlaani; na katika wewe jamaa zote za dunia watabarikiwa” (Mwanzo 12:2-3).

Ahadi hizi zilikaririwa mara kadha wa kadha katika maisha marefu ya Ibrahimu huku kipengee kikiongezwa kwa ahadi asilia. Kwa minajili ya somo hili, tutaangalia vipengele muhimu za ahadi hizi kwa vichwa vifuatavyo:

- ✓ **Uzao wa Ibrahimu utarithi nchi.**
- ✓ **Uzao wake Ibrahimu ungekuwa taifa kuu.**
- ✓ **Kupitia kwa uzao wa Ibrahimu mataifa yote yangepata baraka.**

## 1. UZAO WA IBRAHIMU UTARITHI NCHI YA KANAANI.

Mungu hatimaye alimfikisha Ibrahimu katika nchi iliyojulikana hapo kale kama Kanaani. Ni sehemu ambayo katika nyakati hizi inashirikisha mataifa kama Lebanon, Israeli, Syria na Jordan upande wa mwisho wa Mashariki ya Bahari ya kati. (Angalia Mwanzo 15:18). Ibrahimu alipofika Kanaani, Mungu alimwambia, “Uzao wako nitawapa nchi hii” (Mwanzo 12:7).

Ahadi hii ilirudiwa baadaye,- “Nchi (Kanaan) hii yote uionayo, nitakupa wewe na uzao wako hata milele” (Mwanzo 13:15).

Angalia kwa makini nyongeza ya maneno ya ziada ‘wewe’ na ‘milele’. Kama si kwa maneno haya ya ziada, tungechukulia kwamba ahadi hii ililenga Waisraeli walioshuhudia vita na kumiliki nchi ya Kanaani hapo kale kama ilivyo rekodiwa katika kitabu cha Joshua. Haya yatimizwa kwa sehemu tu kwani ahadi ilikuwa kwanza, iwe ya Ibrahimu na uzao wake na pili, umiliki uwe ni wa kufurahiwa milele.

Hoja ya kwanza yaonyesha ya kuwa Ibrahimu alipokuwa angali Kanaani kama vile Wamaasai wetu na mkewe alipokufa alilazimika kununua kipande cha ardhi ili amzike. Hatimaye hata yeye akafa, pasi na kupokea urithi wa nchi hiyo aliyoahidiwa (Matendo 7:2-5).

Hoja ya pili, ni bayana kuwa si Ibrahimu wala uzao wake, yaani taifa la Israeli limepata kurithi nchi ya Kanaani milele kwani wamekuwa katika hali ya kutawanywa mbali na nchi ya Kanaani.

## UFUFUO NI LAZIMA NA NDIO JAWABU

Ni wazi kuwa ahadi hii itatimizwa siku za usoni. Itahitaji tukio kubwa-ufufuo wa Ibrahimu na uzao wake, wale ambao Biblia iliwataja kama watu walio na imani na utiifu kwa Mungu kama wa Ibrahimu. Ni baada ya ufufuo na baada ya kupokea miili isiyoweza kupatikana na mauti ambapo watairithi nchi ya Kanaani milele (Mathayo 8:11).

Ukweli huu utadhihirika zaidi pale ambapo tutaangalia ahadi zingine.

## 2. UZAO WAKE IBRAHIMU UNGEKUWA TAIFA KUU.

Ahadi hii inapatikana katika kuangalia mambo yanayohusiana na maisha ya Ibrahimu na kwa upande mwingine ni kama yametimizwa kama Biblia inavyoonyesha (Mwanzo 12:2; 22:7; 13:16; 15:5; 22:17).

Kitabu cha Mwanzo chaonyesha kuwa mwanawe Ibrahimu, Isaka na mjukuu wake, Yakobo (ambaye alibadilishwa jina akawa Israeli) ndio mababu wa asili wa taifa la Israeli. Walikuwa wakiishi nchi ya Kanaani hadi wakati ule ambapo palitokea njaa na Yakobo akawahamisha watu wake katika nchi ya Misri. Kitabu cha kutoka kinaeleza jinsi uzao huu wa Yakobo ulivyoongezeka hadi ukafikia idadi ya watu milioni mbili na wakafanywa watumwa wa Wamisri. Mwaka wa 1,500 kabla ya Masihi, Mungu alimtuma Musa awakomboe na kuwaongoza waende Kanaani. Kitabu cha Yoshua, aliyekuwa mrithi wa Musa, chaeleza jinsi makabila kumi na mbili ya Israeli yalivyotoka na kutwaa Kanaani. Vitabu vya baadaye vya Biblia vyaeleza vile Israeli ilivyoendelea hadi mwaka wa 1,000 kabla ya masihi na kuwa Ufalme mkuu na uliostawi wakati wa enzi za Daudi na Sulemani.

### AGANO JIPYA YATOA MAELEZO JUU YA AHADI

Biblia yaonyesha kuwa baada ya kufa kwake Sulemani, Israeli ilififia na hatimaye ikatawanywa kutoka Kanaani kwa sababu watu, kusema kweli, walikosa imani na waasi kwa Mungu (Kumbukumbu 28:15-68). Ni katika Agano Jipya ambapo twapata ufafanuzi wa ajabu kuhusu ahadi kwa Ibrahimu. Katika waraka wake kwa Warumi, Mtume Paulo anaonyesha bayana kuwa “ Hawawi wote Waisraeli walio wa uzao wa Israeli. Wala hawawi wote wana kwa kuwa wazao wa Ibrahimu” (Warumi 9:6-7).

Kuna dhana mpya inayojitokeza ambayo imetajwa kwa ufupi wakati wa kuangalia ahadi ya kwanza. Taifa kuu ambalo lingetokana na Ibrahimu halingetokana tu na taifa lisilo na imani linalotokana na uzao asili bali ni wale ambao wameonyesha imani iliyo ya Ibrahimu. Katika kila kizazi wamepatikana wachache lakini wakati watakapofufuliwa kutoka kwa wafu, Yesu atakaporudi duniani, watakusanywa pamoja kuwa taifa moja kuu.Wakati huo ndipo Ibrahimu atakapowaona wazao wake ambao wana miili isiyopatikana na mauti wakimsifu Mungu kwa kukombolewa kwao; watafanyiza mkutano mkubwa …wa watu wa kila taifa, na kabila, na jamaa na lugha” (Ufunuo 7:9). Kwa njia hii ahadi hii itatimizwa kwa njia mwafaka kuliko ilivyokuwa hapo awali.

## 3. KUPITIA KWA UZAO WAKE IBRAHIMU MATAIFA YOTE YANGEPATA BARAKA.

Hata hivyo, mwanadamu hajapokea baraka iliyo muhimu mno kulingana na ahadi hii-kukombolewa kutoka kwa laana ya dhambi na mauti. Biblia yadhihirisha kuwa wakati waja ambapo, “Dunia hii nzima itakavyojawa na utukufu wa BWANA” (Hesabu 14:21).

Utukufu wa Mungu kuijaza dunia ni ndoto wakati huu ambapo imejawa na vurugu na dhuluma na wakati ambao dhambi na mauti vingalipo. Mabadiliko makubwa yanahitajika ili wakati huo wa baraka ya ajabu upatikane kama tunavyosoma katika unabii wa Biblia (Zaburi 72; Isaya 32). Ingawa ni mabadiliko makubwa, hata hivyo, hayana budi kutokea! Huu ndio ujumbe wa injili (habari njema) ambayo inafunzwa katika Biblia. Ni wachache sana wanaotambua kuwa ahadi iliyotolewa kwa Ibrahimu miaka 2,000 kabla ya Kristo ni msingi wa injili.

"Na andiko, kwa vile lilivyoona tangu zamani kwamba Mungu atawahesabia haki mataifa kwa imani, lilimhubiri Ibrahimu habari njema zamani, kusema katika wewe Mataifa yote yatabarikiwa. (Wagalatia 3:8)

## YESU KRISTO- UZAO WA IBRAHIMU.

Yesu ndiye kiungo muhimu wa injili na kwa hivyo kwa ujumla ahadi zote kwa Ibrahimu. Yeye ndiye mzao mkuu wa Ibrahimu. Kitabu cha Agano jipya, chaanza kwa maneno haya, "Kitabu cha ukoo wa Yesu Kristo ... mwana wa Ibrahimu" (Mathayo 1:1).

Yaendelea kuonyesha vizazi vinavyofululiza uzao wa Yesu kutoka kwa Ibrahimu na wazo/dhana hii yapatikana kote katika Agano Jipya. Paulo anaonyesha katika waraka wake kwa Wagalatia kuwa kuna uzao maalum unaolengwa katika ahadi ile na mhusika ni Yesu: "Basi ahadi zilinenwa kwa Ibrahimu na kwa uzao wake. Hasemi, kwa wazao, kana kwamba ni wengi, bali kana kwamba ni mmoja, kwa mzao wako, yaani Kristo" (Wagalatia 3:16).

Yesu anadhihirishwa kama mwana wa kawaida wa Ibrahimu; katika waraka uo huo ianelezwa kuwa "walio wa imani, hao ndio wana wa Ibrahimu" (Wagalatia 3:7).

Tukikumbuka ya kuwa fasihi ya neno imani katika Biblia kama kumwamini na kumtii Mungu (kinyume kabisa cha dhambi), ni bayana kuwa Yesu alikuwa mwana mkuu kuliko wana wote wa Ibrahimu. Kati ya wote walio jamii ya wanadamu ni yeye tu angekabiliana na adui zake na kusema, "Ni nani miongoni mwenu anishuhudiaye ya kuwa nina dhambi?" (Yohana 8:46). Ujumbe mkuu wa Agano Jipya ni kuwa Yesu alishinda kifo kwa imani aliyokuwa nayo na ndiye "aliyebatili mauti, na kuufunua uzima na kutokuharibika kwa ile Injili." (2 Timotheo 1:10).

## INJILI YAHUBIRIWA KWA MATAIFA YOTE

Katika Agano La Kale ujumbe wa wokovu (Injili) uliwaendea wale wa taifa la Israeli tu lakini walishindwa kufuata matakwa ya kuwa waaminifu kwa utiifu kwa Mungu. Yesu akaja na kuwatuma mitume ili waihubiri injili ya wokovu kwa mataifa yote (Marko 16:15).

Wengi wanaona ya kuwa huu utimilifu wa Ahadi ya Mungu ya kuwabariki mataifa yote kupitia kwa Yesu Kristo ambaye ni uzao wa Ibrahimu. Ilikuwa ni hatua tu, ingawa ni hatua muhimu kwa Mungu kuujaza ulimwengu kwa utukufu wake. Yesu alifahamu kuwa ni wachache sana ndio watakaokubali ujumbe huu wa ajabu kwa sababu unahusisha kupitia mlango uliosonga na mwembamba wa imani; na kusema kweli ukiangalia sasa, miaka 2,000 baadaye, mahubiri ya injili hayajaleta baraka kwa mataifa yote.

## UFALME WA MUNGU DUNIANI

Hata hivyo wakati huu mzuri waja! Yesu Kristo atarudi tena duniani ili awafufue wote wanaowajibika na wale wote “waliomvaa Kristo” na kwa hivyo wamekuwa warithi sawasawa wa ahadi kwa Ibrahimu.(Wagalatia 3:27-29).

Wakati ule baraka ya Ibrahimu itawajia mataifa yote kupitia kwa uzao wake Yesu Kristo (Wagalatia 3:14). Yesu atakuwa mfalme juu ya nchi yote na Ufalme wa Mungu utaimarishwa na kuleta baraka ambayo ulimwengu huu haujawahi kushuhudia.

Wakristo wote wanafunzwa kumwomba Mungu: **“Ufalme wako uje, Mapenzi yako yatimizwe hapa duniani kama huko mbinguni”** (Mathayo 6:9-10).

## MUHTASARI

1. Ahadi ya ukombozi kutoka kwa dhambi na mauti ilitolewa mara Adamu na Hawa walipoanguka.
2. Mpango wa Mungu wa wokovu umedhihirishwa kupitia kwa ahadi zilizonenwa kwa waaminifu.
3. Maelezo yanayohusu Gharika yaonyesha kuwa watakaookolewa watakuwa wachache.
4. Ugunduzi wa Akiolojia unathibitisha usahihi au ukweli wa Biblia.
5. Mungu alitoa ahadi nyingi kwa Ibrahimu kwa sababu ya imani yake.
6. Hakuna ahadi ambayo imetimizwa kabisa.
7. Ahadi zote zamlenga Yesu Kristo ambaye alishinda dhambi na mauti.
8. Yesu Kristo anaweza kuwaokoa kutoka kwa kifo wale wote ambao wataamini na kutii kama alivyofanya Ibrahimu.
9. Ufalme wa Mungu ukija basi dunia itajawa na baraka na kujazwa na utukufu wa Mungu.
10. Ahadi hizi zote zitatimizwa wakati ambapo Yesu atarudi tena Duniani ili kuimarisha ufalme wa Mungu.

**VIFUNGU VYA KUSOMA KATIKA BIBLIA**

- Mwanzo 6,12,13,15,17,22
- Kumbukumbu 28
- Zaburi 72
- Isaya 32
- Yohana 8
- Matendo 7
- Warumi 4
- Wagalatia 3
- Waebrania 11.

## KITIHANI CHA SOMO LA 5

Pigia mstari jibu lililo sahihi kwa kila swali lililoulizwa kisha uhamishe majibu hadi hati ya muhtasari ya majibu iliyo katikati ya kurasa za hizi.

1. **Jina la mtu ambaye Mungu alipendezwa naye kulingana na Mwanzo 6:9?**

a) Adamu
b) Nuhu
c) Enoka

d) Habili

2. **Mungu aliangamiza vipi kizazi cha watu waovu kama ilivyo katika Mwanzo mlango wa 6 hadi 8?**

a) Tetemeko la ardhi
b) Njaa
c) Gharika
d) Magonjwa.

3. **Ni watu wangapi waliookolewa kutokana na mkasa wa Mwanzo 6 hadi 8?**

a) 8
b) 18
c) 88
d) 80

4. **Watu waaminifu walilindwa vipi kutokana na maafa yaliyotokea katika Mwanzo 6 hadi 8?**

a) Waliishi katika safina
b) Mungu aliwaficha
c) Waliishi kwenye mlima mrefu
d) Mungu aliwaondosha.

5. **Ibrahimu alikuwa akiishi wapi kabla ya Mungu kusema naye?**

a) Babeli
b) Betheli
c) Sodoma
d) Uri

6. **Mungu alimwelekeza Ibrahimu aiendee nchi gani?**

a) Misri
b) Kanaani
c) Edom
d) Hatujui.

7. **Je, ujumbe wa Injili ulihubiriwa Ibrahimu?**

a) Ndio
b) La
c) Labda
d) Hatujui

8. **Ibrahimu atapokeaje kutimizwa kwa ahadi ya Mungu**

**kwake?**

a) Amekwisha pokea
b) Hatujui
c) Yesu atakaporudi duniani ili aimarishe Ufalme wa Mungu.
d) Ibrahimu alikufa kwa hivyo hatapokea utimilifu wa ahadi.

**9. Ni nani alikuwa mzao mkuu wa Ibrahimu?**

**(a) Yuda**
**(b) Yakobo**
**(c) Yusufu**
**(d) Yesu**

**10. Ni ahadi zipi kati ya hizi alimwahidi Ibrahimu.**

a) Wazao wake wangemiliki nchi ya Kanaani.
b) Angeishi mbinguni milele
c) Wazao wake watakuwa taifa kubwa.
d) Angepata utajiri mkubwa mara moja
e) Kupitia mmoja wapo wa uzao wake mataifa yote yangebarikiwa
f) Wazo wake wote wangekuw waaminifu kwa Mungu.
g) Wazao wake wangekumbuka imani ya Ibrahimu kila mara.

Shiti ya Muhtasari wa Majibu

Ni muhimu kuandika JINA LAKO , ANWANI KAMILI NA NCHI vizuri Kwenye karatasi hii ya Muhtasari wa majibu.

Kila somo lina karatasi ya Kitihani na maswali 10 yakiwa na majibu kama 5 hivi – a,b,c,d,e; Mahali pengine utapata majibu zaidi yatahitajika. Chorea mstari herufi moja au zaidi kuonyesha jibu lako. KWA MFANO : Somo la kwanza swali la 7 ; ikiwa baada ya kusoma mambo yanayohusiana na Somo hili na ufikirie kuwa Biblia ina vitabu 23 tofautitofauti , utachorea mstari wako herufi d

Jibu maswali yote kwenye karatasi ya kitihani kwa kuwekea alama jibu sahihi – kisha utahamisha shiti hii ya muhtasari TU kwa anwani hii ; na hakuna anwani kwenye kisanduku basi huna budi kutumia anwani hii:

Christadelphian advancement Trust,
P.O. BOX 3034, South Croydon,
Surrey CR2 OZA
NDUGU WA KRISTO OR
P.O. BOX 552-50200 , BUNGOMA , KENYA ,E. AFRICA

SHITI YA MUHTASARI

WA MAJIBU

Jina…………………………………………

Anwani……………………………………..

……………………………………………..

**……………………………………………..**

……………………………………………..

…………………………………………….

SOMO LA KWANZA

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| a | a | a | a | a | a | a | a | a | a |
| b | b | b | b | b | b | b | b | b | b |
| c | c | c | c | c | c | c | c | c | c |
| d | d | d | d | d | d | d | d | d | d |
| e | e | e | e | e | e | e | e | e | e |

SOMO LA PILI

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| a | a | a | a | a | a | a | a | a | a |
| b | b | b | b | b | b | b | b | b | b |
| c | c | c | c | c | c | c | c | c | c |
| d | d | d | d | d | d | d | d | d | d |
| e | e | e | e | e | e | e | e | e | e |

SOMO LA TATU

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| a | a | a | a | a | a | a | a | a | a |
| b | b | b | b | b | b | b | b | b | b |
| c | c | c | c | c | c | c | c | c | c |
| d | d | d | d | d | d | d | d | d | d |
| e | e | e | e | e | e | e | e | e | e |

SOMO LA NNE

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| a | a | a | a | a | a | a | a | a | a |
| b | b | b | b | b | b | b | b | b | b |
| c | c | c | c | c | c | c | c | c | c |
| d | d | d | d | d | d | d | d | d | d |
| e | e | e | e | e | e | e | e | e | e |

SOMO LA TANO

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| a | a | a | a | a | a | a | a | a | a |
| b | b | b | b | b | b | b | b | b | b |
| c | c | c | c | c | c | c | c | c | c |
| d | d | d | d | d | d | d | d | d | d |
| e | e | e | e | e | e | e | e | e | e |

SOMO LA SITA

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| a | a | a | a | a | a | a | a | a | a |
| b | b | b | b | b | b | b | b | b | b |
| c | c | c | c | c | c | c | c | c | c |
| d | d | d | d | d | d | d | d | d | d |
| e | e | e | e | e | e | e | e | e | e |

SOMO LA SABA

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| a | a | a | a | a | a | a | a | a | a |
| b | b | b | b | b | b | b | b | b | b |
| c | c | c | c | c | c | c | c | c | c |
| d | d | d | d | d | d | d | d | d | d |
| e | e | e | e | e | e | e | e | e | e |

SOMO LA NANE

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| a | a | a | a | a | a | a | a | a | a |
| b | b | b | b | b | b | b | b | b | b |
| c | c | c | c | c | c | c | c | c | c |
| d | d | d | d | d | d | d | d | d | d |
| e | e | e | e | e | e | e | e | e | e |

SOMO LA TISA

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| a | a | a | a | a | a | a | a | a | a |
| b | b | b | b | b | b | b | b | b | b |
| c | c | c | c | c | c | c | c | c | c |
| d | d | d | d | d | d | d | d | d | d |
| e | e | e | e | e | e | e | e | e | e |

SOMO LAKUMI

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| a | a | a | a | a | a | a | a | a | a |
| b | b | b | b | b | b | b | b | b | b |
| c | c | c | c | c | c | c | c | c | c |
| d | d | d | d | d | d | d | d | d | d |
| e | e | e | e | e | e | e | e | e | e |

SOMO LA KUMI NA MOJA

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| a | a | a | a | a | a | a | a | a | a |
| b | b | b | b | b | b | b | b | b | b |
| c | c | c | c | c | c | c | c | c | c |
| d | d | d | d | d | d | d | d | d | d |
| e | e | e | e | e | e | e | e | e | e |

SOMO LA KUMI NA MBILI

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| a | a | a | a | a | a | a | a | a | a |
| b | b | b | b | b | b | b | b | b | b |
| c | c | c | c | c | c | c | c | c | c |
| d | d | d | d | d | d | d | d | d | d |
| e | e | e | e | e | e | e | e | e | e |

**SOMO LA 6**

# BWANA YESU KRISTO

Somo hili litaangalia Bwana Yesu Kristo aliye kiini cha kusudi la Mungu. Jina alilopewa yule mtoto aliyezaliwa Bethlehemu yapata miaka 2,000 iliyopita niYesu. Jina hili lamaanisha 'Mwokozi' na jina lenyewe lilitolewa kama alivyoagiza malaika.

"Nawe utamwita jina lake Yesu, maana yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao" (Mathayo 1:21). 'Kristo' ni kichwa hasa na kina maana ya 'Mpakwa mafuta', kwa hivyo ni mteule. Yesu alikuwa ndiye KRISTO kama Yohana alivyotajwa kama YOHANA MBATIZAJI.

# KUSUDI LA MUNGU TANGU MWANZO.

Katika somo lililotangulia imeonyeshwa kuwa Mungu alikuwa na mpango maalum tangu hapo, katika Bustani ya Edeni, ili amtoe Mwokozi- yule ambaye angeweza kushinda nguvu za dhambi. Somo letu lilionyesha kuwa yule ambaye angeleta baraka hizi ziwafikie wanadamu angetokea katika ukoo wa Ibrahimu. Mariamu alitambua kwamba mwanawe alikuwa ndiye aliyeahidiwa na katika wimbo wake wa furaha aliimba hivi:

"Moyo wangu wamwadhimisha
Bwana,
Na roho yangu imemfurahia
Mungu, Mwokozi wangu…
Amemsaidia Israeli, mtumishi
wake;
Ili kukumbuka rehema zake
Kama alivyowaambia baba zenu;
Ibrahimu na uzao wake hata
Milele"
(Luka 1:46-47,54-55).

# AHADI ZINGINE

Nabii Danieli alizungumzia wakati wa kufunuliwa Masiya. Nabii Mika naye aliandika juu ya mahali ambapo angezaliwa. Mathayo ameeleza juu ya ziara ya mamajuzi waliomtembelea Herode. Angalia jinsi Mathayo anavyoeleza kuwa matukio haya yalitokea sawasawa na maneno yaliyotabiriwa na manabii katika Agano la kale (Mathayo 1:22; 2:5&15).

Ilikuwa ni kusudi lake Mwenyezi Mungu kumtuma Yesu, na wakati mwafaka ulipowadia, kusudi lake Mungu likatimizwa. Yohana aliandika: "Naye neno alifanyika mwili, akakaa kwetu; (nasi tukaona utukufu wake, utukufu kama wa mwana wa pekee atokaye kwa Baba) amejaa neema na kweli". (Yohana 1:14).

## YESU ALIKUJA KWA NINI?

Kifungu kinachojulikana sana na kilichonukuliwa kabla ya somo hili, chasema, “Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda Ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe wa pekee ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele” (Yohana 3:16).

Mungu alimtoa Yesu na kumkabidhi ulimwengu kikweli. Malaika Gabrieli alimtokea Mariamu kumwambia atampata mototo. Mariamu alitaka kujua itawezekana vipi pasi na kumjua mume, Malaika akamjibu, “Akamwambia, Roho Takatifu atakukujia juu yako, na nguvu zake Aliye juu zitakufunika kama kivuli; kwa sababu hiyo hicho kitakachozaliwa kitaitwa kitakatifu, Mwana wa Mungu” (Luka 1:35). Hili pia lilikuwa limetabiriwa kama vile Mathayo anavyoeleza (Mathayo 1:22-23).

## DHABIHU

Wajua kuwa katika siku za Agano la Kale wanyama walitolewa kama dhabihu kila mara kuwakumbusha wahusika juu ya dhambi na kama njia ya kukombolewa. Aliyetoa kafara alikuwa anatambua kuwa kifo kilitokana na dhambi na wakati mwingine aliweza kujihusisha na kifo cha Yule mnyama kama ishara ya kutambua dhana hii. (Walawi 1:3-4). Paulo aliandika hivi: “Mshahara wa dhambi ni mauti” (Warumi 6:23).

Katika Waraka wa Waebrania, mambo matatu kuhusu dhabihu yanajitokeza vema:

- ❖ Katika nyakati za Agano la kale dhabihu ilikuwa na dhana ya kumbukumbu la dhambi iletayo mauti- dhana iliyoimarishwa hapo mwanzo (Waebrania 10:3).
- ❖ Kwa kuwa wanyama hawakuwa wametenda uovu wowote, walibaki kuwa kiwakilishi cha funzo hili: “Basi torati, kwa kuwa ni kivuli cha mema yatakayokuwa wala si sura yenyewe ya mambo hayo, kwa dhabihu zile zile wanazozitoa kila mwaka daima, haiwezi wakati wowote kuwakamilisha wakaribiao” (Waebrania 10:1).
- ❖ Dhabihu ya wanyama haingeweza kuondoa dhambi. “Maana haiwezekani damu ya mafahali na mbuzi kuondoa dhambi” (Waebrania 10:4).

Biblia yadhihirisha wazi kuwa kile ambacho dhabihu ya wanyama hakingefanya, Yesu kwa kujitoa kwake akawa sadaka kamilifu.

“Lakini huyu, alipokwisha kutoa kwa ajili ya dhambi dhabihu moja idumuyo hata milele, aliketi mkono wa kuume wa Mungu” (Waebrania 10:12).

## MWANZO MPYA

Biblia yaonyesha kuwa kama vile Adamu alivyoleta dhambi ulimwenguni na kwa dhambi hiyo mauti, Yesu naye kwa kuishi maisha ya uadilifu, “wateule…wapate wokovu ule ulio katika Kristo Yesu, pamoja na utukufu wa milele” (2 Timotheo 2:10).

Kwa kuwa Yesu aliishi maisha ya uadilifu, alipokufa, “Mungu alimfufua, akiufungua uchungu wa mauti, kwa sababu haikuwezekana ashikwe nao” (Matendo 2:24).

Mlinganisho unaotaja athari ya kutotii kwa Adamu na athari ya kutii kwake Yesu

unanukuliwa mara nyingi: “Kwa hiyo, kama kwa mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni, na kwa dhambi hiyo mauti, na hivyo mauti ikawafikia watu wote kwa sababu wote wamefanya dhambi.”
“Kwa sababu kama kwa kuasi kwake mtu mmoja, watu wengi waliingizwa katika hali ya wenye dhambi, kadhalika kwa kutii kwake mmoja watu wengi wameingizwa katika hali ya wenye haki”.
“Ili kwamba, kama vile dhambi ilivyotawala katika mauti, vivyo hivyo kwa njia ya haki neema itawale hata uzima wa milele kwa Yesu Kristo Bwana wetu”
(Warumi 5:12,19,21).

Tunavyofuata mkondo uliowekwa na Adamu, hivyo ndivyo twaweza kuenenda kwa mkondo uliowekwa na Yesu. Twaweza kuhusishwa na maisha aliyoyaleta: “Kawa kuwa kama katika Adamu wanakufa, kadhalika na katika Kristo wote watahuishwa” (1 Wakorintho 15:22).

## IMANI YAHITAJIKA

Somo la 4 lilionyesha kuwa kwa asili mtu ni wa kufa na kuwa anahitaji kuwa na imani ili ajihusishe na uzima ambao Mungu anautoa. Somo hilo lilionyesha kuwa hili limerahisishwa kwa kazi yake Yesu:

“Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti, bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu” (Warumi 6:23).

Kwa hivyo wokovu unaotolewa ni wa masharti, “Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe wa pekee ili kila mtu amwaminiye asipotee…” (Yohana 3:16). Hii ndio sababu Mwana wa Mungu aliitwa: “Yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao” (Mathayo 1:21).

## HUDUMA YA YESU SASA

Baada ya ufufuo wake Yesu alipaa kwenda mbinguni. Wakati wa kupaa kwake, malaika wawili walitangaza kurudi kwake mara ya pili:
“Huyu Yesu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja jinsi iyo hiyo mlivyomwona akienda zake mbinguni”(Matendo 1:11).

Naye Petro alisema kuwa Yesu angebaki mbinguni hadi wakati wa “kufanya upya vitu vyote”(Matendo 3:19-21).

Yesu yuarudi tena kutimiza kusudi la Mungu lililo ndani yake. Kwa sasa yeye ni mpatanishi aliye kati ya Mungu na mwanadamu. Anaelezwa kuwa ni Kuhani Mkuu anayetuombea mbele za Mwenyezi Mungu:

“Kwa sababu Mungu ni mmoja na mpatanishi kati ya Mungu na wanadamu ni mmoja, Mwanadamu Kristo Yesu” (1 Timotheo 2:5).

Waraka kwa Waebrania inaeleza kuwa kwa sababu Yesu aliishi duniani na atafananishwa katika kila njia na “ndugu zake” (Waebrania 2:17) anaweza kuchukuana na hali yetu ya udhaifu.

“Basi, iwapo tunaye kuhani mkuu aliyeingia katika mbingu, Yesu, Mwana wa Mungu, na

tuyashike sana maungano yetu. Kwa kuwa hamna kuhani mkuu asiyeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu; bali yeye alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote bila kufanya dhambi." (Waebrania 4:14-15).

## MUHTASARI

1. Yesu alizaliwa kama matokeo ya Roho Takatifu juu yake bikira Mariamu. Kwa hivyo ni Mwana wa Mungu.
2. Jina "Yesu" lamaanisha "Mwokozi" na ilikuwa kusudi lake Mungu kubuni mbinu ya kumwokoa mwanadamu kutokana na matokeo ya dhambi zake.
3. Mshahara wa dhambi ni mauti. Dhabihu ya wanyama ilitoa kumbukumbu ya dhana hii wala haingeondoa dhambi kamwe.
4. Yesu ndiye aliyetoa sadaka kamilifu.
5. Yesu yuko mbinguni ambapo anaweza kuwa kuhani mkuu mwenye rehema kwani anaelewa kutokana na ujuzi wa maisha ya mwanadamu.
6. Mungu ameahidi kumtuma Yesu Kristo mara nyingine hapa duniani ili akamilishe kusudi Lake ndani yake atakapokuja kuwa Mfalme.

**VIFUNGU VYA KUSOMA KATIKA BIBLIA**

- Mathayo 1:18-25
- Luka 1:26-38
- Luka 2
- Mathayo 2
- Yohana 1:1-14
- Warumi 5

## KITIHANI CHA SOMO LA SITA.

Pigia mstari jibu lililo sahihi kwa kila swali lililoulizwa kisha uhamishe majibu hadi hati ya muhtasari ya majibu iliyo katikati ya kurasa za hizi.

1. **Jina la 'Yesu Kristo' linamaanisha?**
   a) Mwokozi
   b) Mpakwa mafuta
   c) Mwokozi mpakwa mafuta
   d) Mpakwa mafuta mwokozi
2. **Mama wa Yesu aliitwa nani?**
   a) Elizabeth

b) Mariamu
c) Marita
d) Ruth

3. **Nani ndiye baba hasa wa Yesu?**
   a) Yusufu
   b) Daudi
   c) Ibrahimu
   d) Mungu
4. **Katika kitabu cha Mika 5:2 mahali pa kuzaliwa Yesu pametajwa kuwa?**
   a) Nazarethi
   b) Bethelehemu ya Efrata
   c) Bethelehemu ya Yuda
   d) Galilaya
5. **Dhabihu ya wanyama katika Agano la kale…**
   a) Ilikuwa kumbukumbu kuwa dhambi huleta mauti
   b) Kitulizo kwa Mungu mwenye ghadhabu.
   c) Ilikuwa kama matokeo ya ushirikina
   d) Ingeleta Wokovu.
6. **Y esu alitumwa miaka 2,000 iliyopita kwa nini?**
   a) Kuwaokoa Wayahudi
   b) Ili awe dhabihu kamilifu kwa ajili ya dhambi
   c) Kuwalisha maskini.
   d) Kuimarisha Ufalme
7. **Yesu yuko wapi hasa?**
   a) Kaburini
   b) Mbinguni
   c) Hapa duniani
   d) Hatujui
8. **Je, Yesu atarudi tena duniani?**
   a) Ndio
   b) La
   c) Hatujui
   d) Labda
9. **Yesu anafanya nini sasa?**
   a) Anatawala maisha yetu
   b) Ni kama kuhani mkuu mbele za Mungu
   c) Ana mamlaka juu ya serikali zote
   d) Hatujui.

10. **Karama/kipawa cha Mungu kupitia kwa Yesu Kristo ni nini?**
    a) Ufanisi
    b) Uzima wa milele siku za usoni
    c) Maisha ya milele sasa
    d) Amani na utulivu sasa

SOMO LA 7

# AHADI KWA DAUDI

Mungu alimwahidi Ibrahimu ya kuwa kupitia kwake yeye na uzao wake jamii zote ulimwenguni zitabarikiwa. Somo la 5 lilionyesha ya kuwa mmoja wapo wa uzao wake utaleta Baraka hizi duniani naye ni Yesu. Mada hii inafunzwa vilivyo katika Agano Jipya (Wagalatia 3:16).

Ibrahimu anatumiwa kama kielezo cha imani, na twaambiwa ya kuwa tukitaka kudhihirisha imani yetu hatuna budi kuishi alivyoishi Ibrahimu huku tukimwamini na kutii mapenzi yake Mungu.

Taifa la Israeli ambao ni ukoo uliotokana na Ibrahimu lilifanywa watumwa katika nchi ya Misri. Waisraeli Waliongozwa na Musa kutoka Misri baada ya mapigo kumi kufanyika Misri na kuwafanya wakubali kuwa kuna Mungu mbinguni anayethibiti ulimwengu na mambo yake. Kitabu cha Kutoka kinatueleza haya yote.

Hatimaye taifa la Israeli likakaa katika nchi ya Kanaani alipoishi Ibrahimu. Mfalme wao wa kwanza alikuwa Saulo, wa pili Daudi, aliyeandika Zaburi tele.

# AHADI KWA DAUDI

Katika kitabu cha Zaburi, Daudi anasema ya kuwa Mungu alimtolea ahadi maalum. “BWANA amemwapia Daudi neno la kweli, hatarudi nyuma akalihalifu. Baadhi ya wazao wa mwili wako nitawaweka katika kiti chako cha enzi”(Zaburi 132:11).

Wakati ambapo Ufalme wake Daudi ulikuwa umekamilika na amani kutanda, alitaka kumjengea Mungu hekalu au nyumba ya kufanyia ibada. Nabii Nathani alitumwa kwa Daudi kumweleza kwamba, ingawa Mungu hakumkubalia Daudi kumjengea nyumba lakini Mungu ataimarisha ufalme wake na mmmoja wa wazao wake atakaaa kwenye kiti chake cha enzi katika ufalme wake milele.

“Nawe siku zako zitakapotimia, ukalala na baba zako, nitainua mzao wako nyuma yako, atakayetoka viunoni mwako, nami nitaufanya imara ufalme wake.Yeye ndiye atakayejenga nyumba kwa jina langu, nacho kiti cha enzi cha ufalme wake nitakifanya imara milele. Na nyumba yako, na ufalme wako, vitathibitishwa milele mbele zako. Nacho kitafanywa imara milele”(2 Samuel 7:12-13,16)

Kuna hoja tatu muhimu katika vifungu hivi:-

❖ Ahadi haikumlenga Suleimani, mwana wa Daudi, kwa kuwa Mungu alisema “kiti cha enzi cha ufalme” kingefanywa imara daima. Ingawa

Suleimani anasifika kwa ukwasi na hekima yake, kusema kweli au ni dhahiri kuwa hakutawala milele. Katika kifungu cha 14, nabii Nathani anamwambia Daudi kuwa Mungu angekuwa baba wa mfalme huyo mkuu ambaye angetoka katika uzao wake. "Mimi nitakuwa babake, naye atakuwa mwanangu" (2 Samuel 7:14).

- Mfalme angekalia kiti cha enzi cha Daudi (2 Samuel 7:12).
- Mungu anatangaza kuwa atatimiza ahadi hiyo (2 Samuel 7:12).

## MAFUNZO YA MANABII

Hoja hizi zatiliwa nguvu katika maandishi ya Biblia nzima. Hebu soma vifungu vifuatavyo kutoka katika kitabu cha Isaya vinavyonukuliwa kila mwaka wakati wa sherehe za Krismas na uone hoja hizo tatu.

"Maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, tumepewa mtoto mwanamume; na uwezo wa kifalme utakuwa begani mwake; naye ataitwa jina lake Mshauri wa ajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, Mfalme wa amani. Maongeo ya enzi yake na amani hayatakuwa na mwisho kamwe. Katika kiti cha enzi cha Daudi na ufalme wake; kuuthibitisha na kuutegemeza kwa haki, tangu sasa na hata milele. Wivu wa BWANA wa majeshi ndio utakaotenda hayo" (Isaya 9:6-7).

Hoja zizo hizo zatiliwa mkazo:

- "Enzi yake…haitakuwa na mwisho kamwe"
- "Katika kiti cha ezi cha Daudi na ufalme wake"
- "Wivu wa Bwana wa majeshi ndio utaotenda hayo"

## ALIYEAHIDIWA NI YESU

Hapana shaka yoyote ni nani atakayekuwa mfalme mkuu katika ukoo wa Daudi. Malaika Gabrieli alimtokea Mariamu kabla ya kuzaliwaYesu na kumwambia, "Huyu atakuwa mkuu, ataitwa Mwana wa Aliye juu, na Bwana Mungu atampa kiti cha enzi cha Daudi baba yake. Ataimiliki nyumba ya Yakobo hata milele na ufalme wake utakuwa hauna mwisho" (Luka 1:32-33).

Angalia tena hoja hizo tatu:

- Ufalme ungefanywa imara daima
- Angetawala juu ya kiti cha enzi.
- Mungu angetimiza haya.

## WIMBO WA FURAHA WA MARIAMU

Katika mlango huu wa Luka, wimbo wa ajabu waimbwa na Mariamu kumsifu Mungu kwa sababu ya ahadi zake. Jambo la kuangalia kwa makini ni kuwa, ingawa malaika amwambia Mariamu kuwa ahadi hii ni kutimiza ahadi ya Mungu kwa Daudi, lakini Mariamu anatoa shukrani zake kwa Mungu kwa ajili ya mtoto atakayezaliwa ili kutimiza ahadi yake kwa Ibrahimu. Yaonyesha kuwa Mariamu alielewa kuwa ahadi kwa Daudi na kwa Ibrahimu

ilimhusu mtoto huyu.

"Amemsaidia Israeli, mtumishi wake… kama alivyowambia baba zetu, Ibrahimu na uzao wake hata milele" (Luka 1:54-55).

## UFALME

Hapana shaka kuwa ufalme alioutangaza Yesu ulikuwa ni ufalme hasa juu ya nchi. Yeye angekuwa mfalme na wafuasi wake wangekuwa na nafasi katika uongozi. Yesu aliwaambia wanafunzi wake "Ninyi mlionifuata mimi, katika ulimwengu mpya, atakapoketi mwana wa Adamu katika kiti cha utukufu wake, ninyi nanyi mtaketi katika viti kumi na viwili, mkiwahukumu kabila kumi na mbili za Israeli" (Luka 19:28).

Nia yake Mungu tangu hapo ni kuijaza nchi kwa utukufu wake na amani tele.

"Hakika yangu, kama niishivyo, tena kama dunia hii nzima itakavyojawa na utukufu wa BWANA" (Hesabu 14:21).

Hili litatimizwa wakati Yesu atarudi duniani kama Mfalme.

Hoja mojawapo maalum alyotaja Petro katika hotuba yake siku ya Pentekote ni kuwa Yesu ndiye mzao mkuu wa Daudi kama alivyoahidi Mungu. Petro alinukuu kitabu cha Zaburi ambacho tumekitaja ya kuwa Daudi alitazamia kuimarishwa kwa ufalme na Kristo awe mfalme:

"Waume, ndugu zangu, mniwie radhi niseme kwa ujasiri mbele yenu habari za baba yetu mkuu, Daudi, ya kuwa alifariki akazikwa na kaburi lake liko kwetu hata leo. Basi kwa kuwa ni nabii, alijua ya kuwa Mungu amemwambia kwa kiapo ya kwamba katika uzao wa viuno vyake atamketisha mmoja katika kiti chake cha enzi" (Matendo 2:29-30).

Mtume huyu akaeleza pia kuwa ishara kuu ya kutimizwa kwa ahadi hii ya Mungu kwa Daudi ni kule kufufuka kwake kutoka kwa wafu. "Yesu huyo Mungu alimfufua, na sisi sote tu mashahidi wake" (Matendo 2:32).

Petro alisema ya kuwa Daudi akielewa kuwa kutokea wakati ambapo Mwenyezi angemwambia Yesu Kristo, "Keti upande wa mkono wa kuume. Hata nitakapowaweka adui zako chini ya miguu yako". Mtume kisha akasema, "Basi nyumba yote ya Israeli na wajue yakini kwamba Mungu amemfanya Yesu huyo mliyemsulubisha kuwa Bwana na Kristo" (Matendo 2:34-36).

## UDHAMINI WA MUNGU

Paulo alitoa muhtasari wa matumaini makubwa yanayotolewa na Biblia alipowambia wasikilisaji wake wa Athene.

"Kwa maana ameweka siku atakayowahukumu walimwengu kwa haki, kwa mtu Yule aliyemchagua; naye amewapa watu wote uthabiti wa mambo haya kwa kumfufua katika wafu" (Matendo 17:31).

## MUHTASARI

1. Nia yake Mungu kwa nchi hii imedhihirishwa katika Biblia.
2. Ibrahamu na Daudi waliambiwa na Mungu ya kuwa nia yake itatimizwa kupitia yule ambaye angezaliwa katika msururu wa ukoo au uzao wao.
3. Yesu ndiye aliyeahidiwa.
4. Atatawala ulimwengu kwa haki wakati ambapo ufalme wa Mungu utaimarishwa.
5. Tumaini hili, msingi wake ukiwa katika mafunzo ya Agano la Kale, uliendelezwa bayana katika ujumbe ambao Yesu na wanafunzi wake waliueneza.

**VIFUNGU VYA KUSOMA KATIKA BIBLIA**

- Isaya 11, 35
- Matendo 2
- Zaburi 132
- Warumi 4
- Luka 19.

# KITIHANI CHA SOMO LA 7

***Pigia mstari jibu sahihi kwa kila swali lililoulizwa kisha uhamishiemajibu yako hadi Hati ya Muhtasari wa Majibu iliyo katikati ya kurasa hizi.***

**1. Ni mzao yupi wa Ibrahimu ataleta Baraka duniani?**

a) Isaac
b) Yusufu
c) Daudi
d) Yesu.

**2. Waisraeli walikuwa watumwa katika nchi gani?**

a) Afrika
b) Misri
c) Kanaan
d) Italia

**3. Ni kitabu kipi katika Biblia kinatueleza kuhusu kukombolewa kwa Waisraeli kutoka katika utumwa?**

a) Mwanzo
b) Kutoka
c) Mambo ya Walawi
d) Hesabu

**4. Ni nani aliyekuwa Mfalme wa kwanza wa Israeli?**

a) Sauli
b) Daudi

c) Suleimani
d) Samweli

5. **Daudi alitaka kumjengea Mungu nini?**
   a) Ikulu
   b) Hekalu
   c) Mji
   d) Madhabahu
6. **Mungu alimwahidi nini Daudi?**
   a) Mali nyingi
   b) Maisha marefu na afya nzuri
   c) Ya kuwa kiti cha enzi cha ufalme wake kingefanywa imara daima
   d) Furaha na mafanikio
7. **Ni nabii yupi wa Israeli aliyesema, "Basi litatoka chipukizi katika shina la Yese"?**
   a) Isaya
   b) Samwel
   c) Obadia
   d) Hosea
8. **Mzao wa Daudi aliyeahidiwa kukaa kwa kiti chake cha enzi ni nani?**
   a) Sulemani
   b) Yesu
   c) Hezekia
   d) Rehoboam
9. **Ufalme huo ulioahidiwa utaimariswa wapi?**
   a) Nchini
   b) Mbinguni
   c) Katika mioyo ya watu
   d) Hewani
10. **Twapata uthibitisho gani kuwa Mungu atatimiza ahadi hii kama Paulo alivyogusia akiwa Athene?**
    a) Majira
    b) Kuzaliwa kwa Yesu
    c) Usiku na mchana
    d) Kufufuka kwake Yesu.

SOMO LA 8

# UFUFUO WAKE YESU KRISTO

Neno 'UFUFUO' linamaanisha 'kuamka kutoka kwa wafu'. Linatokana na neno la Kiyunani 'anastasis' linalotumika katika Agano Jipya kumaanisha 'kuamka' au 'kusimama tena'.

Kufufuka kwake Yesu kutoka kaburini ni kitendo cha kweli cha kihistoria na kisichokanushwa. Kufa na kufufuka kwa Yesu Kristo ni hoja ya kuangazwa katika kuangalia nia ya Mungu na wanadamu. Imani ya Mkristo imejengwa juu ya jambo hili; Ukristo umejikita hasa katika kufufuliwa kwake Yesu kutoka kwa wafu.

# MADA KUU YA MAFUNZO YA MAFUNZO YA MITUME

Mitume walipoamua kumchagua mwingine kuchukua pahali pa Yuda, walimchagua Mathiya, ambaye walisema inampasa awe "shahidi wa kufufuka kwake (Kristo) pamoja nasi" (Matendo 1:22).

Mitume walitiwa gerezani kwa sababu "wanawafundisha watu na kuhubiri katika Yesu ufufuo wa wafu" (Matendo 4:2).

Paulo alihukumiwa "kwa ajili ya tumaini la ufufuo wa wafu" (Matendo 23:6, 24:21).

Nyaraka katika Agano jipya zimejaa mafundisho yanayohusu ufufuo wa Yesu na umuhimu wake kwetu sisi. Hili limetiliwa mkazo na mtume Paulo aliposema: "Tena kama Kristo hakufufuka, basi kuhubiri kwetu ni bure na imani yenu ni bure….mngalimo katika dhambi zenu" (Matendo15:14 na 17.).

# JE, KWA NINI MUNGU ALIMFUFUA YESU?

Mafunzo yaliyotangulia yameonyesha kazi ya Yesu kama dhabihu ya dhambi (Waebrania 9:26). Somo la 4 lilieleza jinsi Adamu alivyoleta dhambi na mauti kwa wanadamu wote kwa kutotii amri za Mungu. Kinyume na Yesu aliyetii amri za Mungu na kuishi maisha ya ukamilifu. Somo la 6 lilishughulikia mada hii.

Kifo cha Yesu, hata hivyo, hakingekuwa na mashiko yoyote kama dhabihu tosha, kama asingelifufuliwa kutoka kwa wafu. Yesu, aliyezaliwa "na mwanamke, amezaliwa chini ya sheria," (Wagalatia 4:4) alikuja katika hali hii iliyolaaniwa ya kufa kama vile sisi tumeirithi kutoka kwa Adamu. Yeye kibinafsi alikuwa huru na dhambi, kwa hivyo kifo

hakingemshikilia,“wala mauti haimtawali tena” (Warumi 6:9).

## UPENDO NA HAKI YAKE MUNGU

Kanuni na msimamo wake Mungu haungethubutu kumkubalia mtu kama huyu aliyeshikilia sheria Zake, kubaki katika hali ya kutawaliwa kwa sheria ya dhambi na mauti. Mtume Petro atwaambia: “Mungu alimfufua, aliufungua uchungu wa mauti, kwa sababu haikuwezekana ashikwe nao” (Matendo 2:24).

Somo la 3 lilionyesha ya kuwa ilikuwa ni kupitia kwa haki yake Mungu hasa na pia upendo wake kwa walimwengu huko kufufuka kwake Yesu kutoka kwa wafu.

“Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee bali awe na uzima wa milele” (Yohana 3:16).

## JE, UFUFUO NI IMANI MPYA YA KARNE YA KWANZA?

Twajifunza kutoka kwa Biblia ya kuwa kuamka kutoka kwa wafu lilikuwa ni tumaini la waumini zama zile kabla ya nyakati za Yesu. Ndio sababu Yesu akasema “Ibrahimu, baba yenu, alishangilia kwa vile atakavyoiona siku yangu; naye akaiona, akafurahi” (Yohana 8:56).

Petro alinukuu maneno ya Daudi, mfalme wa Israeli: “Nilimwona Bwana mbele yangu siku zote...kwa hiyo moyo wangu ukapendezwa, ulimi wangu ukafurahi; tena mwili wangu nao utakaa katika matumaini…yeye (Daudi) mwenyewe akitangulia kuyaona haya, alitaja habari za kufufuka kwake Kristo” (Matendo 2:25-26&31 linganisha na Zaburi 16:8-11).

Daudi pia alisema, “Bali mimi nikutazame uso wako katika haki, niamkapo nishibishwe kwa sura yako” (Zaburi 17:15).

## UFUFUO- AHADI ZA MUNGU ZATIMIZWA

Kama somo la 5 lilivyoonyesha, Ibrahimu na Daudi walitazamia kufufuliwa kutoka kwa wafu ili wafurahie ahadi za Mungu. Na sio wao tu waliokuwa na tumaini hili.

Ayubu alisema, “Lakini mimi najua kuwa Mteteaji wangu yu hai, na ya kuwa hatimaye atasimama juu ya nchi. Na baada ya ngozi yangu kuharibiwa hivi, lakini kwa mwili wangu nitamwona Mungu.” (Ayubu 19:25-26).

Isaya naye akasema,“Wafu wako wataishi, maiti zangu zitafufuka;amkeni, kaimbeni, ninyi mnaokaa mavumbini… nayo ardhi itawatoa waliokufa” (Isaya 26:19).

Danieli aliambiwa “Tena, wengi wa hao walalao katika mavumbi ya nchi wataamka” na kuwa yeye mwenyewe atastarehe katika usingizi wa mauti “na utasimama katika kura yako mwisho wa siku hizo”. (Danieli 12:2&13).

Mtume Paulo anathibitisha kuwa hili ndilo tumaini la wale waliomtangulia Yesu.

“Nimesimama hata leo hivi…wala sisemi neno ila yale ambayo manabii na Musa waliyasema, kwamba yatakuwa; ya kwamba Kristo hana budi kuteseka na ya kwamba yeye kwanza kwa kufufuliwa katika wafu atatangaza habari za nuru kwa watu” (Matendo 26:23).

## KRISTO NDIYE WA KWANZA KUFUFULIWA NA

# KUPATA UZIMA WA MILELE

Biblia yaonyesha wazi kuwa Yesu alikuwa wa kwanza kufufuka kutoka kwa wafu na kupokea uzima wa milele. Paulo aliandika ya kuwa: “Mwokozi wetu Kristo Yesu; aliyebatili mauti na kuufunua uzima na kutoharibika kwa ile injili” (2 Timotheo 1:10).

# JE,UFUFUO NDIO TUMAINI LA PEKEE LA KUPATA MWILI USIOHARIBIKA?

Uzima na kutoharibika ambako Yesu amefunua ni tumaini la kuamka kutoka kwa wafu, na kusimama juu ya ardhi.

Petro alitangaza bayana kuwa “Daudi hakupanda kwenda mbinguni” (Matendo 2:34). Tumeona kuwa halikuwa tumaini la Daudi. Mungu alikuwa amekwisha kumwahidi ya kuwa atamketisha Kristo kwenye kiti chake (Daudi) cha enzi katika mji wa Yerusalemu (Matendo 2:30).

Kama alivyoeleza Paulo katika hotuba yake akiwa Athene, angalia somo la 7, kufufuliwa kwake Yesu ilikuwa dhihirisho kutoka kwa Mungu kuwa, Kristo atatawala ulimwengu kwa haki, wakati na tarehe aliyoweka Mungu katika mamlaka yake siku za usoni (Matendo 17:31).

# UFUFUO- TUMAINI LA KWELI

Martha alikuwa mfuasi wa Yesu. Twaona waziwazi tumaini lake la maisha ya baadaye. Ndugu yake Lazaro alipokufa, Yesu alimwambia, “Ndugu yako atafufuka”. Martha akamwambia, “najua ya kuwa atafufuka katika ufufuo siku ya mwisho.” Yesu akamwambia, “Mimi ndimi huo ufufuo na uzima.Yeye aniaminiye mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi, naye kila aishiye na kuniamini hatakufa kabisa hata milele”(Yohana 11:23-25).

# JE, WOTE WATAFUFULIWA?

Maandiko yatwambia ya kuwa, “Mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Bwana wetu” (Warumi 6:23).

Wale wasiomtafuta Mungu au wale wasio na haja ya kumtumikia, ama wasiotaka kufahamu nia yake katika Yesu Kristo, hawatapokea karama ya Mungu. Biblia yafunza wazi kuwa: “Mtu aikosaye njia ya busara atakaa katika mkutano wao waliokufa” (Mithali 21:16).

“Mwanadamu mwenye heshima, iwapo hana akili, amefanana na wanyama wapoteao” (Zaburi 49:20).

“Wao wamekufa, hawataishi; wamekwisha kufariki na kuupoteza ukumbusho wao” (Isaya 26:14).

# UFAHAMU SAHIHI NI MUHIMU

Kinyume cha maelezo hayo, Yesu anatupa matumaini kwa kusema: “Na uzima wa milele ndio huu, Wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma” (Yohana 17:3).

Ikiwa tunahitaji kushirikishwa kwa nia na kusudi la Mungu, imetupasa kuwa na ufahamu wa mambo haya. Ni lazima tumjue Mungu wa ukweli na kuweza kulielewa Neno lake barabara. Tukiwa na ufahamu huu na imani ya ukweli wa mambo haya, twaweza kuchukua hatua nyingine ambayo ni UBATIZO katika Kristo ambayo itashughulikiwa vilivyo katika somo la 11. Paulo anaeleza vizuri sana umuhimu wa ubatizo kwa muumini wa kweli anayetaka kupokea ufufuo.

"Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake. Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlivyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaunganika kwa mfano wa kufufuka kwake" (Warumi 6:3-5).

# KRISTO KAFUFULIWA MWANZO - WENGINE BAADAYE

Yesu ndiye aliyekuwa limbuko la wale waliolala; alifufuka na kupata hali ya kutoharibika. Twasoma tena,"Lakini sasa Kristo amefufuka katika wafu, limbuko lao waliolala"(1 Wakorintho 15:20).

Limbuko ni mazao ya mwanzo baada ya mavuno, ishara ya mazuri mengi yajayo. Paulo anatumia mfano huu wa mavuno kuonyesha utaratibu wa ufufuo. "Lakini kila mmoja mahali pake; limbuko ni Kristo, baadaye walio wake Kristo, atakapokuja" (1 Wakorintho 15:23).

# KURUDI KWAKE KRISTO MARA YA PILI KUFUFUA WAFU

Kurudi kwake Kristo mara ya pili inashirikisha ufufuo siku za mwisho. Paulo aliandika juu ya "Kristo Yesu, atakayewahukumu walio hai na waliokufa, kwa kufufuliwa kwake na kwa ufalme wake"(2 Timotheo 4:1).

Paulo pia aliandika: "Lakini, ndugu, hatutaki msijue habari zao waliolala mauti, msije mkahuzunika kama na wengine wasio na matumaini. Maana, ikiwa twaamini ya kwamba Yesu alikufa akafufuka, vivyo hivyo na hao waliolala katika Yesu, Mungu atawaleta pamoja naye. Kwa kuwa twawaambieni kwa haya neno la Bwana, kwamba sisi tulio hai, tutakoosalia hata wakati wa kuja kwake Bwana, hakika hatutawatangulia wao waliokwisha kulala mauti. Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza" (1 Wathesalonike 4:13-16).

# UFUFUO NA HUKUMU

Danieli aliambiwa ya kuwa, "wengi wa hao walalao katika mavumbi ya nchi wataamka"; aliambiwa ya kuwa, "wengine" "wataamka" wapate "uzima wa milele, wengine aibu na kudharauliwa milele" (Danieli 12:2). Hili lazungumzia juu ya mkusanyiko wa wale waliofufuliwa na wale walio hai wakati wakurudi kwake Kristo ili afanye hukumu na uwezekano wa Yesu kuwaokoa wengine. Yesu aliyafundisha haya:

"Msistaajabie maneno hayo; kwa maana saa yaja, ambayo watu wote waliomo makaburini wataiskia sauti yake. Nao watatoka; wale waliofanya mema kwa ufufuo wa uzima na wale waliotenda mabaya kwa ufufuo wa hukumu" (Yohana 5:28-29).

Watu wote wanaoajibika ( walio na ufahamu) lazima wasimame mbele ya kiti cha hukumu cha Yesu Kristo. Wale wanaomwamini Mungu na wanaoufahamu upendo na rehema yake, wale ambao wamejaribu kupendeza na kufuata mfano wa Mwanawe mpendwa watapokea karama ya uzima wa milele siku hiyo kwa huruma yake Mwenyezi Mungu.

Yesu anatuzungumzia sisi sote anaposema, "Mimi ndimi huo ufufuo na uzima.Yeye aniaminiye mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi" (Yohana 11:25).

# MUHTASARI

1. Ufufuo wa Yesu Kristo ni jambo la hakika.
2. Ufufuo wa Yesu ndilo fundisho muhimu sana katika Agano Jipya.
3. Yesu alifufuliwa kwa sababu ya tabia yake kamilifu. Kwa hivyo haki na wema wa Mungu ukamtoa kaburini.
4. Tumaini la ufufuo ndilo tumaini la waumini wote kabla na baada ya kuja kwake Yesu.
5. Hatuna uzima wa milele kwa sasa, ama Mungu hangekuwa na haja ya kuahidi au kuwekewa matumaini.
6. Mwanadamu hana maumbile ya kutoharibika. Angekuwa nayo, Kristo asingejitoa ili kumletea mwanadamu wokovu.
7. Ufufuo baada ya kifo ndiyo tumaini la pekee la kupata hali hiyo ya kutoharibika.
8. Sio wote watakaofufuliwa; wale wasio na ufahamu watabaki katika makaburi.
9. Kufahamu, kuamini na kubatizwa ni muhimu sana kwa kujihusisha na Kristo na ufufuo.
10. Kristo alikuwa wa kwanza kufufuka na kupata hali ya kutoharibika; twaweza kuwa kama yeye tukifuata mfalme wake.
11. Ufufuo na hukumu itafanyika Yesu atakaporudi duniani tena.

**VIFUNGU VYA KUSOMA KATIKA BIBLIA**

- Zaburi 49
- Marko 16
- 1 Wakorintho 15
- Isaya 26
- Matendo 26
- Yohana 11

# KITIHANI CHA SOMO LA 8

Pigia mstari jibu lililo sahihi kwa kila swali lililoulizwa kisha uhamishe majibu hadi hati ya muhtasari ya majibu iliyo katikati ya kurasa za hizi.

**Neno 'Ufufuo' lina maana gani?**

(a) Kulala chini
(b) Kuinuka
(c) Kutoka kwa wafu
(d) Kuamka

1. **Ni mwanadamu gani aliyekuwa wa mwanzo kufufuka na kupata kuishi milele?**

(a) Lazaro
(b) Msichana wa Jairo
(c) Stefano
(d) Yesu

2. **Yesu alikufa kwa sababu gani?**

(a) Kwa kuwa alikuwa ni wa maumbile yetu
(b) Alikuwa mwenye dhambi
(c) Mungu alimlazimisha afe
(d) Wayahudi walitaka awaondokee

3. **Yesu aliishi tena kwa sababu gani?**

(a) Hakufa tena
(b) Ufahamu ulimrudia baada ya kusulubiwa
(c) Mungu alimfufua
(d) Alizimia tu alipokuwa kwenye mti.

4. **Ni watatu gani kati ya hawa wanaweza kutarajia ujira wa duniani siku za usoni? (1 Wafalme 14:16)**

(a) Ibrahimu
(b) Daudi
(c) Danieli
(d) Yeroboam

5. **Je, watu wote watafufuliwa kutoka kwa wafu?**

(a) La

(b) Ndio
(c) Labda
(d) Sijui

6. **Wafu watafufuliwa lini?**
   (a) Wanaendelea kuishi baada ya kufa
   (b) Yesu atakaporudi kusimamisha ufalme
   (c) Sijui
   (d) Biblia haitoi ahadi yoyote
7. **Nini litafuatia ufufuo?**
   (a) Ubatizo
   (b) Hukumu
   (c) Kujifunza Biblia
   (d) Kuimba nyimbo
8. **Ni nani atakubaliwa na Yesu siku ya mwisho?**
   (a) Wale wanaomfahamu, wanaomwamini, na kufuata mafundisho yake.
   (b) Wale wanaotenda mema na kuwasaidia wote
   (c) Wale waliohai
   (d) Wale wasioamini lakini kwa sasa wamo makaburini
9. **Je, ungependa kujifunza zaidi kumhusu Yesu na ushiriki ufalme wake unaokuja duniani?**
   (a) La
   (b) Sina hakika
   (c) Ni magumu haya
   (d) Ndio

Somo la 9

# KURUDI KWA YESU KRISTO

Ufufuo wake Yesu ni tukio la kihistoria ambalo matumaini ya wanadamu yanategemea. Kama lilivyotokea hili jambo la ufufuo, ndivyo lilivyo tukio la kweli kwa Mwanawe kama alivyoahidi Mungu. Alipokwisha kufufuka kutoka kwa wafu, Yesu alipaa kwenda mbinguni na malaika wakatoa hakikisho hili: “Huyu Yesu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja jinsi iyo hiyo mlivyomwona akienda zake mbinguni” (Matendo 1:11).

# SABABU YA KURUDI KWAKE KRISTO

Katika sala la Bwana, Yesu aliwafunza wafuasi wake kuomba ili ufalme wa Mungu upate kuimarishwa duniani. “Ufalme wako uje. Mapenzi yako yatimizwe hapa duniani kama huko mbinguni” (Mathayo 6:9-10).

Wakati huu ndipo maneno yake Daudi yatakapotimizwa: “Wenye haki watairithi nchi, nao watakaa humo milele” (Zaburi 37:29).

Kristo hana budi kurudi duniani ili aimarishe ufalme wa Mungu kwa kupindua tawala zote za wanadamu. Atafutilia mbali maovu ulimwemguni na kujaza dunia hii kwa wokovu wake Mungu kama suluhisho la kudumu kwa matatizo yanayoikumba.

Kwa sababu hii, mtume Paulo, katika karne ya kwanza, alimhimiza Tito kukataa ubaya na tamaa za kidunia. “Tupate kuishi kwa kuasi, na haki, na utauwa, katika ulimwengu huu wa sasa, tukilitazamia tumaini lenye baraka na mafunuo ya utukufu wa Kristo Yesu, Mungu mkuu na Mwokozi wetu” (Tito 2:12-13).

# KRISTO ATARUDI LINI?

Tangu hapo, Mungu ameweka siku ambayo Yesu atarudi duniani ili atoe hukumu. Paulo alisema hivi: “Kwa maana (Mungu) ameweka siku atakayowahukumu walimwengu kwa haki, kwa mtu yule aliyemchagua; naye amewapa watu wote uthabiti wa mambo haya kwa kumfufua katika wafu” (Matendo 17:31).

Katika mahubiri yake, Yesu alisema wazi kuwa, ingawa Mungu ana mpango wake na mambo ya kutenda kwa utaratibu au mwelekeo wake wa matukio, siku hasa ya kurudi kwake hakuwa na habari nayo. Katika kitabu cha Marko mlango wa 13, Kristo aliwaambia wasikilizaji wake juu ya kurudi kwake na akawapa ishara mbalimbali ambazo hazina budi kutokea kabla, na hatimaye akasema: “Hapo ndipo watakapomwona Mwana wa Adamu akija mawinguni kwa nguvu nyingi na utukufu” (Marko 13:26). “Walakini habari ya siku ile na saa ile hakuna aijuaye, hata malaika walio mbinguni, wala Mwana, ila Baba” (Marko 13:32).

# KRISTO ATARUDI PASI NA MATARAJIO KAMA MWIZI

Watu wengi wanachukulia kurudi kwa Kristo duniani kama jambo la kimzaha tu, ukiangalia kuwa mwanadamu amekuwepo na ni wa kudumu. Mtume Petro alionya kuwa watu watafikiria hivyo: “Watakuja na dhihaka zao watu wenye kuthihaki, wafuatao tamaa zao wenyewe na kusema iko wapi ahadi ile ya kuja kwake? Kwa maana,tangu hapo baba zetu walipolala, vitu vitu vyote vinakaa hali iyo hiyo, tangu mwanzo wa kuumbwa” (2 Petro 3:3-4).

Tumepewa uthabiti hapa kuwa Mungu hakawii kutimiza ahadi yake, bali jambo hili kuu litatokea wakati ambapo Mungu mwenyewe ameweka: “Lakini siku ya Bwana itakuja kama

mwizi" (2 Petro 3:10).

Hebu tusome mistari ya mwanzo kumi ya Petro mlango wa 3 ili tuyapate maelezo yake vema.

Kama alivyoeleza Kristo, saa hasa ya kurejea kwake haijulikani na yeyote isipokuwa Mungu, na haiwezi kufanyiwa hisibati kutoka kwa maandiko. "Katika saa msiyodhani Mwana wa Adamu yuaja." (Mathayo 24:44).

Hili latufunza ya kuwa imani yahitajika na waumini kuhusu kurudi kwake Kristo, kwani anayejua ni siku ipi hasa ni Mungu tu! Kwa wale wasiotazamia tukio hili kufunuliwa kwake kutakuwa kama vile mwizi atokeavyo usiku.

# JE, HAKUNA ISHARA YA KUONYESHA KRISTO ATARUDI JINI?

Wanafunzi wa Yesu walikuwa na haja sana na swali hili na hata wakamwuliza kwa faragha walipokuwa kwenye Mlima wa Mizeituni. "Tuambie, mambo hayo yatakuwa lini? Nayo ni nini dalili ya kuja kwako, na ya mwisho wa dunia?" (Mathayo 24:3).

Jawabu alilotoa Kristo kwa swali hili na mengine mfanowe katika unabii wa Biblia, waonyesha wazi kabisa kipindi cha wakati unaotarajiwa kutimizwa. Ishara za wakati wa mwisho zinawapata wafuasi wa Kristo moyo wa kujitayarisha kwa kurudi kwake.

# ISHARA YA KURUDI KWAKE KRISTO

### 1. ISHARA YA NUHU.

Katika jibu lake, Yesu aliwakumbusha wanafunzi wake maelezo na matukio siku zilizotangulia kutokea kwa gharika, mambo kama hayo hayana budi kutokea kabla ya kurudi kwake.

"Kwa maana kama vile ilivyokuwa siku za Nuhu, ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake Mwana wa Adamu. Kwa kuwa kama vile siku zile zilizokuwa kabla ya Gharika watu walivyokuwa wakila na kunywa, wakioa na kuolewa, hata siku ile alioingia Nuhu katika safina wasitambue, hata Gharika ikija ikawachukua wote, ndivyo kutakavyo kuwa kuja kwake Mwana wa Adamu." (Mathayo 24:37-39).

Ili upate maelezo sawasawa juu ya kipindi kilicho tangulia hizi Nuhu, soma kitabu cha Mwanzo 6 ambapo inaonyeshwa dhahiri kwa nini Mungu aliamua kuwaangamiza wanadamu na kusaza au kuokoa watu nane tu. Uovu ulikuwa umesheheni mawazo na vitendo vya wanadamu na Mungu akaona "Dunia itaharibika mbele za Mungu, dunia ikajaa dhuluma." (Mwanzo 6:11).

Vyombo vya habari, magazeti, mtandao, redio na runinga vinaonyesha ulinganifu wa

udhalimu; Mabaya yaliyokuwepo siku za Nuhu na udhalimu uliopo nyakati zetu hizi. Mambo haya ni sawa na yale aliyoyamlika mtume Paulo katika kumchora mwanadamu wa siku za mwisho kabla ya kurudi kwake Kristo:

“Lakini ufahamu neno hili, ya kuwa siku za mwisho kutakuwa nyakati za hatari. Maana watu watakuwa wenye kujipenda wenyewe, wenye kupenda fedha, wenye kujisifu, wenye kiburi, wenye kutukana, wasiotii wazazi wao, wasio na shukrani, wasio safi, wasingiziaji, wasiojizuia, wakali, wasio penda mema, wasaliti, wakaidi, wenye kujivunia, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu, wenye mfano wa utauwa, lakini walikana nguvu zake”.

(2 Timotheo 3:1-5).

Ukiangalia kwa makini, maelezo yanayotolewa kuelezea kila neno la unabii wa Biblia, maelezo hayo yanalenga mambo yalivyo wakati huu wetu kuliko wakati mwingine wowote.

s

## 2. ISHARA INAYOHUSU WAYAHUDI

Yesu alizungumzia juu ya kurudi kwake kwa mfano mfupi kama ishara ziada kwa wanafunzi wake:

“Basi kwa mtini jifunzeni mfano; tawi lake likiisha kuchipuka na kuchanua majani, mwatambua ya kuwa wakati wa mavuno u karibu” (Mathayo 24:32).

Nabii Yeremia anatupa fununu ya kuweza kuutambua mtini kwani anatumia ishara iyo hiyo ya mlango wa 24 anapotaja wana wa Israeli (Kasome pia Yoeli mlango wa 1:7). Hebu basi tuangalie mfano huu wa mtini, Israeli, inapochipuka “na kuchanua majani.”

Mfano huu unatuelekeza lwa Wayahudi kutoka pembe zote za dunia abako walitawanywa na Mungu (Luka 21:24; Kimbukumbu 28:25, 32-34, 37, 64-66). Walio wengi wakati huu wanashuhudia Wayahudi katika nchi ya Israeli wakiwa katika hali ya “Kuchanua majani” wanapoendelea kujenga nchi yao tangu iwe taifa mwaka wa 1948 na kutwaliwa kwa mji wa Yerusalemu mwaka wa 1967.

Tukio hili lilitabiriwa na Ezekieli katika mistari ya kwanza 14 katika mlango wa 37. Wakati huu taifa la kiyahudi lafananishwa na mhusanyiko wa mifupa. Nabii huyu aliona bonde la mifupa mikavu:

“Mifupa hii ni nyumba yote ya Israeli; tazama, wao husema, mifupa yetu imekauka, matumaini yetu yamepotea”. (Ezakieli 37:11).

Mifupa yajikusanya, na kupata nyama; pumzi yatiwa ndani ya Waisraeli na wanapata kuishi,

“Nami nitatia roho yangu mdani yenu, nanyi mtaishi, nami ntawawekeni katika nchi yenu.”

“Tazama, nitawatwaa wana wa Israeli toka kati ya mataifa walikokwenda, nami nitawakusanya pande zote, na kuwaleta katika nchi yao wenyewe” (Ezakiel 34:14 & 21).

Kwa hivyo kwa lugha ya mafumbo twaona wana wa Israeli walirejeshwa katika nchi yao ya ahadi na Mungu, taifa changa linalochipuka kama tawi.Nini inafuata mkusanyiko huu? “Tena nitafanya agano la amani pamoja nao…na patakatifu pangu nitapaweka katikati yao milele” (Ezakiel 37:26).

Ishara hii ya Wayahudi inaashiria kuimarishwa kwa ufalme wa Mungu.

Sehemu inayosisimua ya unabii huu ni kuwa twauona mkono wa Mungu ukifanya kazi ya kuwarejesha Wayahudi na kuijenga nchi yao; na twaonywa,

“Nanyi kadhalika myaonapo hayo yote, tambueni ya kuwa yu (Yesu) karibu, milangoni” (Mathayo 24:33).

## UNABII WA YESU KUHUSU ISRAELI

Yesu alitabiri kuhusu yatakayotokea katika taifa la Israeli kwa mhula mfupi na mrefu. Viongozi wa taifa hawakuweza kuuona mkono wa Mungu wao ukiwa umewanyoshea. Alikuwa amewatumia Mwana Wake wa pekee Kama Masiya wao lakini wao wakataka aondolewe Kwa kunawa. Kabla ya kukamatwa na kusulubiwa kwake, Yesu akiwa na wanafunzi wake walisimama juu ya mlima uliokuwa umekabiliana na Yerusalemu; wanafunzi wake walipoona urembo wa majengo ya hekalu waliyastaajabia; Yesu naye aliona vingine, aliona adhabu iliyokuwa inawajia watu wake:

“Haya mnayoyatazama, siku zitakuja ambapo hautasalia jiwe juu ya jiwe ambalo alitabomoshwa.”

“Wataanguka kwa ukali wa upanga nao watatekwa nyara na kuchukuliwa katika mataifa yote; na Yerusalemu utakanyagwa na Mataifa, hata majira ya Mataifa yatakapotimia” (Luka 21:6, 24).

Utabiri huu ulitimia mwaka wa sabini wa bwana yetu wakati ambapo Ufalme wa Warumi ulituma jeshi lake chini ya Tito ili kuzima uasi. Mji wa Yerusalemu ukaangamizwa na kulimwa haswa. Yaliyoandikwa katika kitabu cha Kumbukumbu 28 yakatimizwa; kutawanywa kwa taifa kukamilika. Hapana Myahudi aliyeruhusiwa kusalia katika nchi hiyo. Katika mwaka wa 135 amri ikatolewa ya kuwa Myahudi yeyote aliyepona asionekane Uyahudini. Jina la mji wa Yerusalemu likabadilishwa na kuwa Aelia Kapitolina.

Karne zilizofuatia zikawa za kuwakandamiza watu na nchi yao. Kutawanyika kwao ikawa kama sheria. Wayahudi waliokuwa wakitekwa nyara vitani katika vita vyovyote vile walitawanywa ulimwenguni kama watumwa. Waliobahatika kufanywa watumwa wakawa makabaila na wafanyi biashara. Ungempata Myahudi kote ulimwenguni isipokuwa katika nchi ya Israeli - Neno lake Mungu likatimizwa kwa hakika. Makaazi yao yakawa kote ulimwenguni lakini katika hali ya kukosa starehe kama alivyoagiza Mungu. Maisha yao

yakawa yakudhulumiwa na kuchukiwa kama Wayahudi. Kwa miaka 2,000 nchi na watu wake wakawa wamepondwa vilivyo na kilichohitajika ni muujiza tu ndipo wanusurike. Na muujiza huu ulikuwa umetabiriwa na manabii wa mwenyezi Mungu. Katika mwaka wa 1967 Waisraeli waliukomboa mji wa Yerusalemu, na kwa mara ya kwanza kwa miaka 2000 hivi, Yerusalemu ikawa chini ya himaya ya Israeli.

**2. KUZALIWA UPYA KWA ISRAELI**

Mambo yanayopata uwazi zaidi kwa maneno ya unabii ya Yeremia. "….. Tazama, nitawakusanya na kuwatoa katika nchi zote nilikowafukuza katika hasira yangu, na uchungu wangu, na ghadhabu yangu nyingi; nami nitawaleta tena hata mahali hapa, nami nitawakalisha salama salamini" (Yeremia 32:37).

Mungu alikuwa amesema, atawapa moyo mpya na roho mpya ili wapate kuokoka, na jambo la kustaajabia ni jinsi taifa hili limekuwa na ujasiri na nguvu ya kupigiwa hadidhi. Kwa miaka 2,000 hivi ya matakwa ya Wayahudi yamekuwa katika hali ya unyonge na ya kutoweza kujitetea. Lakini wakati wa kutimizwa kwa yale yaliyonenwa kwa vinywa vya manabii kurejeshwa katika nchi yao, hii roho mpya ikaingia katika taifa hili. Wakafanya vitu hivi kuhakikisha wamerejesha nchi yao- na Uingereza, mkoloni wakati huo, ulifurahia kuwapa. Kisha, taifa hili likageuka na kuwa mashine ya vita kwa kushinda muungano wa mataifa ya kiarabu na Misri. Wayahudi 650,000 walikabiliana na Waarabu 40,000,000; na kama alivyokuwa akifanya awali, Mungu aliwapa ushindi. Kwa hivyo, yaliyonenwa na manabii, yakatimizwa. Milango ya 36 na 37 ya Ezekiali ina unabii wa ajabu, inavyoonyesha pasi na shaka uwezo wa Mungu katika mambo ya mataifa. Nabii alipewa maono ambayo yalionyesha Mungu atawakusanya kuwa taifa katika nchi yao wenyewe, na wawe jeshi kubwa; "Maana nitawatwaa kati ya mataifa, nami nitawakusanya na kuwatoa katika nchi zote, na kuwarudisha katika nchi yenu wenyewe…. Nami nitawapa ninyi moyo mpya, nami nitatia roho mpya ndani yenu, nami nitatoa moyo wa jiwe uliomo ndani ya mwili wenu, nami nitawapa moyo wa nyama…. Nanyi mtakaa katika nchi ile niliyowapa baba zenu." (Ezakieli 36:24,26,28).

Halafu katika maono ya bonde lile lililojaa mifupa iliyakauka iliogeuka kuwa bonde lililojaa jeshi kubwa, Mungu akazidi kutoa hakikisho:

"Wakasimama kwa miguu yao, jeshi kubwa mno…nami nitawawekeni katika nchi yenu….nitawatwaa wama wa Israeli….na kuwaleta nchi yao wenyewe". (Ezekieli 37:10,14,21).

Tangu mwaka wa 1948, takribani Wayahudi millioni sita wamerejeshwa Israeli - tukio kuu linalotazaniwa ni lile la Kristo kurudi tena ili aimarishe Ufalme katika nchi ya Israeli na himaya yake ifikie miisho ya ulimwengu.

**3. ISHARA YA NDOTO YA NEBUKADNEZA**

Somo la 3 lilishugulikia kwa mapana na marefu juu ya ndoto hii. Tafsiri ya Danieli ilionyesha mkondo wa historia ya ulimwengu. Baada ya kuangushwa kwa ufalme wa Warumi twajikuta hivi leo tukiwakilishwa kwa miguu ya sanamu ile, tukiwa na mataifa yenye nguvu (chuma) na

yale dhaifu (udongo), yasipoweza kushikamana vema. Danieli aliendelea:

“Na katika siku za wafalme hao, Mungu wa mbinguni atausimamisha ufalme.” (Danieli 2:44).

Hii inamaanisha ya kuwa hapatakuwepo tena na ufalme mwingine ulimwenguni, hadi tukio hilo ambalo litatimiza unabii wa Danieli. Kwa kuwa Paulo, aliyekuwa mtume, alikuwa na uhakika na kutumia kwa unabii huu kufikia wakati wake, aliweza kuwapa moyo waumini Wakolosai kwani alikuwa hana shaka na kurudi tena kwa Kristo:

“Kristo atakapofunuliwa, aliye uhai wetu, ndipo na ninyi mtafunuliwa pamoja naye katika utukufu.” (Wakolosai 3:4).

## 4. ISHARA YA MSUKOSUKO ULIMWENGUNI

Kristo pia aliwaambia wanafunzi wake kuhusu wakati kabla ya marejeo yake ambapo kutakuwepo na misukosuko na hofu iliyotanda kwa sababu ya matatizo yanayoyakumba mataifa yote:

“Tena, kutakuwa na ishara katika jua, na mwezi, na nyota; na katika nchi dhiki ya mataifa wakishangaa kwa uvumi wa bahari na msukosuko wake; watu walivunjika moyo kwa hofu, na kwa kutazamia mambo yatakayoupata ulimwengu. Kwa kuwa nguvu za mbiguni zitatikisika” (Luka 21:25-26).

Kristo anazungumza kwa mafumbo kuhusu watawala huku bahari na mawimbi yake yaliwakilisha watu. (k.m Isaya 54:20).

Ishara hii yatoa taswira ya watu duniani wakihangaika, wakitumia umoja wa sauti zao kuonyesha uwezo wao juu ya matukio na hali mbalimbali, huku wakibabaisha usalama wa viongozi. Hali kama ilivyo ni ya kuvunja mioyo ya mataifa, inayowafanya watu waelekevu kuhofia matokeo ya machafuko na mizozo ulimwenguni.

Kwa hakika taswira inayotolewa yaweza kugonga vichwa vya habari kuhusu hali ilivyo ulimwenguni!

Kwa mara nyingine, Kristo atwambia kuwa mambo yakiwa ulimwenguni kama alivyoyaeleza, tutarajie kurudi kwake: “….hapo ndipo watakapomwona Mwana wa Adamu akija.” (Luka 21:27).

Kuimarishwa kwa ufalme wa Mungu nchini ndicho kiini cha nia Yake kama tulivyo kwisha kuona. Inahitaji kurudi tena kwa Yesu Kristo duniani ili atimize ahadi za Mungu. Yesu mwenyewe alisema - katika unabii juu ya matukio ambayo hayana budi kutokea kabla ya kurejea kwake duniani.

## 5. MGOGORO UJAO ULIMWENGUNI

Tuliona katika kile ambacho kimekuja kujulikana kama ‘**Unabii wa Mlima wa Mizeituni’**,

Yesu akionya kwanza kuangushwa kwa taifa la Kiyahudi. Ili kutimiza maandiko, Warumi walitawala katika nchi ya Palestina na Wayahudi walikuwa taifa la kitumwa. Yesu alifahamu kuwa haitachukua muda mrefu kabla ya Warumi kutekelezea mpango huu wa Mungu kwa kuwatawanya wana wa Mungu ulimwenguni mwote:

"Wataanguka kwa ukali wa upanga, nao watatekwa nyara na kuchukuliwa katika mataifa yote; na Yerusalemu utakanyagwa na mataifa, hata majira ya majira ya mataifa yatakapotimia. Tena kutakuwa na ishara……" (Luka 21:24,25).

Wanafunzi wa Yesu walikuwa wameuliza juu ya ishara za kurudi kwake na mwisho wa ulimwengu. Yesu hakusita kueleza kinaganaga ishara zitakazoambatana na kurudi kwake katika 'nguvu na utukufu mwingi':

"Tena, kutakuwa .na ishara katika jua na mwezi; na nyota; na katika nchi dhidi ya mataifa wakishangaa kwa uvumi wa bahari na msukosuko wake; watu wakivujika mioyo kwa hofu na kwa kutazamia mambo yatakayoupata ulimwengu. Kwa kuwa nguvu za mbinguni zitatikisika. Hapo ndipo watakapomwona Mwana wa Adamu akija katika wingu pamoja na nguvu na utukufu mwingi". (Luka 21:25-27).

Kurudi kwa Wayahudi katika nchi yao wenyewe na kurejeshwa kwa Israeli kama maskani ya watu wa Kiyahudi mwaka wa 1948 na kutimizwa kwa unabii ambao tayari tumetaja katika Somo hili. Katika miongo amayo imefuata tukio hilo, ishara zimeshuhudiwa 'mbinguni' na kati ya nembu za tawala za mataifa, jua, mwezi na nyota. Kama misukosuko jinsi migogoro ya ulimwengu itakavyosuluhishwa na serikali za wanadamu. Vita vyaendelea- havikomi- na suluhu haipatikani. Yesu alisema hii pia itakuwa mojawapo ya ishara ya kurudi kwake.

Manabii wa Israeli wamezungumzia tangu kitambo mambo yanayowahusu wana wa Israeli na mataifa YOTE, kabla ya kuja kwa Kristo wakitaja zama ziitwazo 'siku za mwisho' au 'siku zile' . Chukulia mfano huu:

"Mwanadamu, hasa uso wako, umwelekee Gogu, wa nchi ya Magogu, mkuu wa Roshi, Mesheki, na Tubali, utatabiri juu yake, useme, Bwana MUNGU asema hivi……" (Ezakiel 38:2,3).

Usomaji makini wa mlango huu waonyesha bayana pasi na shaka yoyote kuwa msururu wa mataifa haya- kama vile Uajemi (Iran), Ethopia na Libya (Ezakiel 38:5)- yatalazimishwa na Mungu kuishambulia nchi ya Israeli. Kwa mfano, katika mstari wa 8 twasoma hivi:

"Katika **Miaka Ya Mwisho,** utaingia nchi iliyorudishiwa hali yake ya kwanza, baada ya kupigwa kwa upanga, ilivyokusanywa toka kabila nyingi za watu, juu ya milima ya Israeli, iliyokuwa ukiwa wa daima; lakini imetolewa katika kabila za watu…". (Ezakieli 38.8).

Hili shirikisho la mataifa litaongozwa na taifa lililo kaskazini mwa NCHI TAKATIFU (Israeli), ni jambo la kutilia uchunguzi wa kina, Israeli tangu hapo na hata sasa, imehitajika kuangalia kwa makini wale walio KASKAZINI mwake kuhusu usalama wake. Syria kwa sasa ndio tisho lao kama walivyokuwa waashuri miaka 2,500 iliyopita.

Akizungumzia wachokozi hawa kutoka 'kaskazini', Mungu kwa kupitia kwa nabii Ezakieli alisema:

"Nawe utakuja kutoka mahali pako kutoka pande za mwisho za KASKAZINI, wewe na watu wa kabila nyingi pamoja nawe…utapanda juu,uwajilie watu wangu, Israeli, kama wingu kuifunika nchi; itakuwa katika SIKU ZA MWISHO" (Ezekiel 38:15,16).

Kutambua shirikisho hili la mataifa mataifa yatakayokuja kinyume cha Israeli hivi karibuni si shida. Gogu, Magovu, Masheki na Tubali inatambuliwa na wasomi wa historia ya kale kama uzao wa wana wa Nuhu, kupitia kwa Yafethi.

Uajemi (Iran), Ethiopia na Lybia ambao kwa muda sasa wamekuwa mahasimu wa Israeli ni jambo linalojulikana leo, na nabii Ezakieli akizungumza kwa nguvu za Mwenyezi Mungu, anatwambia wataungana na uzao wa Yafethi, katika SIKU ZA MWISHO, wanaokaa 'pande za mwisho za kaskazini'.

Kwa sasa Syria iko upande wa Kaskazini mwa Israeli, moja wapo ya adui wa kiarabu wa Israeli. Ukisonga kaskazini zaidi, kina Armenia, na kufikia mataifa mengi yaliyoondoka kutoka kwa muungano wa mataifa ya Kisoviet- USSR. Twaona kuwa mataifa haya yana mlengo wa kiislamu.

Itakuwa jambo la kipumbavu kwa wanafunzi wa unabii kulazimisha kauli kwa matokeo ya unabii wa biblia. Ni Mungu tu aliye na haki ya kutoa uamzi kuhusu matokeo ya mpango wake na ulimwengu huu, mpango ambao tukumbuke ya kuwa utakamilika pale ambapo Ufalme wa Mungu utasimamishwa hapa duniani. Milenia au miaka elfu moja ya utawala wa Kristo duniani. Ikiwa sisi tu wanafunzi wa kweli wa Neno la Mungu, basi sisi tu wainda doria. Kristo alitoa onyo kwa wanafunzi wake akiwaambia, Kesheni! – "Kesheni basi; kwa maana hamjui ni siku ipi atakayokuja Bwana wenu." (Mathayo 24:42).

Tunapochunguza matukio ulimwenguni twaona nini? Twaona Israeli, wamerejea katika nchi yao wenyewe kutimiza unabii kama ule wa Ezakieli katika mlango wa 37. Twaona uhasama dhidi ya Israeli katika mipaka yake yote. Waarabu (waislamu), mataifa yao kusema kweli ni shirikisho lililo kinyume na watu wa Mungu, na wamejitahidi kuwasukumia mbali waangamie baharini:

"Wamesema njoni, tuwakatalie mbali wasiwe taifa; na jina la Israeli halitakumbukwa tena." (Zaburi 83:4).

Mwanafunzi makini wa unabii wa Biblia atafaidi uhondo wa maelezo zaidi akipitia mlango wa Zaburi 83, hasa akijaribu kutambua mataifa ya kisasa yanayotajwa katika Zaburi hii ya kuvutia sana.

Ni mataifa mahasimu a Israeli kutokana na historia ya azali na wanaweza kutambuliwa kwa mipaka yao na adui sasa wa watu wa Mungu.

Mchokozi; dhalimu kutoka kaskazini kutoka wa mlango wa 38 wa Ezakieli akiwa na wengine ambao wanabarikiwa wazi kutokana na mataifa ya kisasi yasiyo na wakati na nchi ambayo

imerejeshwa kutoka upanga wa kukaa salama, ndio watakaoletwa ili kufanya vitu na Yerusalemu.

“Kwa maana mtawakusanya mataifa yote walete vita juu ya Yerusalemu” (Zakaria 14:2).

“Kwa maana, angalieni, siku na wakati ule, nitakapowarudisha mateka wa Yuda na Yerusalemu, nitakusanya mataifa yote, nami nitawaleta chini katika bonde la Yerusalemu….”(Joeli 3:1,2).

Bila shaka hii ni siku ambayo Mungu ataingilia kati tena katika mambo ya wanadamu na kuhakikisha mapenzi YAKE yanatimizwa duniani:

“Makutano, makubwa, makutano makubwa, wamo katika bonde la kukata maneno! Kwa maana siku ya BWANA i karibu….” (Yoeli 3:14).

“Naye BWANA atanguruma toka Sayuni, atatoa sauti yake toka Yerusalemu; na mbingu na nchi zitatetemeka; lakini Bwana atakuwa kimbilio la watu wake na ngome ya wana wa Israeli. Hivyo ndivyo mtakavyojua ya kuwa mimi ndimi Bwana Mungu wenu, nikaaye Sayuni, mlima wangu mtakatifu; ndipo Yerusalemu utakapokuwa mtakatifu, wale wageni hawatapita ndani yake tena kamwe.” (Yoeli 3:16-17).

Nyakati hizi ndizo za kumwona Kristo, mfame ajae kutawala dunia. Unabii huu, hasa ule wa Yoeli na Zakaria, ongeza ule wa Isaya, Yeremia na Ezakieli, unatuchorea MPANGO WA MUNGU. Kama walinda doria, inatupasa kuchanganua kila hatua ijao ya mpango huu. Kila hatua tunayopiga inatuletea karibu siku hiyo ya mgogoro mkuu na wa mwisho unaojulikana katika Biblia kama Hari - magedoni; hatima yake ikiwa, kama anavyoeleza Zakaria:

“…..Naye BWANA atakuwa Mfalme juu ya nchi yote; siku hiyo BWANA atakuwa mmoja, na jina lake moja”. (Zakaria 14:9).

## KURUDI KWA KRISTO NI UKWELI USIOEPUKIKA

Ishara za nyakati za mwisho zinakielezo au mwelekeo wa mambo yajayo. Mambo ya mwanzo ya utangulizi kabla ya Mungu kuingilia kati mambo ya wanadamu yanakaribia kutimia na Yesu Kristo yuko mlangoni, tayari kuwazimbua walimwengu.

Je, tukijua ishara hizi na kufahamu maana yake, twaweza kutoa atarehe starehe bila kutetemeka? Itakuwa kama wale wapumbavu ambao wanayapuuza kwa kutoyawazia hata chembe. Kwa watu sampuli hii, kurudi kwake Yesu kutawafikia kama mwizi ajaye usiku.

Kwa upande mwingine, twaweza kuchukulia maanani ishara hizi na kufanya vitu kwa maonyo kabla ya wakati kupita. Yesu alisema, “Basi mambo hayo YAANZAPO KUTOKEA, changamkeni, mkaviinue vichwa vyenu, kwa kuwa ukombozi wenu umekaribia.” (Luka 21:28). Badala ya kuvunjika kwa matukio yaliyopo sasa, twaweza kuinua macho yetu na kuangalia haja yetu ya ukombozi katika Kristo ambaye ndiye Mkombozi wetu. Twaweza kuwa wenye hekima na kukimbilia safina ya Kristo kabla ya siku hiyo kuu ya Mwnyezi

Mungu itakayowameza waovu.

Kuna uwezo wa kuangalia mada hii kama ya muhimu sana, tukikumbuka kuwa inatuahidi matumaini ya uzima wa milele na kipenyo katika Ufalme wa Mungu – Ufalme ambao Kristo ndiye atakayekuwa mtawala wa haki na amani, sio utawala wa neema mioyoni mwetu bali utwala halisi juu ya nchi.

Wenye hekima wataufikia uamzi huu:

i. Ya kuwa kurudi kwake Kristo ni jambo la muhimu

ii. Ya kuwa tahadhari kutoka katika Neno la Mungu isipuuzwe

iii. Ya kuwa maisha yetu ya sasa hayaridhishi kabisa

iv. Ya kuwa kuamini Injili (Habari Njema) ya Ufalme wa Mungu na kubatizwa (kuchovya) katika jina la Kristo ni lazima.

Uamuzi ni wa kibinafsi ikiwa twataka "kustahimili siku ya kuja kwake Kristo", ambapo "mtapanbanua kati ya wenye haki na waovu, na kati ya yeye mtumikiaye Mungu na yeye asiyemtumikia". (Malaki 3:18).

## MUHTASARI

1. Kurudi kwake Yesu ni hakika.

2. Ahadi ya kurudi huku ilitolewa na malaika wakati wa kupaa kwake (Yesu) mbinguni.

3. Yesu atarudi kuimarisha ufalme wa Mungu duniani.

4. Ni Mungu peke yake anayejua siku aliyoweka ya kurudi kwa Kristo.

5. Ishara maridhawa zaonyesha kurudi kwa Kristo kunakaribia sana.

6. Siku za Nuhu zalinganiswa na siku hizi zetu.

7. Kurejeswa kwa Wayahudi katika nchi ya Israeli ni ishara tunayoiona bayana.

8. Twaishi katika siku za mwisho za maono ya Nebukadineza.

9. Misukosuko ulimwenguni zatangulia kabla ya kurudi kwa

Kristo.

10. Uhasama wa majirani wa israeli.

# Kitihani cha somo la 9.

Pigia mstari jibu lililo sahihi kwa kila swali lililoulizwa kisha uhamishe majibu hadi hati ya muhtasari ya majibu iliyo katikati ya kurasa za hizi.

1. **Kwa nini Yesu yuarudi hapa duniani?**
   (a) Hatarudi tena
   (b) Kusimamisha vita
   (c) Kusimamisha Ufalme wa Mungu
   (d) Kuponya magonjwa
2. **Ni nani ajuaye tarehe au siku atakaporudi Yesu?**
   (a) Malaika
   (b) Yesu
   (c) Mungu
   (d) Paulo
3. **Ishara za kuja kwake Yesu twazipata wapi?**
   (a) Katika Biblia
   (b) Magazetini
   (c) Katika nyota
   (d) Katika sheria za Kiyahudi
4. **Ni hali gani iliyomo ulimwenguni ambayo Yesu aliilinganisha na nyakati za Nuhu?**

(a) Kurudi kwa Israeli katika nchi yao

(b) Kutokea kwa dhalimi wa nchi ya kaskazini

(c) Wakati wa dhiki na kupenda raha

(d) Mataifa mengine kuwa yenye nguvu na mengine dhaifu.

**5. Katika mfano alioutoa Yesu, alitumia ishara ipi kuwasawiri Waisraeli katika Mathayo 24:32-33?**

(a) Bonde la mifupa iliyokauka

(b) Mtini

(c) Mshumaa

(d) Safina

**6. Katika maono ya Nebukadineza ni sehemu gani yaonyesha wakati wa kurudi kwa Yesu?**

(a) Kichwa cha dhahabu

(b) Miguu ikiwa na chuma na udongo

(c) Miguu ya chuma

(d) Tumbo na mapaja ya shaba

**7. Katika Luka 21:25, ni watu wa aina gani au tabaka lipi wanaotajwa kama 'bahari na msukosuko wake'?**

(a) Watu watakatifu

(b) Waovu

(c) Watawala

(d) Wamishonari

**8. Ni taifa lipi lililoko kaskazini mwa nchi ya Israeli?**

(a) Marekani

(b) Syria

(c) Misri

(d) Urusi

9. **'Mikaeli' anayetajwa katika kitabu cha Danieli 12:1 ni nani?**

    (a) Nuhu

    (b) Ezakieli

    (c) Danieli

    (d) Yesu

10. **Ishara zipi kati ya hizi zaonyesha kurudi kwa Yesu siku hizi za leo?**

    (a) Kurejeshwa kwa Wayahudi katika Israeli

    (b) Misukosuko ya ulimwengu

    (c) Hali ya majirani wa Israeli

    (d) Mataifa mengine yana nguvu, mengine dhaifu.

**SOMO LA 10.**

# INJILI

Katika somo hili, tutakusanya maudhui yote tuliyothibitisha au ukweli tulioupata kutokana na masomo yaliyotangulia.

Neno "Injili" linamaanisha 'habari njema'. Neno asili ya habari njema kwa Kiyunani ni '*enaggelion*'. Kwa Kiingereza ni 'gospel' ikiwa na maana ya '*god spell*'. –Abjad Nzuri.

# KIINI CHA MAFUNZO YA KRISTO

Mathayo, Marko, Luka na Yohana wanatuambia kuwa Yesu alienda kotekote katika nchi ya Israeli akihubiri injili- habari njema- juu ya ufalme wake ujao.

"Naye Yesu alikuwa akizunguka katika miji yote na vijiji, akifundisha katika masinagogi yao, na kuihubiri habari njema ya ufalme" (Mathayo 9:35).

"Yesu akaenda Galilaya, akiihubiri, Habari Njema ya Mungu" (Mariko 1:14).

"Roho wa bwana yu juu yangu, kwa maana amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari

njema”(Luka 4:18).

“Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe wa pekee ili kila mtu amwaminiye, asipotee bali awe na uzima wa milele” (Yohana 3:16).

“Wewe wasema, kwa kuwa mimi ni mfalme. Mimi nimezaliwa kwa ajili ya haya, na kwa ajili ya haya mimi nalikuja ulimwenguni ili niishuhudie kweli” (Yohana 18:37).

## WANAFUNZI WALIWAFUNZA WATU INJILI.

Yesu akisha waambia wanafunzi wake habari njema, aliwatuma kuwafunza wengine. “Akawatuma wautangaze ufalme wa Mungu, na kupoza wagonjwa” (Luka 9:2).

Baada ya kifo chake na ufufuo, Yesu aliwambia wanafunzi wake waendelee na kazi iyo hiyo.

“Enendeni ulimwenguni mwote mkahubiri Injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa” (Marko 16:15-16).

Kutokana na maneno haya ya mwisho twaona kuwa twahitajika kufahamu, kuamini na kutii injili ikiwa twataka kuokolewa.

## UWEZO WA INJILI

Kwa sababu ya holi, mtume Paulo aliandika: “Kwa maana siionei haya injili; kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu, kwa kila aaminiye, kwa Myahudi kwanza na kwa Myunani pia” (Warumi 1:16).

Inatupasa kuelewa kinaganaga habari njema aliyofunzwa na Yesu na mitume. Paulo aliandika tena: “Lakini ijapokuwa sisi au malaika wa mbinguni tawahubiri ninyi injili yoyote isipokuwa hiyo tuliyowahubiri na alaaniwe” (Wagalatia 1:8).

## WANAFUNZI WA YESU WALIELEWA ‘INJILI’ KUWA NINI?

Wanafunzi walienda kotekote kutangaza habari njema ya ufalme wa Mungu, kabla ya kusulubiwa kwake Yesu. ‘Habari Njema’ hii ilikuwa na maana gani kwao? Wawili wao waliozungumza na Yesu baada ya ufufuo wake walimwambia,

“Mambo ya Yesu wa Nazareti aliyekuwa mtu nabii, mwenye uwezo katika kutenda na kunena mbele za Mungu na watu wote...Nasi tulikuwa tukitumaini ya kuwa yeye ndiye atakayewakomboa Waisraeli” (Luka 24:19,21).

Kabla Yesu hajapaa kwenda mbinguni, “Wakamwuliza, wakisema, Je! Bwana, wakati huu ndipo unapowarudishia Waisraeli Ufalme?” (Matendo 1:6).

Walitarajia Yesu kusimamisha ufalme wa Mungu papo na hapo. Hii ilikuwa habari njema kweli kweli na waliitaka mara moja. Yesu aliwaambia kuwa wakati ulikuwa haujawadia. “Si kazi yenu kujua nyakati ala majira, Baba aliyaweka katika mamlaka yake mwenyewe” (Matendo 1:7).

## AHADI ZA MUNGU

Walipokuwa (wanafunzi) wamekaza macho yao wakimtazama Yesu alipokuwa akipaa, malaika wawili waliasimama mbele yao wakawambia,

“Huyu Yesu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja jinsi iyo hiyo mlivyomwona akienda zake mbinguni” (Matendo 1:11).

Ahadi hii ni kiini au mada inayorudiwarudiwa na mitume katika mafundissho yao kama tunavyosoma katika Matendo ya Mitume na katika nyaraka zao. Walitazamia kurudi mara ya pili kwake Yesu ili atimize ahadi aliyotoa Mungu kuhusu Ufalme Wake.

Ingawa neno injili lapatikana katika Agano Jipya hasa, habari njema ya ufalme wa Mungu ndio msingi wa ahadi zote za Mungu tangu mwanzo.

## INJILI KATIKA BUSTANI YA EDENI

Hapo mwanzo, baada ya Adamu na Hawa kumwasi Mungu, twayakumbuka maneno Yake kwa nyoka,

“Nami nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke, na kati ya uzao wake; huo utakuponda kichwa na wewe utamponda kisigino” (Mwanzo 3:15).

Hii ndiyo habari njema kuwa nguvu za dhambi na mauti zitaangamizwa hatimaye. Hii ndiyo kazi ambayo Yesu alikuja kuifanya. Anangalia Waebrania 2:14-15.

## INJILI KWA IBRAHIMU

Tumejifuza kuhusu ahadi za Mungu kwa Ibrahimu. Mtume Paulo aliandika, “Na andiko, kwa vile lilivyoona tangu zamani kwamba Mungu atawahesabia haki mataifa kwa imani lilimhubiri Ibrahimu habari njema zamani, kusema, katika wewe Mataifa yote yatabarikiwa” (Wagalatia 3:8).

Yesu atakaporudi atamfufua Ibrahimu kutoka kwa wafu, na ahadi zote kwa Ibrahimu zitatimizwa kikamilifu.

Ahadi hizi zilithibitishwa kwa Isaka na kwa Yakobo, nao pia watafufuliwa kutoka kwa wafu Yesu arudipo, na watapokea nafasi zao za hadhi katika Ufalme wa Mungu. (Mathayo 8:11)

# INJILI KWA DAUDI

Aliyemwambia Daudi habari njema ya Ufalme wa Mungu alikuwa nabii Nathan - Kasome 2 Samweli 7:12-16.

“Nitainua mzao wako…nami nitaufanya imara ufalme wake...na nyumba yako, na ufalme wako, vitathibitishwa milele mbele yako: na kiti chako kitafanywa imara milele.”

Ingawa Waisraeli walikana Mungu baadaye, hakusahau ahadi zake, kitabu cha Zaburi za Daudi na maandishi ya manabii yanarudiarudia mambo haya na kumbukumbu hii Mungu, kupitia kwa nabii Ezekieli alimwambia Zedekia, mfalme wa mwisho wa Yuda, “Nitakipindua, nitakipindua, nitakipindua; hiki nacho hakitakuwa tena, hata atakapokuja yeye ambaye ni haki yake; nami nitampa.” (Ezekieli 21:27).

Yesu alipokuja, malaika alikiri ahadi kwa Mariamu,

“Huyo atakuwa mkuu, ataitwa Mwana wa Aliye juu, na Bwana Mungu atampa kiti cha enzi cha Daudi, baba yake. Ataimiliki nyumba ya Yakobo hata milele, na ufalme wake utakuwa hauna mwisho” (Luka 1:32-33).

# INJILI KWETU SISI

Hii ndiyo habari njema ya ufalme wa Mungu iliyotujia sisi katika ujumbe wa Biblia. Yesu yuaja tena duniani hivi karibuni kusimamisha ufalme wa Mungu. Hebu soma Mathayo 25. Mifano huu watufunza kukesha, kutenda kazi na kuangaza upendo wa Kristo ikiwa twataka kushiriki katika Ufalme wa Mungu.

1. **Mfano wa wanawali kumi**

Wale waliojitayarisha vema na wakawa katika kukesha walialikwa karamuni lakini wale ambao mafuta yao yalikwisha waliukuta mlango umefungwa.

2. **Mfano wa Talanta**

Kutumia uwezo au vipaji vyyetu vyema kutatambuliwa na Yesu na atawalipa mema wale waliotumia maarifa na nafasi zao vilivyo.

3. **Mfano wa Mchungaji akiwatenga kondoo**

Mchungaji mwema huwajua kondoo wake na anaelewa uwezo wao. Anatambua jitihada zao za kuwasaidia wengine na atakubali msaada huo kana kwamba alitendewa yeye.

# TUFANYEJE?

Imetupasa kuttubu, tubadilishe mienendo yetu, “wakati umetimia, na ufalme wa Mungu

umekaribia; tubuni, na kuiamini Injili" (Marko 1:5).

"Tubuni basi, mredjee, ili dhambi zenu zifutwe, zipate kuja nyakati za kuburudishwa kwa kuwako kwake Bwana; apate kumtuma Kristo Yesu mliyewekewa tangu zamani."(Matendo 3:19,20).

"Baba, zamani zile za ujinga Mungu alijifanya kama hazioni, bali sasa anawaangalia watu wote wa kila mahali watubu. Kwa maana ameweka siku atakayowahukumu walimwengu kwa haki, kwa mtu yale aliyemchagua" (Matendo 17:30-31).

Inafaa tumfuate Yesu - kugeuza mioyo na mawazo yetu - tuzaliwe upya kupitia kwa ubatizo, na somo letu lifuatalo, litatufunza maana ya hili. Hii pia ni muhimu.

"Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmevaa Kristo...Na kama ninyi ni wa Kristo, basi, mmekuwa uzao wa Ibrahimu, na warithi sawasawa na ahadi" (Wagalatia 3:27-29).

Hii ndiyo injili, habari njema ya ufalme wa Mungu. Sisi, kama walivyotazamia wanafunzi, twatamani Ufalme huu uje mapema. Ndio sababu twaomba, kama vile Yesu alivyowafunza wafuasi wake, "Ufalme wako uje."

"Baba yetu uliye mbinguni, Jina lako litakaswe, Ufalme wako uje. Mapenzi yako yatimizwe hapa duniani kama huko mbinguni. Utupe siku kwa siku riziki yetu. Utusamehe dhambi zetu, kwa kuwa sisi nasi tunamsamehe kila tumwiaye na usitutie majaribuni lakini tuokoe na yule mwovu" (Luka 11:2-4).

## MUHTASARI

1. Neno injili lina maanisha 'habari njema'.
2. Habari njema ya ufalme wa Mungu ujao ndio iliyokuwa mada kuu ya mafundisho ya Yesu na wafuasi wake.
3. Ufahamu, imani ya, na utiifu kwa injili ni muhimu ili kupata wokovu.
4. Injili yafunzwa katika Maandiko yote katika Agano la kale na Jipya.
5. Bado twatangaziwa habari njema.
6. Tutapata nafasi katika ufalme wa Mungu ikiwa tutasikia, tuelewe na kutii ujumbe wa injili.
7. Twafaa kuitilia mwito wa injili kwa wekelevu kama alivyofanya Ibrahimu na watumishi waaminifu wa Mungu wa zama zile.

**VIFUNGU VYA KUSOMA KATIKA BIBLIA**

8. 2 Samweli 7
9. Zaburi 96,1
10. Isaya 55
11. Matendo 9
12. Zaburi 1.

**KITIHANI CHA SOMO LA 10**

Pigia mstari jibu lililo sahihi kwa kila swali lililoulizwa kisha uhamishe majibu hadi hati ya muhtasari ya majibu iliyo katikati ya kurasa za hizi.

1. **Neno 'Injili' linamaanisha nini?**
   (a) Habari
   (b) Habari njema
   (c) Ahadi ya Mungu
   (d) Ujumbe
2. Zipi kati ya hivi vifungu yatueleza Yesu alihubiri Injili ya Ufalme?
   (a) Mathayo 1:14
   (b) Marko 1:14
   (c) Luka 1:14
   (d) Yohana 1:14
   (e) Mathayo 3:16
   (f) Marko 3:16
   (g) Luka 3:16
   (h) Yohana 3:16
   (i) Mathayo 4:18

(j) Marko 4:18

(k) Luka 4:18

(l) Yohana 4:18

(m) Mathayo 9:35

(n) Marko 9:35

(o) Luka 9:35

(p) Yohana 9:35

**3.** Mbali na Yesu, ni nani mwingine alihubiri Injili?

(a) Makuhani wa Kiyahudi

(b) Wanafunzi

(c) Wakuu wa Rumi

(d) Mamajuzi

**4.** Ufalme wa Mungu utasimamishwa duniani lini?

(a) Hatujui

(b) Yesu atakaporudi duniani

(c) Tayari ufalme upo

(d) Haitakuja

**5.** Nani aliwambia wanafunzi kuwa yesu waliyekuwa wakimwangalia akipaa mbinuni atarudi?

(a) Mungu

(b) Malaika

(c) Yesu

(d) Malaika wawili

**6.** Wawezaje kupokea ujumbe wa wokovu unaotolewa katika Biblia?

(a) Tenda mema kwa marafiki

(b) Gawa mali yetu yote

(c) Tii sheria za nchi

(d) Fahamu, amini na tii injili.

**7.** Ni ahadi ipi ya Mungu iliyotabiri kuwa nguvu za dhambi na mauti itakuwa ushindani kwa wanadamu?

(a) Ahadi katika Bustani ya Edeni

(b) Ahadi kwa Ibrahimu

(c) Ahadi kwa Nuhu

(d) Ahadi kwa Daudi

**8.** Ni vifungu vipi katika Agano Jipya vinavyotueleza ya kuwa Injili ilihubiriwa kwa Ibrahimu?

(a) Wagalatia 8:3

(b) Wagalatia 3:8

(c) Warumi 8:3

(d) Warumi 3:8

**9.** Ni nabii yupi wa Mungu aliyemwambia Daudi habari njema ya Ufalme wa Mungu?

(a) Danieli

(b) Isaya

(c) Eliya

(d) Nathani

**10.** Ni mwanafunzi yupi aliyemsaidia Sauli (Paulo) kupata ubatizo kama ilivyoandikwa katika mlango wa 9 wa kitabu cha Matendo?

(a) Petro

(b) Andrea

(c) Anania

(d) Yohana

**Somo la 11**

# UBATIZO

Katika somo letu lililotangulia, tuliona ya kuwa imani na ufahamu wa injili, kufuatiwa na utii amri za Mungu ni lazima kwa kupata wokovu. Twasoma maneno ya Yesu baada ya ufufuo wake yasemayo, “Endeni ulimwenguni mwote mkahubiri Injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka” (Marko 16:15-16).

Twaona mara moja ya kuwa ubatizo wa maandiko wawezekana tu baada ya mtu mume au mke kuelewa na kutii neno la Mungu. Ni masharti ya lazima kwa wote watakao kukubaliwa na Mungu.

Tuna mfano mwafaka kwa mtu aitwaye Kornelio, aliyekuwa mtu mwema,aliyekuwa akida wa kikosi kilichoitwa Kiitalia, aliyekuwa mtu ‘mwema’ kwa vipimo vyote (Matendo 10:2), lakini Mungu alimwagiza apeleke watu wamwite Petro, “atakuambia yakupasayo kutenda” (Matendo 10:6). Petro alikuja, na akafunza Kornelia juu ya Yesu.

“Akatwagiza tuwahubiri watu na kushuhudia ya kuwa huyu ndiye aliyeamriwa na Mungu awe mhukumu wa walio hai na wafu. Huyo manabii wote humshuhudia ya kwamba kwa jina lake kila amwaminiye atapata ondoleo la dhambi”.

Na bado haya hayakutosha , palisalia jambo la muhimu:

“Akaamuru wabatizwe kwa jina lake Yesu Kristo” (Matendo 10:42-48).

Kutokana na hili na maandishi mengine katika Matendo ya Mitume ni bayana kuwa Mungu ameweka utaratibu muhimu kwa hatua tatu za kufikilia wokovu: ufahamu, kuamini na ubatizo (soma Matendo 2:37-38,41; Matendo 8;35-38; Matendo 16:25-33).

# BATIZA

Nena la kiswahili limetolewa kwa neno la Kiyunani ‘batizo’ iliyo na maana ya kuchovya, kutumbukiza au kutosa majini kabisa. Inatumiwa Ugiriki au Uyunani kwa sanaa ya kutia rangi: Ukitaka kugeuza rangi ya jora, itakulazima kuitia rangi kwa kuichovya au kuitosa katika rangi ili jora lote likolee kwa rangi.

# UBATIZO

Matumizi ya neno hili katika Agano Jipya laonyesha kuwa matumizi ya kumwagilia maji au kunyunyiza haitoshi. Ubatizo wa kimaandiko wahitaji kumtosa mtu kabisa majini. Twasoma vile Filipo alivyombatiza towashi hivi.

"Wakatelemka wote wawili majini, Filipo na yule towashi, naye akambatiza." (Matendo 8:38)

Pia twasoma alivyofanya Yohana Mbatizaji, ya kuwa alikuwa akibatiza Ainoni, karibu na Salimu, "Kwa sababu huku kulikuwa na maji tele." (Yohana 3:23).

# UMUHIMU WA UBATIZO

Tukisoma kwa makini Agano Jipya, tutaona kuwa ubatizo una umuhimu mara nne.

## 1. Kuoshwa, Kutakaswa

**"**Simama, ubatizwe, ukaoswe dhambi zako, ukilitia jina lake." (Matendo 22:16)

"Au hamjui ya kuwa wadhalimu hawatauridhi ufalme wa Mungu?... na badhi yenu mlikuwa watu wa namna hii; lakini mlioswa, lakini mlitakaswa, lakini mkihesabiwa haki katika jina lake Bwana Yesu Kristo" (1 Wakorintho 6:9-11).

Matumizi ya mfano huu yanapatikana pia katika Agano la Kale hata katika Kugeuza rangi. "Jiosheni, jitakaseni ondoeni uovu wa matendo yenu usiwe mbele za macho yangu; acheni kutenda mabaya; jifunzeni kutenda mema… Dhambi zenu zijapokuwa nyekundu kama bendera, zitakuwa kama Sufu" (Isaya 1:16-18).

## 2. Kuunganika na Kristo Katika Mauti na Ufufuo Wake.

Kama inavyoonekana tumezikwa kabisa katika maji kwa kutenda hicho cha ubatizo, twafa kwa mfano, na tunapoinuka kutoka majini ni kama twainuka kwa upya wa uzima. Katika hali hii tunashiriki pamoja na Yesu katika kifo na kufufuka kwake. Mtume Paulo ameandika hivi:

"Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya Utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima kwa maana kama mlivyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaunganika kwa mfano wa kufufuka kwake"(Warumi 6:3-5).

Katika kitendo cha ubatizo tunapitia mfano wa kufufuka na kuenenda katika upya wa Uzima, mageuzi ya sura ambayo ni muhimu kwa upande wetu katika kumtii Mungu.

Yesu alisema, "Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuingia ufalme wa Mungu." (Yohana 3:5).

Paulo pia akiwaandikia waumini Wakolosai juu ya ubatizo akisema: "Mkazikwa pamoja naye katika ubatizo; na katika huo mkafufuliwa pamoja naye, kwa kuziamini nguvu za Mungu aliyemfufua katika wafu. Na ninyi mlipokuwa mmekufa kwa sababu ya makosa yenu na

kutotahiriwa kwa mwili wenu, aliwafanya hai pamoja naye, akiisha kutusamehewe makosa yote.” (Wakosai 2:12-13)

### 3. Tunaunganishwa Kwa Ubatizo Katika Kristo

Ubatizo unatuunganisha katika Kristo na kuwa jamaa wake na warithi sawasawa na ahadi alizotoa Mungu kupitia kwake.

“Maana kama vile mwili ni mmoja, nao una viungo vingi, na viungo vyote vya mwili ule, navyo ni vingi ni mwili mmoja, vivyo hivyo na Kristo. Kwa maana katika Roho mmoja sisi sote tulibatizwa kuwa mwili mmoja, kwamba tu Wayahudi au kwamba tu Wayunani; ikiwa tu watumwa au ikiwa tu huru; nasi sote tulinyweshwe Roho mmoja.” (1 Wakorintho 12:12-13).

“Fahamu basi ya kuwa wale walio wa imani, hao ndi wana wa Ibrahimu. Basi ahadi zilinenwa kwa Ibrahimu na kwa mzao wake. Hasemi kwa wazao kana kwamba ni wengi bali kana kamba ni mmoja, kwa mzao wako yaani Kristo .”… “Kwa kuwa ninyi nyote mmekuwa wana wa Mungu kwa njia ya imani katika Kristo Yesu. Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmevaa Kristo. Hapana Myahudi wala Muyunani. Hapana mtumwa wala huru. Hapana mtu mume wala mke. Maana ninyi nyote mmekuwa mmoja katika Kristo Yesu. Na kama ninyi ni wa Kristo, basi, mmekuwa uzao wa Ibrahimu, na warith sawasawa na ahadi” (Wagalatia 3:7,16 26-29).

Paulo anandika tena kuhusu mageuzo yanayotokea wakati wa ubatizo, “Zamani zile mlikuwa hamna Kristo, mmefarakana na jamii ya Israeli, wageni wasio wa maagano ya ahadi ile. Mlikuwa hamna tumaini, hamna Mungu duniani. Lakini sasa, katika Kristo Yesu ninyi mliokuwa mbali hapo kwanza mmekuwa karibu kwa damu yake Kristo.” “Basi tangu sasa ninyi si wageni wala wapitaji, bali ninyi ni wenyeji pamoja na watakatifu, watu wa nyumbani mwake Mungu.” (Waefeso 2:12-13,19).

### 4. Bwana mwingine - Mwito wa Kujitenga.

Soma 2 Wakorintho 6:14-18; 1 Yohana 2:15-17.

Mungu hapendezwi na kupenda kwetu vitu kiasi ya kuviabudu. Watu wa kiume na wa kike wana ulegevu wa kuwa watumwa wa dhambi. Tunapobatizwa tunabadilisha utumishi.

“…tusitumikie dhambi tena. Kwa kuwa yeye aliyekufa amehesabiwa haki mbali na dhambi…..vivyo hivyo ninyi jihesabuni kuwa wafu kwa dhambi na walio hai kwa Mungu katika Kristo Yesu. Basi dhambi isitawale ndani ya miili zenu ipatikanayo na mauti, hata mkazitii tamaa zake…. Hamjui ya kuwa kwake yeye ambaye mnajitoa nafsi zenu kuwa watumwa wake katika kumtii, mmekuwa watumwa wake yule mnayemtii, kwamba ni utumishi wa dhambi uletao mauti, au kwamba ni utumishi wa utii uletao haki.

Lakini Mungu na ashukuriwe kwa maana mlikuwa watumwa wa dhambi, lakini mlitii kwa

mioyo yenu ile namna ya elimu ambayo mliwekwa chini yake; na mlipokwisha kuwekwa huru mbali na dhambi, mkawa watumwa wa haki." (Warumi 6:6-7, 11-12, 16-18)

Katika ubatizo maisha mapya ya utiifu kwa Mungu huanza nayo yatuhusisha na karama ya ahadi ya Mungu.

"Lakini sasa mkiisha kuwekwa huru, na kuwa mbali na dhambi, na kufanywa watumwa wa Mungu, mnayo faida yenu, ndiyo kutakaswa, na mwisho wake ni uzima wa milele. Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti, bali karama ya Mungu ni Uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu." (Warumi 6:22-23).

Tunazikataa njia za mwanadamu katakata! Hizo ni njia za ulimwengu. Katika kukubali kubatizwa twaigeukia njia ya Mungu kuitii Injili – " Nguvu za Mungu ziletazo Wokovu".

### MFANO WA NUHU

Nuhu alifanya haya. Ulimwengu wa nuhu ulijaa udhalimu za maovu. Nuhu akaijenga safina, walimwengu wengine wakipoangamizwa kwa gharika, Nuhu na jamii yake iliokoka.

"Siku za Nuhu, safina ilipokuwa ikitengenezwa; ambamo ndani yake wachache, yaani, watu wanane, waliokoka kwa maji. Mfano wa mambo hayo ni ubatizo, unaowaokoa ninyi pia siku hizi, (siyo kuwekea mbali uchafu wa mwili bali jibu la dhamiri safi mbele za Mungu) kwa kufufuka kwake Yesu Kristo" (1 Petro 3:20-21).

Hukumu kwa wote walio waovu Kristo atakaporudi itakuwa ya ghafla na bila rufani kama ilivyokuwa siku za Nuhu. Kama alivyookolewa Nuhu akiwa safinani nasi pia, ikiwa tumo 'katika Kristo' tutaokolewa. Tumeona mwelekeo wa kuwa katika Kristo ni kupata ufahamu bora, kuamini, kubatizwa na kuendelea kutii.

## UBATIZO UNA UMUHIMU GANI?

Wengi wanaonelea kuwa cha muhimu ni kubadilisha mwenendo wao wa maisha uwe mwadilifu hapana haja ya kitendo hiki cha ubatizo. Ni kosa lilioje; jitihada zao zote za kutenda haki zagonga mwamba. Hebu tafakari juu ya kisa cha Naamani, Jemedari wa jeshi la shamu. (2 Wafalme 5:1-27).

Nabii Elisha, mtu wa Mungu, alimwambia aende akaoge katika mto wa Yordani ili apone ugonjwa wake wa ukoma. Kwanza alikataa, lakini watumishi wake walipomrairai alitii na akatimiza maagizo kama yalivyotolewa na Mungu, akapona mara moja.

Tukitii neno la Mungu kama tunavyoagizwa bila chembe ya uasi, twaweza kupona na kuanza maisha upya. Labda twaweza kuwazia juu ya makosa na dhambi tunayoweza kufanya baadaye, yaani yanatendeka baada ya ubatizo. Kama tulivyoona mwanzoni, katika ubatizo tunaunganishwa kwa mauti ya Yesu Kristo na kitendo hiki kilikuwa cha mara moja tu kama

dhabihu ya dhambi, yale tunayokosea katika maisha yetu mapya yanasamehewa katika sala kupitia kwa mwakozi wetu. Tukitubu na kuomba msamaha, dhambi na makosa yetu yote hufutiliwa mbali kutoka rekodi zote na kuendelea mbele na safari yetu kwa ujasiri ikiwa tutajitahidi kutenda haki; Mungu ameahidi kutusamehe kwa rehema zake nyingi.

Mungu ametupa nafasi hii ya ajabu kupitia kwa Neno Lake. Je, waona kuwa waweza kutaka kuanza maisha yako upya? Kwa ujuzi wa maisha uliyo nayo, yaliyojaa makosa uliofanya na hamu ya kutaka kufutilia mbali madoadoa yanayosawiri maisha yako ya kwanza, sasa una nafasi ya kuanza upya. Maisha mapya yanaanza kwa mkondo tofauti na wa awali, sio kuelekea kaburini bali kufuata njia iendayo kwenye hali ya mwili kutoharibika na ufalme wa Mungu wenye utukufu. Njia ya Mungu ndiyo njia ya pekee ya kupata upatanisho na Muumba wako.

Hii ndiyo faida kuu ya Ubatizo. Ni kitendo muhimu cha utii, hatua maalum ya njia ya Mungu ya kupata wokovu.

## MUHTASARI

1. Ubatizo ufanyike baada ya kuelewa kikamilifu na kuamini injili.

2. Kumchovya mtu majini, ndio ubatizo hasa.

3. Kitendo cha ubatizo kinachangia yafuatayo;

    - Dhambi zetu zinaoshwa kwa mfano.

    - Tunaunganishwa kwa kifo na ufufuo wa Bwana Yesu Kristo.

    - Tunaunganika katika Kristo, na tunahusishwa na ahadi za Mungu kupitia kwa Kristo.

    - Tunabadilisha utumishi wetu - tunamtumikia Mungu badala ya kutumikia dhambi na twajitenga na ulimwengu.

4. Kama vile Nuhu alivyookolewa kwa kuingia katika safina, twaingia katika Kristo kwa njia ya ubatizo ili tupate kuokolewa kutoka kwa hukumu ilayo.

5. Ubatizo ni muhimu kwa kupata wokovu.

**VIFUNGU VYA KUSOMA KATIKA BIBLIA**

- Mwanzo 6,7 na 8
- Marko 16
- Matendo 8 na 22

**KITIHANI CHA SOMO LA 11**

Pigia mstari jibu lililo sahihi kwa kila swali lililoulizwa kisha uhamishe majibu hadi hati ya muhtasari ya majibu iliyo katikati ya kurasa za hizi.

1. Neno “ubatizo” lima maana gani?
   (a) Nyunyuzia
   (b) Mwagilia
   (c) Chovya
   (d) Lowesha
2. Ni nani aliyembatiza towashi kutoka Ethiopia?
   (a) Stefano
   (b) Paulo
   (c) Filipo
   (d) Barnaba
3. Ni kifungu kipi cha Biblia kinachotueleza maagizo waliyopewa wanafunzi ya kuhubiri injili?
   (a) Marko 15:15-16
   (b) Marko 16:15-16
   (c) Marko 5:15-16
   (d) Marko 6:15-16
4. Chagua watatu kati ya hawa waliobatizwa.

(a) Pilato

(b) Paulo

(c) Mlinzi wa gereza, Filipi

(d) Lydia

5. Ni wakati gani ubatizo wa kweli wafaa kufanywa?

(a) Wakai wa kufa

(b) Wakati wa kuzaliwa

(c) Utakapotoka shuleni

(d) Unapopata ufahamu kamili na kuamini mpango wa Mungu kuhusu uokovu.

6. Kitendo cha ubatizo kinawakilisha nini?

(a) Karama ya Mungu

(b) Kifo hasa cha mtu

(c) Safina ya Nuhu

(d) Kufa na kufufuka kwa Yesu.

7. Ni mlango upi katika Biblia watoa wazi maana ya Ubatizo?

(a) Warumi 6

(b) Ruth 4

(c) Ufunuo 6

(d) Wakolosai 4

8. Ni tukio gani analotumia Petro kutuonyesha usambamba wa Ubatizo?

(a) Kupita bahari ya shamu wakati wa kutoka

(b) Kuvuka kwa mto wa Yordani na kuingia Nchi ya Ahadi

(c) Kutolewa kwa maji jangwani

(d) Kutolewa kwa Safina na Nuhu wakati wa gharika

9. Ni kitendo kipi cha utiifu unachohitajika kutenda ili upate nafasi katika Ufalme wa Mungu ujao?

(a) Upendo

(b) Imani

(c) Kuamini na kubatizwa

(d) Uaminifu

10. Je, ungependa kujifunza zaidi ujumbe wa Mungu ili upate ufahamu kamili wa kukuwezesha ubatizwe?

(a) Ndio

(b) La

(c) Sina hakika

(d) Labda

SOMO LA 12

# UFALME WA MUNGU

Kristo atakaporudi - somo tangulizi laonyesha tukio hilo latarajiwa wakati wowote ule - kazi yake ya kwanza itakuwa ni kuwafufua wafu.

“Tena, wengi wa hao walalao katika mavumbi ya nchi wataamka” (Danieli 12:2).

“Kwa kuwa twaambieni haya kwa neno la Bwana, kwamba sisi tulio hai, tutakaosalia hata wakati wa kuja kwake Bwana, hakika hatutawatangulia wale waliokwisha kulala mauti. Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza” (1 Wathesalonike 4:15-16).

Hukumu itafuata kisha wenye haki watatunukiwa na uzima wa milele na kupewa jukumu la kumsaidia Yesu katika kutawala ufalme wa Mungu,

Biblia yatoa ahadi kuwa maovu yanayoukumba ulimwengu huu yataondolewa pindi Kristo ashikapo usukani wa uongozi.

## HALI ITAKAVYO KUWA KATIKA UFALME

Hapatakuwepo na ukandamizaji (Zaburi 72:4) wala vita tena.

“Naye atafanya hukumu katika mataifa mengi, atawakemea watu wa kabila nyingi nao watafUa panga zao ziwe majembe, na mikuki yao iwe miundu; taifa halitainua upanga juu ya taifa lingine wala hawatajifunza vita tena kamwe” (Isaya 2:4).

Utawala wa Mfalme utakuwa wa kweli na haki:

“Hatahukumu kwa kuyafuata ayaonayo kwa macho yake, wala hataonya kwa kuyafuata ayasikiayo kwa masikio yake, bali kwa haki atawahukumu maskini naye atawaonya wanyenyekevu wa dunia kwa adili” (Isaya 11:3-4).

Magonjwa yatasitishwa na laana ya maradhi na ndwele yataondolewa.

“Ndipo macho ya vipofu yatafumbuliwa, na masikio ya viziwi yatazibuliwa. Ndipo mtu aliye kilema atarukaruka kama kulungu na ulimi wake aliye bubu utaimba” (Isaya 35:5-6).

Nchi nyingi kwa sasa zinateseka kwa sababu ya gumba (njaa) na maelfu ya watu wanaokufa kila siku kwa njaa. Siku hiyo hapatakuwepo na njaa tena. Vijito vya maji katika jangwe vitafanya mimea ipate kukua kotekote.

“Maana katika nyika, maji yatabubujika, na vijito jangwani. Na mchanga ung’aao mfano wa maji utakuwa ziwa la maji,na nchi yenye kiu itakuwa chemchemi za maji” (Isaya 35:6-7).

“Na uwepo wingi wa nafaka katika ardhi juu ya milima; matunda yake na yawayewaye kama Lebanoni” (Zaburi 72:16).

Mwishowe, kifo kitaondolewa kabisa.

“Hapo ndipo mwisho atakapompa Mungu Baba Ufalme wake; atakapobadilisha utawala wote, na mamlaka yote na nguvu. Maana sharti amiliki yeye hata awaweke maadui wake wote chini ya miguu yake. Adui wa mwisho atakayebatilishwa ni mauti.” (1 Wakorintho 15:24-26).

“Naye atafuta kila chozi katika macho yao, wala mauti haitakuwepo tena; wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu hayatakuwepo tena; kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita” (Ufunuo 21:4).

Sasa ni bayana kwa nini mafunzo haya kuhusu ufalme wa Mungu kuitwa injili - tumejifunza ya kuwa neno hili linamaanisha ‘Habari Njema’

# WOKOVU

Baada ya ufufuo wake, Yesu aliwatuma wanafunzi wake akiwaagiza kuwa, “Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka” (Marko 16:15-16).

Yaonekana kuwa kinachotangulia ubatizo ni kuamini injili. Kifungu hicho chaendelea –

“asiyeamini, atahukumiwa”.

Siku ya Pendekoste, mtume Petro alizungumzia juu ya ufufuo wake na kurudi kwake Mara ya Pili. Waliosikiliza hotuba yake waliguswa na yale walioyasikia na wakataka kujua wafanye nini. Waliambiwa watubu na wabatizwe. Kutubu, ni kugeuza mawazo yako - kuanza mambo mapya.

“Nao waliolipokea neno lake watabatizwa…wakawa wakidumu katika fundisho la mutume, na katika ushirika na katika kuumega mkate na katika kusali”. (Matendo 2:41,42).

Angalia, utaratibu wa hatua ni uleule- ufahamu na imani, inafuatiwa na utii utaokupeleka katika maji ya ubatizo. Yanayofuatia ni jitihada za waumini kuishi maisha mema kwa njia ya kumpendeza Mungu.

Mfuasi wa Yesu ambaye amebatizwa, anayesemekana amefufuka na Kristo, anaweza kuishi kwa uhakikisho wa kumsubiri Bwana arudi.

“Basi mkiwa mmefuufuliwa pamoja na Kristo, yatafuteni yaliyo juu Kristo aliko, ameketi mkono wa kuume wa Mungu. Yafikirini yaliyo juu, siyo yaliyo katika nchi. Kwa maana mlikufa, na uhai wenu umefichwa pamoja na Kristo katika Mungu. Kristo atakapofufuliwa, aliye uhai wetu ndipo na ninyi mtafufuliwa pamoja naye katika utukufu” (Wakolosai 3:1-4).

## MSAMAHA

Ikiwa, katika wakati huu wakumsubiri Kristo, mfuasi wake atakosea, anafahamu kuwa Yesu ni wakili wake mwenye rehema na atamtetea kwani anajua majaribu ni nini. Katika waraka kwa Waebrania, twakumbushwa ya kuwa kuhani wetu Mkuu alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, ingawa yeye hakushindwa, hakufanya dhambi. (Waebrania 4:15) Unaweza kuwa na matumaini kuwa maombi yako kama jamaa wa Kristo, yatasikika.

“Basi na tukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri, ili tupewe rehema na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji” (Waebrania 4:16).

## KARAMA YA MUNGU

Hatuwezi lolote kwa nguvu zetu wenyewe. Ni kwa mapenzi na rehema ya zake Mwenyezi Mungu ndipo twapata wokovu kupitia kwa Kristo. Ndipo mtume Paulo akaandika: “Kwa maana mmekuokolewa kwa neema , kwa njia ya imani ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu” (Waefeso 2:8).

“Karama ya Mungu ni uzima wa Milele katika Kristo Yesu Bwana wetu” (Warumi 6:23).

## HATUA NYINGINE

Sasa umekamilisha masomo kumi na mbili ya mafunzo haya. Umepata kwa kiasi fulani kujua yale ambayo Biblia inafunza kuhusiana na mpango wake na nchi. Kuna uwezekano wa wewe kuwa mmojawapo wa wale watu wa Athene, walimsikiliza Paulo na “waliposikia habari za ufufuo wa wafu wengine walifanya dhihaka; wengine wakasema, tutakusikiliza tena katika habari hiyo.” (Matendo 17:32). Kwa uneni mwingine twaweza kusema, walifurahia kumsikiliza lakini hawakuwa na tamaa ya kuendelea na masomo.

Waweza kuwa kama watu wa Beroya aliowatembelea mtume, ambao “Walilipokea lile neno kwa uelekevu wa moyo, wakayachunguza maandiko kila siku waone kwamba mambo haya ndivyo yalivyo.” (Matendo 17:11).

Kwa kundi lolote lile unaloweza kuwamo, mpango na kusudi la Mungu halina budi kutimia. Petro aliandika kuwa katika siku za mwisho watu watadhihaki dhana ya kurudi kwake Kristo. Petro anasema walidharau na kupuuzilia mbali mahubiri ya Nuhu lakini wakati uliowekwa ulipowadia, mvua ilikunya. Hali kadhalika watu watambue au wapuuze, “Siku ya Bwana itakuja” (2 Petro 3:9-10).

# UJUMBE MAALUM KWAKO WEWE

Mtume anahitimisha waraka wake kwa kusema, mnapofahamu hivi:

“Imewapasa ninyi kuwa watu wa tabia gani katika mwenendo mtakatifu na utauwa?” (2 Petro 3:11).

Swali hili twamwachia kili mwanafunzi alijibu kibunafsi yeye mwenyewe. Ni imani yetu kuwa mtafanya “bidii ili mwonekane katika amani kuwa hamna mawaa wala aibu mbele yake.” (2 Petro 3:14).

**Vifungu Vya Kusoma Kutoka Katika Biblia**

Isaya 65:17-25, 66:1-2

Waefeso 2 na 5

Warumi 13

Wakolosai 3

2 Petro 3.

**KITIHANI CHA SOMO LA 12.**

Pigia mstari jibu lililo sahihi kwa kila swali lililoulizwa kisha uhamishe majibu hadi hati ya muhtasari ya majibu iliyo katikati ya kurasa za hizi.

1. Kazi ya kwanza atakayoifanya Yesu akarudi duniani ni?
   (a) Kuwambia wote kuwa amerudi
   (b) Kufufua wafu
   (c) Kuwapa raha wote
   (d) Kuwaangamiza waovu

2. Ni hali gani itaonekana katika Ufalme wa Mungu?
   (a) Vita vitakoma
   (b) Magojwa yatatoweka
   (c) Njaa na ukame havitakuwepo
3. Ni wakati wa sherehe gani Petro alizungumzia kurudi kwa Yesu kama ilivyorekodiwa katika Matendo 2?
   (a) Pasaka
   (b) Pentekote
   (c) Usafi
   (d) Sikukuu ya vibanda
4. Muumini aliyebatizwa anafaa kuishi maisha ya namna gani?
   (a) Utawa
   (b) Kipekee
   (c) Katika namna ya kupendeza Mungu
   (d) Awe na kazi bora
5. Mfuasi wa Yesu anaweza kuomba msamaha kivipi?
   (a) Kwa kutoa dhabihu
   (b) Zaka
   (c) Matoleo
   (d) Kwa maombi
6. Karama ya Mungu inayotajwa katika Warumi 6 ni nini?
   (a) Uzima wa milele katika Kristo
   (b) Uumbaji
   (c) Biblia
   (d) Majira
7. Watu wa Athene walifanya nini waliposikia Paulo akihubiri?
   (a) Walimpiga mawe
   (b) Walisema, 'tutasikia zaidi wakati mwingine'
   (c) Walimsifu Paulo
   (d) Walimtukuza Paulo
8. Watu wa Beroya walifanya nini walipomsikiza Paulo akihubiri?
   (a) Waliimba nyimbo za sifa
   (b) Walichunguza maandiko kila siku
   (c) Walihubiri
   (d) Waliuza mali yao
9. Ni mambo yepi ambayo Wanadamu hawawezi kuyazuia yasitukie?
   (a) Uchafuzi
   (b) Kusimamishwa kwa ufalme wa Mungu
   (c) Chuki
   (d) Kurudi kwa Yesu.

**10. Ni mtume yupi wa Yesu alijaribu kutwambia tusiwe na lawama katika maisha yetu mbele za Mungu?**

(a) Paulo
(b) Filipo
(c) Yohana
(d) Petro

Kama umefurahia kitabu hiki na ungependa kuendeleza masomo yako, kuna kitabu kingine kiitwacho **MISINGI WA BIBLIA** kinachoweza kutupatikana kutoka kwa anwani hii:

Christadelphian Advancement Trust
P.O Box 3034,
SOUTH CROYDON
SURREY,
CR2 OZA,
ENGLAND
Wavuti: www.Carelinks.net

Baruapepe: info@carelinks.net